Jumatatu Novemba 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581143
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US






**Mshtuko** watoto kudungwa sindano za kuzuia ujauzito

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wanaume wafichua maficho ya ukatili

UKURASA 2



Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye akiwa kwenye mazungumzo na ujumbe wa Benki ya CRDB ulioongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Ally Laay na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa nne kushoto), ulipomtembelea kwenye makazi yake Kiriri, Bujumbura. Mkutano huo ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 10 ya kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Burundi, ambayo kilele chake kilikuwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rais Samia aonya watunza kumbukumbu mafao wastaafu

UKURASA 2



## Raia wa Ukraine aliyekwama Zanzibar asimulia yaliyomkuta

UKURASA 4

**MICHEZO** NABI APIGA MBILI KWA MOJA YANGA UK.32 **KATUNI** UK.6

# Wanaume wafichua maficho ya ukatili

Na Salome Kitomari

WANAUME wametaja vichocheo vya matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kwenye jamii yanayotokea sasa ni kutaka kuonyesha nguvu walizonazo na kuachwa nyuma kwenye mipango, sera na mikakati ya nchi.

Aidha, wamesema ni muhimu sera, mipango na mikakati yote ya nchi ikajumuisha wanaume na wanawake, huku wakitaka kuanzishwa kwa majukwaa ya wanaume ngazi ya mtaa, kijiji hadi taifa ili waeleze matatizo wanayopitia.

Wanaume zaidi ya 30 walisema hayo mwishoni mwa wiki walipokutanishwa kujadili chanzo cha ukatili wa kijinsia na nini kifanyike katika mdahalo ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), katika siku 16 za kupinga ukatili.

Mwakilishi kutoka Gender Health, Dk. Katanta Simwanzi, alisema wanaume wanaofanya kazi ambazo hazijazoeleka katika jamii kama kumsaidia mkewe anaonekana hana nguvu au amelogwa.

"Wanaume tuliambiwa tusilie, kuna rafiki yangu alifiwa na baba yake akawa analia alifuatwa na wanaume wengine akaambiwa wewe ni mwanaume hutakiwi kulia, kila nikionana naye ananiambia natamani kulia kwa kuwa sikupata nafasi ya kulia siku ya msiba wa baba yangu. Wanaume tumenyimwa fursa ya kuonyesha hisia zetu tunaambiwa tuvumilie ndio uanaume, tusikubali hizi sifa," alisema.

Wakili Severine Allute, alisema kikao cha Beijing nchini China, kiliwasahau wanaume na kuja na mikakati ya kumkuza mwanamke kwa nyanja zote ndio maana mipango, mikakati mingi imejikita kumpa fursa mwanamke na kumuacha nyuma mwanaume.

"Nguvu ya kiuchumi ni tatizo kubwa kwa wanaume wengi, wanawake wameinuka sana kwa sasa, mtu anapokuwa na nguvu kiuchumi anashirikiana na wanaofanana naye. Mwanaume anaona aheshimiwe kwenye familia, watoto hawamuheshimu kwasababu ni mnyonge na mama anajiweza kiuchumi," alisema.

Alisema ujengaji wa uwezo ulifanyika upande mmoja na hasira ya wanaume hujitokeza anapoona anadharaulika kwa sababu hana kipato, nguvu zake hazionekani na kuheshimika ndipo ukatili hutokea kwasababu anataka nafasi yake ionekane.

Mtaalamu wa Vimbwembwezo (IT), Ikundwila Mwambona, alisema tangu zamani wanaume walipewa majukumu mazito kama kwenda vitani, kazi ngumu wakijengwa kisaikolojia kwamba ni wenye nguvu na wanatakiwa kusikilizwa, lakini sasa dunia imebadilika.

"Tupo kwenye utandawazi siku hizi jinsia zote zina nguvu, zamani wakati nakua ilikuwa mama akitaka kukutisha anakwambia nitamwambia baba yako akija, na kweli akija anakusema unatandikwa, hivyo unamuona baba ni mbaya na mama mzuri."

"Kwenye makundi songezi ya wanaume tunayojadiliana ni mambo ambayo hayatusaidii bali kuonyesha misuli yetu, tunatumia mabavu kupata mamlaka yetu wakati inatakiwa tuendeshe maisha pamoja kwa kujadiliana na kukubaliana. Tunategemeana, hakuna aliyejizaa na hakuna aliyejipa mimba mwenyewe," alisema.

Akichangia mjadala huo, Juma Rashid alisema; "mifumo ya jamii ilitujenga kwamba sisi ndio kila kitu, unadharaulika wakati mwingine unaitwa mwanaume suruali, ukiona unadharaulika hivyo ujue kuna mahali ulikosea, unarudi nyumbani umelewa chakari, unavua nguo mbele ya watu na watoto nani atakuheshimu?"

"Kuwa kichwa cha familia sio kumpiga mke, kwa sasa matukio yote mabaya ni wanaume wanatajwa lazima tujitathmini tunakosea wapi, lazima tuishi kwa kushirikiana badala ya kulipiza kisasi kwa kuwapiga, kuwajeruhi au hata kuua.

James Maduka, alisema mfumo ndio tatizo kubwa huku akirejelea wakati wanakua nyumbani kwao walikuwa na jina la kikatili wanamuita baba yao, na wakifanya kosa lolote baba akiambiwa aliwaadhibu hali iliyozidi kujenga umbali naye.

Joseph Msendo, alisema sera na sheria zinawapa nguvu na kuwalinda wanawake zaidi akitoa mfano wazazi wanapotengana baba haruhusiwi kumlea mwanawe hadi afikishe umri fulani, wakati mama anaruhusiwa kuwa naye tangu mdogo.

Wakili wa kujitegemea, Mlowe Pasience, alisema maandiko matakatifu yameelekeza wanaume kuishi kwa upendo na wake zao, wanapokosa kuyatimiza matatizo yanaanza na kuona hapewi heshima kama kichwa cha familia.

"Umeoa, lakini unaendelea kuishi maisha ya ubachela, unahama baa moja kwenda nyingine wa washikaji ambao hawana familia, unarudi asubuhi ukiombwa fedha unasema huna ila unalewa, ukijibiwa vibaya unarusha ngumi na kumnyanyasa mkeo na watoto, huu ni katili, lazima turudi kwenye upendo," alisema.

Aidha, alisema chanzo kingine cha ukatili ni umaskini na utajiri kwamba maskini anamuumiza mkewe kwa kipigo kwasababu kaombwa fedha naye hana, tajiri anampiga mkewe kihisia kwamba atakuwa na wanawake wengi.

Wakili huyo alisema vijana hawaandaliwi kuingia kwenye ndoa bali wanatumia sababu za kwamba amepata mimba, msukumo wa jamii au umri umekwenda, ndio maana wanaendelea kuishi maisha ya ujana ikiwamo kuwa na mchepuko ambao ni gharama kwake.

Naye Zenno Ngowi alisema; "ukitaka watoto wakupende mpende mama yao, muwe na vikao vya mara kwa mara vya familia kuzungumza kwa uwazi, kushirikiana kwa uwazi kuendesha maisha, wanaume tuwe wakweli kwa familia zetu kuanzia kipato na kila kitu, tusiishi maisha ya kudanganya."

Naye Azam Zahoro alisema hali ya uchumi ni kikwazo kikubwa kwa wanaume na kwamba wanawake wengi wana vikundi wanawezeshana. "Anakuomba fedha kila siku huna, hajui mshahara wako ila unalewa, akikuita mwanaume suruali unarusha ngumi, lazima tujijenge kiuchumi."

Mchambuzi wa Uwekezaji, Moshi Elinaja alisema wanaume wengi hawako makini na mfano ni siku ya wababa huoni anayesema lolote kwa kuamini wataonekana ni dhaifu au wanapigania haki, huku siku ya wanawake kuna shamrashamra nyingi wanaweka mikakati ya kujiendeleza kiuchumi.

"Wanawake wana VIKOBA wanapeana mikopo mikubwa, zamani tuliwanyanyasa kiuchumi na kimila ila kwa sasa kiuchumi wako vizuri, ukiambiwa mwanaume suruali unarusha ngumi wakati ni kweli huna fedha. Nimesoma mahali kuwa ikifika 2050 tutaanza kupigania haki za wanaume," alisema.

## Rais Samia aonya watunza kumbukumbu mafao wastaafu

Na Waandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaagiza watunza kumbukumbu na nyaraka nchini kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uaminifu na uadilifu mkubwa ili wasiwe chanzo cha watu wengi hasa wastaafu kukosa haki zao.

Aidha, amewataka kutunza siri za serikali kwa mujibu wa sheria na taratibu, kwa kuwa baadhi wanavujisha mitandaoni.

Amemwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Jenister Mhagama, kushirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haruni Ally Suleiman, kuandaa mkutano mkuu maalum wa watunza kumbukumbu na nyaraka nchini (TRAMPA) na Makatibu Makhussi (TAPSEA) kwa ajili ya kula kiapo cha uaminifu.

Akifungua Mkutano wa 10 wa TRAMPA, jijini Arusha, Rais Samia alisema tasnia hiyo ni roho ya serikali na kitovu cha mafanikio.



Alisema wananchi wengi hasa wastaafu wameingia katika kadhia ya kucheleweshewa au kutopata stahiki zao kutokana na uzembe wa kutoweka kumbukumbu za nyaraka vizuri unaofanywa na baadhi ya watumishi hao hali inayosababisha baadhi kupata msongo wa mawazo, maradhi ya moyo na hatimaye kufariki.

"Serikali inatambua umuhimu wenu na tutawalinda, wastaafu wanapofuata stahiki zao kwenye mifuko ya hifadhi ya kijamii kama hakuna kumbukumbu wanapoteza stahiki zao, anajifia bila kupata haki yake," alisema.

"Lakini angalia mfano mwingine, wewe ni mtunza kumbukumbu wa ajira za watu, unakwenda kupoteza kumbukumbu za watu, unaweka ovyo hazionekani, watu wanastaafu wanatayarishiwa karatasi zao kila kitu, anakwenda NSSF, PSSSF anafika kule anaambiwa taarifa zako hakuna, sasa embu vaa viatu vya huyu mtu."

Rais Samia alisema maendeleo ya teknolojia yameboresha huduma ya utunzaji wa kumbukumbu na kumrahisishia mtumishi kazi na kukitaka chama hicho kuendelea kuwekeza katika teknolojia hiyo ili kuendelea kurahisisha upatikanaji wa nyaraka na utekelezaji wa majukumu ya kiserikali.

"Sisi tulivyokuwa watunza kumbukumbu tulikuwa hatuna vitendea kazi mlivyonavyo nyie leo, tulikuwa tukiandika kumbukumbu namba ya faili wenyewe, kwa mwandiko maalum, unapanga kwenye kabati mwenyewe, barua zote unaziweka na kuzijua mwenyewe, lakini nyie leo mna makompyuta, kila kitu mnaweka huko na kwenye makabati mnaweka, hakuna sababu ya kuharibu kazi," alisisitiza.

Kuhusu kutunza siri za serikali, alisema: "Siku hizi tunaona siri za serikali hususani mahakamani zinavuja kwenye mitandao, hilo halitakufikisha mbali unayevujisha zaidi unafanya uchonganishi."

Alisema utunzaji mzuri wa kumbumbuku unaimarisha huduma za umma na kuleta mafanikio kwa kila mmoja.

"Kweli kuna umuhimu wa kula kiapo kutokana na kazi zenu mnazofanya ila hakizuii kwenda kinyume sababu sio wote wanaokula kiapo wanatenda mema," alisema.

Aliagiza mamlaka kumkabidhi kiwanja jijini Dodoma, Mwenyekiti wa TRAMPA, Josephine Manase kwa ajili ya kujenga kituo cha kuongeza ujuzi kwa kada hiyo.

"Lakini kiwanja nawapatia msitake tena kurudi kwangu, kuomba na fedha za ujenzi mimi mchango wangu natoa kiwanja sababu nyie ni wenzangu nilifanya kazi hii Zanzibar katika uadilifu na uaminifu mkubwa," alisema.

Alisema kuna changamoto za waajiri nchini katika matumizi ya teknolojia ya utunzaji wa kumbukumbu. Na kuwaagiza waajiriwa sekta binafsi na umma kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu, ikiwamo kuwapandisha madaraja.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haruni Ally Suleiman, alisema TRAMPA ni sekta muhimu nchini ya kuimarisha muungano.

"TRAMPA ni sekta muhimu hapa nchini kwa sababu wanatunza siri kubwa kwa serikali, ifike wakati tuangalie namna ya watumishi wa sekta hii kula kiapo cha uadilifu," alisema.

Waziri wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mhagama, alisema lipo tatizo kubwa la madaraja ya watunza kumbukumbu nchini na kwa miaka yote watunza kumbuku wa stashahada na astashahada walikuwa kila daraja moja na Rais ameagiza kutenganisha kwa daraja la astashahada na stashahada na kumwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro, kukamilisha kanuni za kutekeleza agizo la Rais.

Pia alisema katika mwaka 2022/2023 serikali imetenga bajeti ya kutoa ajira 30,000 zitakazotangazwa katika kada hiyo na hata kama hawataajiriwa wote mwaka ujao wa fedha walio na shahada wataajiriwa.

Awali Mwenyekiti wa TRAMPA, Manase alisema chama hicho kimepata mafanikio kwa kuongeza wanachama kutoka 149 mwaka 2012 hadi 45,000 mwaka huu, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watunza kumbukumbu hai ili kuwajengea uwezo.

***Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Jenipher Gilla (DAR)**

## HABARI KITAIFA

# TANESCO: Makali mgawo umeme kuendelea kupungua

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema makali ya mgawo wa umeme yanaendelea kupungua, baada ya megawati 350 zilizopungua siku za hivi karibuni kuanza kurejea na wiki ijayo zitaendelea kushuka hadi megawati 100.

Aidha, limesema hadi Februari mwaka huu hakutakuwa na mgawo wowote kutokana na kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I kuongeza upatikanaji wa nishati hiyo kwa uhakika zaidi.

Shirika hilo lilitoa ahadi hiyo katika mdahalo wa mtandaoni kupitia Twiter uliouandaa na kushirikisha wananchi ambao wamewataka wanasiasa kukaa kando na kuwaacha watendaji kufanyakazi zao kitaalamu, ili kuwa na suluhisho la kudumu la matatizo ya umeme nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande (pichamni), wakati akijibu maswali ya wananchi kupitia mdahalo huo wa kumekucha, uliojumuisha zaidi ya watu 1,000 alitoa nafasi ya watu kuuliza maswali na kujibiwa papo hapo. Alisema TANESCO itaendelea kusema ukweli na kutatua kero za wananchi kwa wakati bila kujali mazingira kwa kuwa lengo ni huduma nzuri, yenye kuridhisha na tija kwa nchi.

Chande alisema mahitaji ya umeme yanazidi kuongezeka, wateja wapya wanaongezeka kila siku, miezi sita iliyopita hakukuwa na hii presha, lakini ukame umefanya hali kuwa ngumu zaidi.

Hata hivyo, alisema mvua zimeanza kunyesha na vituo kama Kidatu na Iyovu maji yameongezeka, hadi Desemba kutakuwa na hali nzuri zaidi.

Mbunge wa Jimbo la Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo, aliwataka wanasiasa kujenga utamaduni wa kuwapa wataalamu nafasi, kutokana na ukweli kuwa wamejipanga vizuri na baadhi ya wanasiasa wanawatoa kwenye msimamo.

"Tunawaomba wanasiasa hawa wataalamu wapewe nafasi, haya mambo ya zimamoto hayatasaidia nchi," alisisitiza.

Aliitaka TANESCO kuwa na msimamo wa sababu za kukatika kwa umeme kwa kufanya utafiti kabla ya kueleza umma, ili wanasiasa wanapozungumza kwa wananchi waweze kueleweka.

"Kero ni adui wa mipango ya kesho ni sawa na kuwa na chawa kichwani au kunguni mwilini lazima utajikuna, shughulikieni kero ndogondogo ziondoke, mwananchi akiwa na kero akienda kwa mwanasiasa anataka atoe majibu hataangalia mipango. Kero za umeme kwa kusababu ya uzembe zikae kando sasa," alisema.

Akijibu hoja hizo, Chande alisema "Tanesco tutajitahi tuwe wa kweli, ndio maana tunakuwa wazi kusema hata kama itasababisha tatizo fulani, lakini ndio namna ya kusonga mbele, ukisema uongo utasema huu na kesho utasema ule, tunapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wizara na nitahakikisha tunatekeleza kwa umahiri na kwa dhati ili tusiwaangushe wateja."



**BIASHARA YA MAJENERETA**

Aidha, mwananchi mmoja aliuliza kuhusu madai ya kufungua maji kwenye mabwawa ili waruhusu kushamiri kwa biashara ya majenereta.

Chande alisema takwimu zinaonyesha mwaka 2011 na 2015 kulikuwa na ukame mkali, pia 2016, 2017 na 2018 ulikuwa wa wastani, lakini kilichofanyika ni kuwanyima umeme wazalishaji wakubwa na kuwapa wananchi hali iliyoonyesha hakuna shida ya umeme.

Alifafanua kuwa mabwawa yanapojaa maji na kufunguliwa ni kuzuia lisipasuke, kitaalamu maji hufunguliwa na kamati za vijiji na usalama zinahusishwa, pia mageti yanaendeshwa kielektroniki yananakiri nani kafungua, sio rahisi mtu kufungua kwa nia ovu.

"Kusema tunafungua mageti ili maji yaishe ili kushamirisha biashara ya majenereta sio kweli, kitaalamu maji yanapojaa tunayafungulia bila kuathiri uzalishaji. Mtu anapofungulia ili kuruhusu majenereta ni kiwango cha juu sana cha utovu wa maadili nasi TANESCO hatuwezi kukubali hilo kutokea," alisema.

Naye Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alitaka kujua ni lini serikali itaruhusu sekta binafsi kuwekeza kwenye gesi ya Mtwara, Somanga Fungu na Kinyerezi, pia lini watajiunga kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSA).

Chande alisema watu binafsi kuruhusiwa kuwekeza kwenye nishati kumekuwa na kusuasua kutokana na historia ya uongo kuliko uhalisia hali iliyozalisha maneno mengi, kutafutana tafutana kwa watendaji jambo lililowaogopesha na kurudi nyuma.

"Tunaposaini mikataba na sekta binafsi tunaweka wazi na tutakuwa tayari kusimamia kile tulichokubaliana hadi tunaingia karibuni, mambo yako wazi sana kwa sasa lazima mkubaliane muundo wa uwekezaji, faida na hasara. DSA tutajiunga pale mapato yetu yatakapokuwa imara na vitabu vyetu kuwa sawa."

Alisema TANESCO inakwenda dijitali zaidi na ndio maana imetoka kutumia rimu 3,000 za karatasi kwa mwaka, pia kutoka kuwa na watumishi 30 hadi watatu wa kufanya kazi hiyo na mwakani wateja wengi watafikiwa na 'smart meter" ambazo itakuwa ngumu kuzichezea na kuhujumu mapato ya shirika.

Akijibu swali la mwananchi mwingine aliyetaka kujua mipango ya baadaye ya kuwa na nishati ya uhakika, Chande alisema mahitaji ya lazima ni megawati 8,000 na nchi ikizifikia hakutakuwa na shida, huku malengo ya karibuni ni megawati 4,000 hadi 5,000 ifikapo 2025.

# Mshtuko watoto kudungwa sindano za kuzuia ujauzito

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya Ruangwa ameeleza kusikitishwa na vitendo vya baadhi ya wazazi kulazimisha watoto wa kike kuchomwa sindano za kuzuia kupata ujauzito.

Hassani Ngoma amesema vitendo hivyo vinachangia wanawake katika mikoa ya Lindi na Mtwara kuwa hatarini kukumbwa na tatizo la utasa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mdahalo wa kujadili kero zinazowakabili vijana, wakiwamo wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) katika maadhimisho Wiki ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa mwaka huu yanafanyika mkoani Lindi.

Ngoma alisema maambukizi mapya ya VVU yanayoendelea kuongezeka hivi sasa, yanatokana na kundi la vijana wa kiume na wa kike kutokuwa na hofu ya Mungu na kubeza matumizi ya mipira ya kiume na kike.

Aliyataja mambo mengine yanayochangia kuongezeka kwa tatizo hilo ni pamoja na kushamili kwa matumizi ya sindano za kuzuia ujauzito, huduma inayoendelea kutolewa maeneo mbalimbali ya vituo vya kutolea huduma za afya na maduka ya dawa muhimu.

Alisema kuwa katika wilaya anayoiongoza, amebaini watoto wa kike walio na umri kuanzia miaka minane hadi 13 wanachomwa sindano za kuzuia wasipate ujauzito, huku wazazi wakidaiwa kuweka msisitizo kwa vijana wao kuchomwa sindano za aina hiyo, jambo alilosisitiza si sahihi na ni hatari katika kuchochea maambukizi ya VVU na ugumba.

"Watoto wa kike hivi sasa hawahitaji matumizi ya kondomu kutokana na matumizi ya sindano ya kuzuia kupata ujauzito," alifafanua.

Ngoma alisema hali hiyo isipodhibitiwa, kuna hatari ya kuongezeka kwa maambukizi ya VVU, huku kiwango cha kuzaliana kusini mwa Tanzania kikishuka.

Alisema kutokana na hali hiyo, baadhi ya shule zikiwamo za msingi ndani ya Wilaya ya Ruangwa zimekuwa na idadi ndogo ya wanafunzi, akiitolea mfano moja ya shule hizo yenye wanafunzi 126.

"Baadhi ya shule wanafunzi wanaomaliza elimu ya darasa la saba ni kati ya saba na wanane kutokana na kushiriki zaidi mapenzi kuliko masomo," alisema Ngoma.

Awali akieleza hali ya maambukizi ya VVU wakati wa mdahalo huo, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema maambukizi yameendelea kupungua na yalivyopo kwa sasa idadi kubwa ipo kwa vijana kwa asilimia 30 huku wasichana wakiongoza kwa asilimia 80.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na 229/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SARA CATHERINE FUBUSA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA CHARLES FRANK FUBUSA**
**TANGAZO**
**( kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 1 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo Tarehe 24 mwezi 11 mwaka 2022**

HAKIMU

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ANTHONY .K. CHOYA.** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.125 AGZ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/RB/ 771/ 2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MTWARA**
**LILILOPO MTWARA**
**MAOMBI MADOGO NA 902/2021**
**NMB BANK PLC..............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**HAWTE INVESTMENT LIMITED............MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**HAWTE INVESTMENT LIMITED, POPOTE ULIPO,**

**UFAHAMU** kwamb shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 28, Novemba 2022 saa 2:30 asubuhi.
**UNAAMRIWA** kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Baraza idaya ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.
**FAHAMU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litapangiwa kusikilizwa upande mmoja na kuamuriwa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe **31 Oktoba, 2022**

NGUKULIKE, N.O
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MTWARA.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**EMMANUEL NKWABI KABALO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 759 AFY** aina ya **SCANIA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/770/2022.**

**KUPOTEA KADI YA GARI**

**OBREY SAFARIS & HINKING LIMITEDA** natangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 134ALB Station Wagon /White. Chasses Namba HJ750034640,** Engine Namba **2H1190738** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : **KIL/MOS/RB/454099/2022**

**KUPOTEA KADI YA GARI**

**SIMON MUYEMBA BITURO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX PICK-UP** yenye namba **371967** na usajili namba **T200 AHE.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0713418546 ,** Zawadi itatolewa . **POLISI TAARIFA: DAR/OST/RB/456780/2022**

# Raia wa Ukraine aliyekwama Zanzibar asimulia yaliyomkuta

• Apata mchumba mwenyeji, ajifunza kukuna nazi

Na Salome Kitomari



Vladyslava Yanchenko akifurahia maisha Zanzibar . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"MAISHA ya hapa Zanzibar ni mazuri sana kuliko ambayo ningeendelea kuishi nyumbani kwetu Kiev (Ukraine)," Vladyslava Yanchenko (23), raia wa Ukraine anasimulia utofauti wa maisha ya Zanzibar na nchi aliyotoka.

Vladyslava ambaye sasa anaishi Kijiji cha Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja baada ya kukwama kurejea kwao kutokana na vita, anaendeleza simulizi ya ushuhuda wake, akitamka:

"Kwa kuishi hapa Zanzibar nimejua kufua, kulima na kujipikia. Kule kwetu Kiev zinasikika sauti za mabomu na risasi, hakuna amani, muda wote ni wasiwasi."

Binti huyo ni miongoni mwa watalii 1,200 ambao wakati vita inatokea, walikuwa visiwani Zanzibar kwa shughuli za utalii. Baadhi waliondoka kwenda maeneo mbalimbali duniani na wengine walibaki na kusaidiwa na serikali kupata visa na sehemu za kuishi.

Vladyslava alipata unafuu kuwa siku za nyuma katika safari zake za utalii, alipapenda Zanzibar na kununua ardhi kwa ajili ya uwekezaji, hivyo kulipotokea vita, alijenga nyumba ya kawaida kwenye eneo lake na ndiko anakoishi kwa sasa.

Anasema katika maisha yake hakuwahi kufikiri kuna siku angeishi kijijini kwenye maisha ya kawaida kabisa ya Kiafrika na akamudu kujipikia, kufua na kulima mazao yanayomsaidia, lakini imetokea na sasa amekuwa swahiba wa wenyeji wa Zanzibar.

Vladyslava, katika mazungumzo mahususi na Nipashe visiwani Zanzibar, anasema kwa sasa ameshakuwa mwenyeji na anaendesha biashara zake mtandaoni na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yake.

Anasema anafurahi maisha yake mapya kwenye eneo lisilo na msongamano na shughuli nyingi kama ilivyo Kiev.

"Nimepita kipindi kigumu sana cha maisha, msongo wa mawazo uliniandama, niliikumbuka sana familia yangu, kuna wakati hadi nilikuwa ninaumwa kila nikiwakumbuka wazazi wangu, bibi yangu mwenye umri wa miaka 72 na ndugu zangu wengine, nimelia kwa muda mrefu sana, sijaweza kuwasiliana nao kwa muda mrefu hadi hivi karibuni nilipoanza kuongea nao kwa WhatsApp.

"Vita ni mbaya sana, watu wanafikiri Ukraine ni mji mdogo, lakini ni nchi yenye watu zaidi ya milioni 43.8, lakini tumevamiwa na kuharibiwa maisha yetu na nchi yenye watu zaidi ya milioni 143.4, athari ni kubwa sana hasa tukizingatia watu wengi hawana hati za kusafiria," anasema.

Vladyslava anasema alitua visiwani Zanzibar kwa ajili ya mapumziko lakini alishindwa kurejea Ukraine kutokana na vita hiyo, akalazimika kujifunza maisha ya wenyeji, akipokewa na raia wa Ujerumani ambao aliishi nao kwa muda baadaye akaamua kwenda kuishi kwake kwenye nyumba ya matofali ya udongo aliyojenga.

"Ninayafurahia maisha ya hapa kwangu, kwa sasa Ukraine hali ya hewa ni nyuzi joto sita hadi 12, kuna baridi kali sana pia chakula ni cha shida kutokana na vita. Hapa (Zanzibar) nina uhakika wa maisha, watu wanaishi maisha ya kawaida sana lakini ya amani, ninapata chakula, nimelima mapapai nimevuna.

"Hali ya Ukraine ni ngumu sana, watu hawana chakula, mali zimeharibiwa, wengi wako nyumbani hawana uhakika wa maisha. Kuishi hapa Zanzibar kuna ahueni kubwa ingawa muda wote mawazo ni kwa familia yangu.

"Ninapenda hali ya hewa ya hapa, nilikuwa sijui kupika lakini sasa ninapika, tena kwa gesi ya kawaida, sikuwahi kufua kwa mikono, nilifua kwa mashine, sikutarajia nitaishi kwenye nyumba isiyo na umeme wala maji na miundombinu ya kisasa.

"Nilikuwa sijui kutafuta maji lakini sasa ninatafuta maji, ninaishi maisha ya Kiafrika. Kuna wakati ninapitia maisha magumu sana, sina kipato chochote, ninasaidiwa na majirani, ninachofurahia ni amani niliyonayo, sisikii sauti za mabomu," anasema.

Vladyslava anainyoshea kidole Russia kwa anachokiita kuharibu kwa makusudi maisha ya zaidi ya watu milioni 43, akiitaja familia yake kwamba mdogo wake mwenye umri wa miaka 15 sasa anaishi Uswisi kama mkimbizi.

### KUNUNUA NYUMBA

Binti huyo anasimulia maisha yake kwamba mwaka 2020 aliingia nchini kwa ajili ya likizo na kusherehekea siku yake ya kuzaliwa na alipapenda Zanzibar na kumwambia baba yake ambaye alimruhusu anunue ardhi.

Alirejea Zanzibar kwa ajili ya likizo nyingine Februari mwaka huu na wakati anajiandaa kuondoka, wakapata taarifa, Russia imeivamia kivita nchi yao.

"Niliwasiliana na baba aliniambia yeye atabaki Ukraine kupigania nchi yetu. Aliniambia nibaki Zanzibar, nisirudi Ukraine kutokana na hali iliyoko, haikuwa rahisi kwangu, tangu Februari hadi Juni nilikuwa ninalia tu kila siku, nimepoteza kila kitu kuanzia nyumba niliyokuwa nimepanga na ofisi ya kampuni yangu, sina ndugu hapa nilipo ila nina Watanzania ambao wamekuwa watu wema kwangu muda wote," anasema.

Vladyslava anasema majirani wanampenda, hasa watoto ambao wakitoka shuleni wanakwenda nyumbani kwake kuongea naye.

"Ninapenda sana watoto hadi ninafikiria baadaye nifungue kituo cha kulea watoto, nina marafiki wengi na ninajulikana," anasema.

Vladyslava anabainisha kuwa alipokuwa Ukraine, alikuwa anaishi maisha yake mwenyewe mbali na wazazi wake na alifungua kampuni inayotoa ushauri wa kibiashara na ujasiriamali na kumpatia fedha nyingi.

"Nilifungua kampuni nikiwa na miaka 19, ilikuwa inafanya vizuri sana, nilipata fedha nyingi lakini kutokana na vita biashara yangu iliharibika yote, nilikuwa na ndoto kubwa sana," anasema.

### APATA MCHUMBA

Vladyslava anasema amepata mchumba ambaye ni Mzanzibar na amemwomba wafunge ndoa, lakini anafikiria kama yuko tayari kuishi maisha ya familia na kuwa na watoto.

"Ameniomba anioe ila bado ninafikiria kwa maisha niliyonayo ninaweza kulea mtoto? Watoto wana mahitaji mengi sana, ni lazima nijiandae kuwasaidia ipasavyo, ni lazima nifikirie kwa kina kabla ya kuwa na familia, ni uamuzi mgumu ambao lazima niufanye kwa uangalifu.

"Tumeshaongea, tumebaki kuwa marafiki wakati ninaendelea kutafakari uamuzi wangu, ameniambia anasubiri niamue," anasema Vladyslava na kusita kutaja jina la kijana huyo.

### MAJIRANI WANENA

Ibrahim Rashid, jirani wa Vladyslava, anasema kuwa kijijini kwao ni umbali wa zaidi ya saa moja kutoka mjini Unguja na walimpokea raia huyo na kuishi naye kwa kumsaidia mahitaji ya msingi kutokana na nyumba yake kutokuwa vizuri.

"Awali ilikuwa vigumu sana kuishi naye, alikuwa na msongo wa mawazo, ilikuwa kazi kuzoea watu wengine na hasa maisha yetu haya, nilimsaidia kutafuta mafundi waelewa kujenga kibanda chake kwa kuwa kuna wakati ana fedha na wakati mwingine hana.

"Siku nyingine alikuwa anakuja kuishi kwangu, anataka kuchaji simu zake, lugha haikuwa shida sana kwa sababu nami shughuli zangu ni za utalii, hivyo ninaijua kiasi.

"Nilimpa mtungi wa gesi na mahitaji mengine, siku ninacho namsaidia, siku sina ninamwambia leo sina," anasema Rashid na kubainisha kuwa jirani yake huyo alipanga kujenga jengo la hadhi kubwa lakini akaamua kujenga kibanda kutokana na kukosa fedha.

Mmoja ya wanakijiji wa Kizimkazi, Hassan Ali anasema wanaishi vizuri na Vladyslava na kumwelezea kama binti anayependa kujichanganya na wanakijiji.

Mkurugenzi Uratibu wa Shughuli za Utalii kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Omar Suleiman Mohammed anasema kulikuwa na raia wa Ukraine 1,200 waliokuja kwa shughuli za utalii ambao wakati vita vinatokea nchini mwao walikuwa visiwani Zanzibar.

Mohammed afafanua kuwa wakati vita vinaendelea, wengi wao waliondoka na kuelekea mataifa mbalimbali ya Ulaya kwa gharama zao, sita walisaidiwa usafiri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na 12 wamebaki Zanzibar.

"Kati ya hao 12, wapo waliokodi nyumba na wengine wamepewa hifadhi na serikali inawasaidia gharama za viza ili kuendelea kubaki nchini," anasema.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN), vita vya Ukraine na Russia vilivyoanza Februari mwaka huu, vimesababisha zaidi ya raia milioni 6.3 kuikimbia Ukraine.

# CCM yabadili kanuni umri kuwania uongozi UVCCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimebadili kanuni ya ukomo wa umri wa kugombea uongozi ndani ya Jumuiya ya Vijana wa chama hicho (UVCCM) kuwa miaka 35 badala ya 30 iliyokuwapo awali ili kutoa fursa zaidi ya kuongoza jumuiya hiyo.

Vilevile, viongozi wa UVCCM wameonywa kujigeuza kuwa viongozi wa watu fulani kwa kuwa watu wana mwisho lakini chama hakina mwisho.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo alibainisha hayo jana wakati wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa UVCCM ngazi ya taifa unaofanyika jijini Dodoma.

Alisema moja ya mambo ambayo yalianza kuleta vikwazo kwenye jumuiya ni alichokiita ombwe kutoka vijana wanaofuzu ujana wakiwa vijana sana, kukosa fursa ya uongozi ndani ya jumuiya zingine.

"Vijana wamewekewa umri wa mwisho miaka 30 kugombea nafasi kwenye jumuiya ya vijana, matokeo vijana wengi wanapata fursa ya kujifunza kwa muhula mmoja wakati wanaanza kukomaa kuwa vijana, fursa inakoma na hapati fursa ya kuendeleza uongozi wa nafasi nyingine.

"Matokeo yake vijana wazuri ambao wameanza kujengeka na kukomaa kiuongozi walianza kujikuta wanaelewa kwa kukosa fursa wakaenda wazazi wanaangaliwa mara mbili mbili nawe umekuwa mzazi subiri kidogo, ukienda UWT wanaambiwa bado hujawa mama, akirudi vijana anaambiwa umri umepita vijana wengi wakajikuta wanaingia kwenye changamoto ya kutafuta vyeti vya kutengeneza ili waonekane bado vijana.

"Sasa chama hiki ni sikivu na chama hiki kinaona mbali, kwa sababu leo ndiyo tunahitimisha uchaguzi wa UVCCM ngazi ya taifa baada ya hapo nafasi yoyote itakayotokea huko mbele mwisho wa kugombea ni miaka 35, lengo ni kurejesha nafasi ya kuwakuza vijana mpaka miaka 40 ndani ya umoja wa vijana," alifafanua.

Akifungua mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana aliwataka vijana wa CCM kuelewa kwa kina sera, ilani na katiba ili kukitetea chama na serikali kwa hoja bora.

"Kazi yenu ya kwanza ni kuelewa kwa umakini, kwa kina sera, ilani ya Chama Cha Mapinduzi, huwezi kutetea jambo kama hulijui, bahati nzuri maandishi mengi ya chama yapo kwenye vitabu na mtandao wa chama, jambo la kwanza ni kuelewa vizuri sera, ilani, katiba na mwelekeo wa chama, mkifanya hivyo, mtakuwa na uwezo mkubwa sana wa kukitetea.

"Hoja hushindwa na hoja iliyo bora zaidi na hoja iliyobora zaidi haitoki hewani, haiwezi kubuniwa, lazima iwe ni hoja iliyofanyiwa uchambuzi, wakati mwingine ninasoma watu wanavyobishana, hauoni uzito mkubwa wa mabishano au thamani ya hoja zinazojengwa," alisema.

Aliwataka kutumia muda mwingi kusoma na kuelewa katiba na ilani ya chama na yanayofanyika kwenye maeneo yao kwa kila sekta na kuyasemea.

"Kiongozi mzuri wa vijana ni yule anayefahamu ahadi zilizotolewa na kinachofanyika kwenye eneo lake, ukiyafahamu hayo ni rahisi kukitetea chama, ni rahisi kuisemea serikali ya CCM, kama hufahamu utazungumza mambo ya jumla jumla, mambo ambayo wewe mwenyewe huyajui.

"Wasiotutakia mema wanatutoa kwenye ajenda muhimu kwa sababu na sisi hatujajiandaa mkajiingiza kwenye mkumbo wa kujadili mambo ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na mambo ambayo tumewaahidi Watanzania na mambo ambayo tumejipanga kuyatekeleza," alionya.

Awali akisoma taarifa ya uchaguzi mkuu wa jumuiya hiyo, Katibu Mkuu wa UVCCM, Kenani Kihongosi alisema vijana 641,654 walijitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya matawi hadi taifa.

Alisema wakati wa uchaguzi yalipokewa malalamiko 65 na kati ya hayo 48 yalishughulikiwa huku 17 yakishindwa kushughulikiwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo walalamikaji kushindwa kuthibitisha malalamiko yao.

## Jela maisha kwa kunajisi mtoto

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MKAZI wa Ilembo, Kata ya Vwawa wilayani Mbozi mkoani Songwe, Betwel Anyalwisye (51) amehukumiwa kifungo cha maisha gerezani baada ya kukutwa na hatia ya kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka sita.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Mbozi, Names Chami, alisema mahakama imemtia hatiani mshtakiwa baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka pasi na kuacha shaka yoyote.

Hakimu Chami alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo Agosti 6 mwaka huu eneo ya Ilembo, Kata ya Vwawa kwa kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka sita huku akijua kufanya hivyo ni kosa.

Alisema mahakama baada ya kujiridhisha na ushahidi inamhukumu Anyalwisye kutumikia kifungo cha maisha gerezani ili liwe fundisho kwa watu wanaofanya vitendo hivyo.

"Mtuhumiwa alikuwa akifanya tendo hilo mara kadhaa lakini Agosti 6, 2022 alikamatwa katika Kitongoji cha Ilembo iliko nyumba yake akitumia njia ya kumdanganya kwa kumpa zawadi ya pipi mtoto mdogo mwenye miaka sita na kufanya uovu huo wa kikatili kwa mtoto," alisema Hakimu Chami.

Ilidaiwa mahakamani huko na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Ally Kambona kuwa mtuhumiwa alikuwa akimfanyia ukatili huo mtoto huyo mara kwa mara huku akimdanganyishia zawadi, hasa pipi na biskuti.

Alidai mtuhumiwa alikamatwa Agosti 6, mwaka huu, kutokana na ushirikiano wa majirani waliobaini vitendo vya mtuhumiwa huyo ambapo siku hiyo alidaiwa kumrubuni mtoto huyo na kwenda kulala naye nyumbani kwake.

Kambona aliiomba mahakama kutoa adhabu kali ambayo itakuwa fundisho kwa wale wote wenye tabia za kuwafanyia ukatili watoto.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire (kushoto), akizungumza na mteja wakati wa hafla ya kumtambulisha mkurugenzi mpya kwa wateja wa kampuni hiyo, hafla hiyo imefanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RAS acharuka kukosekana mpango wa utoaji wa dawa

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Songwe, Happiness Seneda, amechukizwa na kitendo cha kutokuwapo mpango mzuri wa upokeaji na utoaji wa dawa kwa wagonjwa katika Kituo cha Afya Ileza, Kata ya Magamga wilayani Songwe.

Seneda alieleza kukerwa na kitendo hicho juzi alipotembelea kituo hicho kufuatilia ujenzi wa majengo mapya na utoaji wa huduma za matibabu, akishuhudia ukosefu wa taarifa za utoaji wa dawa kwa wagonjwa.

Kata ya Magamba iliyoko pembezoni mwa wilaya hiyo ina zaidi ya wakazi 17,400. Awali wakazi wake walikuwa wakitembea Km 18 kupata huduma za afya makao makuu ya wilaya yaliyoko Kata ya Mkwajuni.

Sophia Mwashilindi, mkazi wa Kijiji cha Ileza alisema kituo hicho kimeanza kutoa huduma, hivyo wananchi wameondokana na kadhia ya kutembea umbali mrefu kupata matibabu.

Alfonce Mponzi, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema aliipongeza serikali kwa kutimiza wajibu wake kikatiba kwa kuwajengea kituo cha afya na sasa wana uhakika wa kupunguza vifo, vikiwamo vitokanavyo na uzazi.

"Katibu Tawala tunakupongeza kwa jitihada za kuja hapa kujua maendeleo ya kituo hiki, hapa kuna tatizo la ukosefu wa dawa, pia daktari anayetegemewa anaishi kwenye kata nyingine ng'ambo ya mto, maji yakijaa hatakuwa na uwezo wa kuvuka, wagonjwa hapa watakosa huduma, watakufa," alitahadharisha.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Timoth Simkonde, alipotakiwa kujibu kuhusu shutuma hizo, aliahidi watajirekebisha na watakuwa wanatunza kumbukumbu za dawa zinazoingia na kutumika.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Dk. Egfrid Mwingilihela, alikiri kuwapo malalamiko ya wananchi kuhusu daktari kukaa nje ya kata kutokana na ukosefu wa nyumba za watumishi, hivyo jitihada za kujenga nyumba zinafanyika.

Ujenzi wa kituo hicho ulianza mwaka 2019 kwa utaratibu wa kutumia nguvukazi ya ndani (Force Account), ukijumuisha majengo ya wazazi, upasuaji, maabara, nyumba moja ya mtumishi na uendelezaji jengo la wagonjwa wa nje (OPD) lililokuwa likijengwa kwa nguvu za wananchi tangu mwaka 2014.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi chukueni darasa hili Kombe la Dunia Qatar

**USHINDANI** mkubwa unaendelea kuonekana kwenye Fainali za Kombe la Dunia zinazoendelea nchini Qatar ikiwa ndiyo kwanza imetinga raundi ya pili kwenye hatua ya makundi, timu zisizokuwa zinatarajiwa zinaendelea kuishangaza dunia.

Tayari tumeshuhudia vigogo vya soka duniani vikiangukia pua, ambapo Argentina imekubali aibu dhidi ya Saudi Arabia kwa kipigo cha mabao 2-1 wakati Ujerumani nayo ikisalimu amri kwa kupokea kichapo kama hicho kutoka kwa Japan, lakini wenyeji wa michuano hiyo, Qatar wakipoteza mechi zote mbili za awali.

Utamu na ladha ya michuano hiyo kwa hakika inachagizwa na kuvutia zaidi kutokana na sheria 17 za soka kufuatwa ipasavyo na waamuzi bila kujali ukubwa wa timu, umaarufu, ukongwe kwenye michuano hiyo ama uenyeji.

Kwa wanaofuatilia michuano hii watakubaliana nasi kwamba ni mbingu na ardhi ukifananisha maamuzi yanafanywa katika soka la hapa nchini na waamuzi wetu, ambao kimsingi wopo chini wa mwavuli mmoja, Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), linalosimamia sheria 17 soka.

Tofauti katika michuano hiyo na hapa nchini ni kwamba uwezo wa timu kwa mwongozo wa sheria hizo 17 za soka ndio huamua matokeo na si kama inavyotokea katika baadhi ya mechi hapa nchini waamuzi kuonekana kuwa sehemu ya matokeo. Timu inayopoteza na inayoshinda kila moja inakuwa inastahili kwa matokeo inayoyapata kwani haki inatendeka na inaonekana kweli ikitendeka, jambo ambalo waamuzi wetu hawana budi kuendelea kujifunza kupitia michuano hiyo mikubwa zaidi duniani.

Hatukuona Argentina na Ujerumani zikibebwa na waamuzi kutokana na ukubwa wao ama Qatar kwa kuwa mwenyeji, bali kinachoshuhudiwa ni haki ikitendeka kwa kufuata sheria 17 zinazoruhusu ubora na uwezo kuamua matokeo.

Kitu ambacho mara nyingi kwa baadhi ya waamuzi nchini wamekuwa wakikutwa na hatia na kisha kufungiwa kutokana na kushindwa kutenda haki husus an wanapochezesha timu pendwa na tunazoziita kubwa, Simba na Yanga.

Kupitia fainali hizo, tumeshuhudia pia muda wa nyongeza ukiongezwa hadi dakika 14, kitu ambacho ni nadra kukiona kikifanywa na waamuzi wa soka nchini licha ya kwamba katika baadhi ya mechi muda mwingi umekuwa ukipotezwa kutokana na wachezaji kuumia, kufanya mabadiliko na mambo mengine ndani ya uwanja.

Pamoja na kwamba uamuzi huo bora kwenye Kombe la Dunia unachangiwa na uwapo wa Teknolojia ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR), lakini hilo halipaswi kuwa kisingizio kwani kuna mambo mengi yakujifunza kwa waamuzi wetu ambayo hayahitaji hata teknolojia hiyo.

Nipashe tunatamani kuona waamuzi wakiitumia michuano hiyo kwa lengo la kujifunza na kuleta mapinduzi makubwa kwenye ligi yetu ili kuendelea kuwa kivutio kwa wawekezaji lakini pia kwa wachezaji wakubwa kuja kucheza soka nchini.

Tunaamini kama waamuzi wakipata darasa hilo ipasavyo, ligi yetu inauwezo wa kuwa ndani ya ligi tano bora barani Afrika katika kipindi kifupi kijacho na kuvutia wawekezaji wengi zaidi pamoja na wachezaji wakubwa.

Hivyo, ni wakati wa kubadilika sasa kwa waamuzi ili kutoa fursa kwa soka letu kupiga hatua kwani kwa njia hiyo ndiyo pia inayoweza kuifanya Tanzania siku kutoa waamuzi wakuchezesha michuano hiyo mikubwa pamoja na nchi kushiriki fainali hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Adhabu ya Prisons, Singida Big Stars iwe somo usajili dirisha dogo

Na Adam Fungamwango

**KATIKATI** ya mwezi Desemba, dirisha la usajili Ligi Kuu Tanzania Bara linatarajiwa kufunguliwa ambapo timu mbalimbali za ligi hiyo pamoja na za madaraja mengine ya chini zitaruhusiwa kusajili wachezaji kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye vikosi vyao.

Kwenye mpira wa miguu mara nyingi vikosi huwa havikamiliki moja kwa moja, ni lazima kunakuwa na mapungufu, hivyo klabu zinapata fursa ya kusajili kwa ajili ya kuziba mapengo ambayo wanaona yanatakiwa kuzibika ingawa si lazima.

Wakati tunaelekea huko, ni klabu 14 tu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zitaruhusiwa kusajili, huku mbili zikiwa zimefungiwa. Timu ambazo haziruhusiwi kusajili kipindi hiki cha dirisha dogo ni Prisons na Singida Big Stars. Ni kwa sababu ya makosa ambayo viongozi wao waliyafanya kipindi cha dirisha kubwa la usajili.

Ziliwasajili wachezaji ambao bado wapo kwenye mikataba na timu zao. Prisons ilimsajili mchezaji Mussa Mbisa wa Coastal Union wakati akiwa na mkataba wa klabu yake, huku Singida Big Stars nayo ikimsajili Metacha Mnata kutoka Polisi Tanzania akiwa ndani ya mkataba. Timu zote hizo ziliwasajili makipa kutoka timu zingine wakiwa na mikataba na ndicho ambacho kitawagharimu kwenye kipindi cha dirisha dogo linalokuja.

Mwezi Oktoba mwaka huu, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ilizifungia klabu hizo kutosajili kwa dirisha moja la usajili kwa maana hiyo zitabaki na wachezaji hao hao mpaka mwisho wa msimu.

Zitaanza kufanya usajili kwa ajili ya msimu ujao wa ligi na si katikati. Hili ni pigo kubwa kwa timu hizo, hasa Prisons ambayo inaonekana kuwa na upungufu.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Shaaban Mtupa, akakiri kuwa walihitaji sana kukitumia kipindi hiki kuboresha kikosi chao, lakini haiwezekani.

"Niseme lazima ukishacheza ligi kwa nusu msimu utaona upungufu na mkishakaa na wachezaji kwa muda mrefu lazima uwe na matamanio ya kuongeza baadhi kwa ajili ya kuziba upungufu na kuleta ushindani, lakini kwa bahati mbaya sisi tumefungiwa hivyo tunasikitika kuwa hatutokuwa na nafasi ya kuongeza mchezaji yeyote, hawa waliokuwapo maana yake tutaendelea nao. Tutakuwa na hawa hawa hadi mwishoni mwa msimu," akasema kocha huyo.

Maneno haya yanaonyesha kuwa benchi la ufundi lilihitaji sana kuongeza wachezaji, lakini haitowezekana hivyo kuwapa kazi kubwa makocha kutumia rasilimali walizonazo mpaka mwisho wa msimu licha ya kwamba zingine zina mapungufu.

Hali inayowakuta Prisons na Singida Big Stars iwe funzo kwa klabu zingine ambazo zinakwenda kufanya usajili. Kuna baadhi ya viongozi wa klabu wamekuwa wakifanya usajili wa kujiamini kupita kiasi kwa sababu wanazozijua wao, kusajili wachezaji ambao bado wana mikataba na klabu zingine.

Yanaweza kuwakuta kama yalivyozikuta timu hizi. Tena afadhali hata usajili wa dirisha dogo, ule mkubwa ni muhimu sana, hivyo kama viongozi watatokea kuvurunda kusajili kipindi hiki, basi watarajie kupigwa nyundo ya kutosajili mwanzo wa msimu. Kufungiwa kutosajili mwanzo wa msimu ni kujitengenezea mazingira ya kuishusha daraja timu kwani baadhi ya klabu huondokewa na wachezaji wakati mwingine zaidi ya 10 kwa kumaliza mikataba au kusajili na timu zingine wakiwa ndani ya mikataba.

Kwa maana hiyo timu itakayofungiwa na wachezaji wake zaidi ya 10 kuondoka itakuwa kwenye hali ngumu sana.

Nawasihi viongozi wa klabu wawe makini kwenye usajili, lakini na wachezaji wadanganyifu. Kuna wachezaji ambao hawasemi kweli, wana mkataba kwenye klabu moja, lakini wanasajili klabu nyingine kwa tamaa ya pesa.

Viongozi wa klabu wanatakiwa kwanza waletewe mikataba yao kabla hawajawasajili, na kama hawatoridhika au kutaka kujiridhisha wapige hodi TFF kwa ajili ya kujua mikataba yao kama imeisha au la. Vinginevyo basi ni lazima waongee na klabu zao kwa ajili ya kuvunja mikataba yao. Vinginevyo wategemee kuyapata kama ya Prisons na Singida Big Star.

# Watuhumiwa 230 mbaroni, wamo wa dawa za kulevya

**Na Samson Chacha,** TARIME

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Tarime/ Rorya limekamata silaha aina ya bastola na Shortgun pamoja na risasi 82, pikipiki tisa, bangi Kg 4,241, lita 2,370 za pombe haramu aina ya gongo na watuhumiwa 236 wakiwamo wezi wa mifugo na majambazi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Geofrey Sarakikya alisema: "Tulianza msako Julai mwaka huu wa wahalifu katika wilaya zetu sita za kipolisi za Nyamwaga, Sirari, Utegi, Kinesi, Shirati na Tarime Mjini na kufikia Oktoba 30, tulikuwa tumewakamata watuhumiwa 236 wakiwamo wezi wa mifugo, wauaji, kupatikana na silaha, dawa ya kulevya aina ya bangi na mirungi, majambazi sugu, wezi wa pikipiki, wauzaji pombe haramu ya gongo na wezi wa mawe ya dhahabu katika Mgodi wa Barick North Mara.

"Katika msako huo tulikamata silaha mbili, moja bastola aina ya Pietro Berretta yenye namba TZ CAR 76091 na silaha ya pili ni Shortgun ambayo namba zake zimefutwa na mtutu kukatwa, risasi 82 za AK 47."

Kamanda huyo alibainisha kuwa kati ya watuhumiwa hao, 35 walikamatwa wakidaiwa kuwa na kilogramu 4,241 za bhangi zikiwa zimebebwa kwa pikipiki tisa na gari moja aina ya Probox lenye namba za usajili T 242 DUU, watuhumiwa 11 wa wizi wa mawe ya dhahabu walikamatwa wakiwa na jumla ya Kg 61.16 za mawe ya dhahabu na viroba vya mawe hayo 2,367 wakiwamo wafanyakazi wa Mgodi wa Barrick North Mara.

Pia alisema walikamatwa wahamiaji tisa walioingia nchini bila kufata utaratibu na kukabidhiwa kwa maofisa wa Jeshi la Uhamiaji ngazi ya wilaya kwa hatua zaidi.

Kamanda huyo pia alisema walikamata vilipuzi vya miamba vitatu aina ya V16 ambavyo havikuwa na vibali, kemikali aina ya zebaki, watuhumiwa watatu wa wizi wa mifugo, watuhumiwa 28 waliokuwa wamelima mashamba ya bangi ekari 9.5 na wezi wa pikipiki zilizoibwa mikoa ya Geita Simiyu, Mwanza na Mara.

Kamanda Sarakikya aliiomba jamii kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili wahalifu wakamatwe, hivyo raia kuishi kwa amani na kuendesha shughuli zao kwa kuwa jeshi hilo limejipanga kupambana na uhalifu wa aina zote.

**Katika msako huo tulikamata silaha mbili, moja bastola aina ya Pietro Berretta yenye namba TZ CAR 76091 na silaha ya pili ni Shortgun ambayo namba zake zimefutwa na mtutu kukatwa, risasi 82 za AK 47.**



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atupele Mwakibete, akizungusha kifaa maalumu kuashiria uzinduzi wa Chama cha Wamiliki wa Matipa na Mitambo (TTMA) jijini Dar es Salaam. (Wa pili kushoto) ni Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks & Equipments Ltd, Ally Jawad Karmal, (kushoto) Salman Karmal Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Masoko wa GF na (kulia) ni Mwenyekiti wa chama hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: Tumieni mapato ya ndani kutekeleza miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka halmashauri nchini kutumia fedha za makusanyo ya ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo badala ya kusubiri fedha kutoka serikali kuu pekee.

Aliagiza hayo jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa sita katika Shule ya Sekondari Mwandege wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Majaliwa alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mwantumu Mgonja, kutenga Sh. milioni 120 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika shule hiyo ifikapo Januari mwakani.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa, Waziri Mkuu alisema serikali imejipanga vizuri kuwahudumia Watanzania ili kusaidia kuchochea shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

"Huu ni wakati wa kufanya kazi, nimeridhika na viwango vya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hii, endeleeni kusimamia viwango kwenye miradi mingine, twende na matakwa ya Rais wetu na kumsaidia kutimiza maono yake ya kuwahudumia Watanzania," alisema.

Waziri Mkuu alisema mipango ya Rais Samia ni kuhakikisha serikali inawafikia Watanzania popote walipo hadi vitongojini kwa kupeleka huduma mbalimbali za kijamii zikiwamo za afya, maji, elimu, umeme na mawasiliano.

Majaliwa pia alitoa wito kwa wakulima wote nchini kutumia mvua inayonyesha kulima mazao, akitamka: "Mvua za kwanza ndiyo mvua za kupandia, twende tukaanze kazi ya kilimo, tupande mazao yenye uwezo wa kuota kwa muda mfupi ili yaweze kuiva na kutusaidia kupata chakula".

Majaliwa pia aliwataka watendaji wa serikali kuzungumza na wakulima kutumia vizuri chakula kilichoko ili kiwasaidie kufika msimu ujao wa mavuno.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema Mkoa wa Pwani umepokea Sh. bilioni 6.8 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 341.

"Wananchi wa Mkuranga niwahakikishie kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria na anafanya kwa vitendo kutuondolea adha ya vyumba vya madarasa," alisema.

Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdala Ulega aliishukuru serikali kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Mkuranga na Mkoa wa Pwani kwa ujumla.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa, Ofisa Elimu Idara ya Sekondari, Benjamin Majoya, alisema Wilaya ya Mkuranga imepokea fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 132 ya kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 katika shule 26 za sekondari yenye thamani ya Sh. bilioni 2.64.

Alisema kukamilika kwa vyumba hivyo vya madarasa pamoja na vilivyoko kutawezesha jumla ya wanafunzi 10,800 kupata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 wilayani Mkuranga.

Waziri Mkuu jana alianza ziara ya kikazi inayolenga kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kuzungumza na watumishi katika Mkoa wa Pwani.

## KABWELA



# TCAA yaikabidhi NIT ithibati ya mafunzo ya usafiri wa anga

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimekabidhiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ithibati za mafunzo ya kozi mbili za usafiri wa anga.

Kozi hizo ni za uhandisi wa matengenezo ya ndege pamoja na uendeshaji wa safari za ndege.

Akizungumza kabla ya makabidhiano hayo mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Aron Kisaka alisema:

"Kupatikana kwa ithibati hizi ni hatua muhimu sana kwa taifa hasa katika kipindi hiki ambacho serikali inaendelea kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na sekta ya usafiri wa anga kwa ujumla."

Kisaka alisema serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutatua vikwazo mbalimbali kwa NIT ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuongeza uwezo wa watumishi katika kutoa na kusimamia mafunzo ya usafiri wa anga.

"Ninawapongeza sana kuhusu uanzishwaji na utekelezaji wa majukumu ya chuo kwa upande wa Shule Kuu ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga ambayo yameainishwa katika Mpango Mkakati wa Nne wa Miaka Mitano (2020/21 - 2024/25).

"Pia nimefurahi kusikia mafanikio mliyoyapata ambayo matunda yake yamewezesha kupatikana kwa ithibati hizi. Hii ni ishara ya juhudi kubwa za chuo katika kuhakikisha kinatimiza malengo ya uanzishwaji wake ikiwa ni pamoja na kuandaa wataalamu wa usafiri wa anga kwa kuhakikisha mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga yanatolewa nchini kupitia chuo hiki kwa kiwango cha kimataifa," alipongeza.

Alisema serikali imewekeza nguvu kubwa katika kuimarisha na kuboresha usafiri wa anga ambao ni moja ya kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

"Hatua hii inakwenda sambamba na ununuzi wa ndege 10 na katika mwaka huu wa fedha 2022/23, serikali itanunua jumla ya ndege tano (5) ambazo zinatarajiwa kuanza kuwasili kuanzia mwezi wa Machi mwakani.

"Ununuzi wa ndege pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu utaongeza idadi ya safari za ndege na hivyo kuongeza mahitaji ya wataalamu wa usafiri wa anga katika fani mbalimbali.

"Hivyo, mafunzo haya ni muhimu katika kuandaa wataalamu wa kutosha wenye ubora unaokubalika kimataifa na hivyo kuboresha huduma ya usafiri wa anga nchini," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisisitiza kuwa katika kuhakikisha sekta hiyo inakua kwa haraka, serikali imekuwa ikiongeza bajeti katika sekta ndogo ya usafiri wa anga kutoka mwaka hadi mwaka.

"Juhudi hizi ni ushahidi tosha kuwa serikali ina dhamira ya dhati ya kukuza na kuimarisha sekta ya usafiri wa anga ambayo ni kiungo muhimu katika ukuaji wa sekta mbalimbali ikiwamo ya utalii, kilimo na biashara.

"Hivyo, nitoe wito kwa chuo kuhakikisha kinaendelea kutoa elimu bora inayoendana na mahitaji ya sasa kwa umakini wa hali ya juu na kwa kuzingatia matakwa ya ithibati hizi.

"Pia nitoe rai kwa mashirika ya usafiri wa anga kuwa na utaratibu wa kutoa fursa za mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kozi hizi wakati wa mafunzo na baada ya kuhitimu mafunzo.

"Programu hizi zitaongeza umahiri zaidi katika vitendo na pia zitawafanya wanafunzi wapate uzoefu wa kazi ili kukidhi moja ya vigezo vinavyohitajika kufanya mitihani ya leseni katika Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)," alisema.

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema ithibati hizo ni ishara na mwanzo wa chuo hicho kuendelea kutoa mafunzo bora katika taaluma ya uhandisi wa matengenezo ya ndege na uendeshaji wa safari za ndege.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Teophory Mbilinyi, aliwataka NIT kuendelea kutoa wahitimu bora kwa kuwa sekta ya usafiri wa anga inakabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali watu.



Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Aron Kisaka (kushoto), akipata maelezo kuhusu mafunzo ya anga baada ya kutembelea Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) katika hafla ya chuo hicho kukabidhiwa ithibati ya mafunzo ya kozi mbili za usafiri wa anga na uendeshaji wa safari za ndege kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Mazao ya wakulima yaoza shambani kwa kukosa soko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKULIMA wa mboga katika Tarafa ya Mgeta wilayani Mvomero wamelalamika kupata hasara kila mwaka ya tani 30,000 za mazao hayo kuharibika na kuoza kutokana na kukosa soko.

Shida kuu inayotajwa na wakulima hao ni kutokuwa na uhakika wa usafiri kutokana na ubovu wa barabara.

Wakulima hao waliwasilisha kilio chao hicho kwa nyakati tofauti katika mkutano wa vijiji vyote vya tarafa hiyo uliolenga kuibua miradi ya kutatua kero zinazowakabili ukiwamo ubovu wa barabara na ukosefu wa masoko.

Wananchi hao wanashirikiana na Mtandao wa Wakulima Afrika Mashariki na Kusini (ESAFF) na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Wadogo Tanzania (MVIWATA) kutatua kero hizo.

Akizungumza katika mkutano huo uliofanyika katika Kijiji cha Kibagala, Kata ya Tchenzema, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Sist Mkude alisema licha ya wakulima kuzalisha kwa wingi mboga, hawapati faida ya kutosha kutokana na kushindwa kusafirisha mazao yao kwa kuwa barabara ni mbovu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Tchanzema, Prosper Ngatigwa, alisema wakulima wake wanazalisha msimu mzima kuanzia Januari hadi Desemba lakini wanalazimika kuzitupa mboga hizo kutokana na kuoza na kuharibika kwa kukosa soko.

"Tunaomba serikali itusaidie kukarabati hii barabara yetu, tunalazimika kutoa Sh. 8,000 mpaka 10,000 kusafirisha gunia moja la mboga kwa pikipiki kutoka Tchezema mpaka Kata ya Mlali kwenye soko kwa sababu malori hayaingii huku," alisema.

Ofisa Kilimo Kata ya Tchenzema, Luis Mpombo alisema wakulima wa tarafa hiyo wanazalisha karoti, maharage, nyanya, kabichi, njegere, mbaazi, kunde na aina zingine nyingi za mboga za majani lakini zinaharibika na kuoza shambani na nyingine majumbani kutokana na kukosa soko.

# 'Hatuwezi kuingia kwenye njaa kwa kuwaendekeza wakulima'

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amesema hayupo tayari kuliingiza taifa kwenye njaa kwa kuendekeza wafugaji, akipiga marufuku wafugaji kuingia kwenye maeneo ya wakulima.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na watumishi wa Halmashauri ya Madaba na Songea mwishoni mwa wiki, Kanali Thomas alisisitiza Mkoa wa Ruvuma si wa ufugaji, bali ni wa kilimo na unaongoza kitaifa kwa kuzalisha mazao ya chakula.

"Ruvuma sio mkoa wa wafugaji, ni mkoa wa wakulima, hatuwezi kuliingiza taifa kwenye njaa kwa kuendekeza wafugaji," alisisitiza.

Alisema operesheni ya kuondoa mifugo yote iliyoko katika maeneo ya wakulima itafanyika katika mkoa mzima kuanzia Desemba 10 mwaka huu.

Aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Madaba kuwatafuta wafugaji wenye makundi makubwa ya ng'ombe waliopewa dhamana baada ya mifugo yao kukamatwa ikila mazao ya wakulima ili walipe faini.

Mkuu wa Mkoa pia aliwapongeza wakulima wa Madaba kwa kutumia busara kwa kuwa wangechukua sheria mkononi, yangetokea maafa kati ya wakulima na wafugaji.

Alisisitiza wafugaji wote wasiokuwa na kibali waondolewe na hayuko tayari kuona kundi fulani linakandamiza makundi mengine.

Kiongozi huyo alisema uchunguzi umebaini kuwa hivi sasa wafugaji hawapandishi mifugo kwenye magari badala yake wanashusha ng'ombe Wilaya ya Njombe na kuingia nao kwa miguu mkoani Ruvuma, hivyo akamwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma kuwadhibiti wafugaji hao.

Aliagiza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa mifugo yote inayokamatwa na watoe taarifa kwake endapo kuna kiongozi yeyote anayekwamisha maagizo yake.

"Hatuwezi kuwa na viongozi wababaishaji ndani ya Mkoa wa Ruvuma ambao wanadhulumu haki za wananchi, nilishasema sitaki wafugaji kwenye maeneo ya wakulima," alionya.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Menasi Komba, alimshukuru mkuu wa mkoa kwa kuwadhibiti wafugaji katika maeneo ya wakulima.

Alisema tayari wamefanikiwa kuondoa mifugo zaidi ya 5,000 katika eneo la Kikunja, Kata ya Matimira na wanashirikiana na Jeshi la Polisi kuondoa mifugo hiyo katika maeneo mengine ya wakulima.

Mkoa wa Ruvuma unatajwa kuwa 'kapu la taifa la chakula', ukiongoza kwa uzalishaji chakula nchini kwa miaka minne mfu-

## RC ahimiza upandaji miti kukabili ukame

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amewataka wananchi kujenga utamaduni wa kupanda miti kwa wingi kwenye maeneo yanayowazunguka ili kukabiliana na ukame.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti mkoani humo uliofanyika katika eneo la mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana huko Butengwa, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, miti 500 ikipandwa.

Alisema miti ina faida nyingi ikiwamo kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuvuta mvua, akisisitiza wananchi wa mkoa huo wapande miti kwa wingi ili kukabiliana na ukame.

"Tusipopanda miti kwa wingi, hatuwezi kukabiliana na hali ya ukame na matokeo yake mvua inakuwa kidogo na tutakosa chakula," alitahadharisha.

Mkuu wa Mkoa pia aliwaagiza wakuu wa wilaya mkoani hapo kutoa elimu ya upandaji miti kwa wananchi na kuwaeleza faida yake pamoja na kuchukulia hatua dhidi ya wanaokata miti ovyo na kuharibu mazingira.

Pia aliziagiza halmashauri zote mkoani hapo kuhakikisha zinatenga maeneo maalum ya vitalu kwa ajili ya kuotesha miche ya miti ili wananchi wasisumbuke mahali pa kupata miche.

Baadhi ya wananchi walioshiriki upandaji miti, waliishukuru serikali kwa kuwapatia miti bila malipo kwa ajili ya kwenda kupanda kwenye makazi yao, huku wakiomba kudhibiti uchungaji holela maeneo ya mjini na kusababisha mifugo kula miti iliyopandwa.

# RUWASA yashtuka madhila wanawake kuliwa na mamba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) amemtaka wa Meneja wa wakala huo wilayani Ludewa mkoani Njombe, Mlenge Nasibu, kuandaa mradi mkubwa utakaotatua kero ya uhaba wa maji katika vijiji 17 vilivyoko mwambao wa Ziwa Nyasa ili kuwanusuru wanawake kuliwa na mamba wanapokwenda kuchota maji.

Clement Kivegalo alitoa agizo hilo juzi baada ya Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga kumweleza kwamba wanawake wanaliwa na mamba wanapokwenda kuchota maji katika Mto Ruhuhu na Ziwa Nyasa.

"Kwanza, sio jambo la kupendeza kusikia wananchi wanaokaa mwambao wanakosa maji. Kwa hiyo, tumemwagiza meneja aandae mradi na tumesisitiza uwe ni mradi mkubwa unaohudumia vijiji vyote kwa wakati mmoja.

"Sasa inategemeana na mhandisi anaweza akasema iwe miradi miwili au mradi mmoja au hata mitatu, inategemeana na jiografia ya hivyo vijiji.

"Ninaamini kabisa katika bajeti ijayo usanifu wa mradi huo utaanza, hatuna sababu ya kutesa wananchi ambao wanaishi ziwani, lazima tuwe na hali ya kusaidia kwa sababu suala la pampu ni la kiuhandisi, lazima itumike kuyatoa maji kule chini kuyaleta kwa wananchi, ni suala la kawaida," alisema.

Kivegalo alisisitiza miradi inaposanifiwa, wahakikishe inajengwa kwa gharama ndogo kadri inavyowezekana ili fedha za serikali zitumike kwenye maeneo mengine zaidi.

Awali Mbunge wa Ludewa, Kamonga, alimweleza mkurugenzi huyo kuwa wananchi wa Kijiji cha Kihogo wanakwenda kuchota maji katika Mto Ruhuhu ambao si salama kwa sababu ya shughuli za uchimbaji madini.

"Kule kuna uchimbaji wa makaa ya mawe na dhahabu, yale maji si salama. Pia wananchi wanaliwa na wanyama wakali, hasa mamba.

"Kijiji cha Kipingu wanaliwa sana na mamba, kwa hiyo maeneo kama hayo hatuwezi kuwaondoa mamba kwenye mto na hatuwezi kuwazuia wananchi wasiende kuchota maji kwa sababu maji hayana mbadala, suluhisho ni kuwapa wananchi maji ya uhakika ili wapunguze safari za kwenda kuchota maji ziwani na mtoni," alisema Kamonga.

Akisoma taarifa kwa mkurugenzi, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Ludewa, Nasibu, alikiri vijiji 17 vilivyoko mwambao wa Ziwa Nyasa havijawahi kupata majisafi na salama tangu uhuru.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka (wa pili kulia), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi wa Taasisi ya ESRF, Dk. Tausi Kida (kulia), Mtaalamu wa utalii, Dk. Shonga Mlozi (kushoto) na mshauri wa masuala ya fedha, Irene Madeje Mlola (wa pili kushoto), wakati wa kongamano la nne la Sneakers & Heels Exposition: Women & The Economy, lililofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ahoji sababu wazawa kuacha kuujenga mkoa wao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema anajiuliza ni kwanini wafanyabiashara wengi wa Moshi, wanakimbia kuujenga mji wao na kufanya biashara kwao, badala yake wanakwenda kuwekeza mikoa mingine ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Mbeya, wakati kuna vivutio vingi vya utalii na fursa za uwekezaji.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wafanyabiashara wa mkoa huo, wakati alipokwenda kuhitimisha kilele cha wiki ya shukrani kwa walipa kodi, iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Babu, alisema licha ya mkoa huo kuvuka malengo ya ukusanyaji wa kodi, anashangazwa na kitendo cha wageni wengi wanaoshuka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kwenda kulala Arusha na kurudi Moshi kwa kutumia magari.

"Wafanyabiashara wa Kilimanjaro, nawashukuru sana ninyi ambao mkoa hapa na mnashirikiana nasi kulipa kodi na kujenga uchumi wa kwenu. Nyie mnawekeza Kilimanjaro na mnatulipa kodi na ndio maana tunavuka malengo. Lakini wapo wafanyabiashara wazaliwa wa Kilimanjaro, wanakwenda kujenga Arusha, wanajenga Dodoma, wanajenga Dar es Salaam, wanajenga Mbeya.

"Sasa jamani yaani huu mkoa wenu hamuutaki, mnapeleka hela kwa watu wengine mnakimbia nyumbani kwenu? Mkurugenzi wa Fedha wa TRA, nimegundua tunapata wageni wengi sana hapa Kilimanjaro, wanalala Kilimanjaro lakini asubuhi wanakwenda Arusha, hao ni wafanyabiashara tena wazawa.

"Ina maana sisi hatuna nyumba za kulala hapa? Ehee tuambizane labda nyumba zetu zina kitu fulani ukilala hupati usingizi. Hapana! Nataka nitoe wito, nazungumza suala la vivutio na fursa za Mkoa wa Kilimanjaro. Nimesema tuna maeneo mengi, leo watalii wanakuja, mama amefungua nchi (Rais Samia Suluhu Hassan), wageni wengi wanakuja pale KIA, lakini wageni wote wanakwenda Arusha, huku wanakuja na magari. Naomba niwaambie msiwe na wasiwasi, mama Samia, amefungua nchi na niwaambie tu ukija kwangu ukileta tatizo lako nalitatua mara moja. Kwa hiyo mje, acheni kukimbia na hizi salaam zifike."

Kuhusu biashara ya magendo, alitangaza kuwa kuanzia sasa wakikamata magari na mali za magendo mkoani humo watazitaifisha na kuwa mali ya serikali. Kwa mujibu wa Babu mpaka kufikia sasa, katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, kuna magari manane na pikipiki yamekamatwa yakiwa na mali za magendo.

"Wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara za magendo waache mara moja. Naelekeza TRA kuongeza juhudi zaidi katika eneo hili la magendo ili kutokomeza tatizo hili ambalo sio la kiungwana kukwepa kulipa kodi. Ongezeni nguvu kwenye mipaka tuwakamate, tukishawakamata watu wanne, watano, wengine watajifunza," alisisitiza.

Awali, Meneja wa TRA, Mkoa wa Kilimanjaro, Masawa Masatu, akitoa taarifa yake alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021, TRA ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 227.72 sawa na ufanisi wa asilimia 108, wakati lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 210.52.

"Ongezeko hili ni ukuaji wa makusanyo ya mwaka uliopita, kwa asilimia 17. Mafanikio ya makusanyo haya ni matokeo ya Watanzania kuhamasika kulipa kodi zao kwa hiari kwa sababu wanatambua ndizo zinazotumika kupeleka huduma za jamii kwa nchi. Walipa kodi hawa walifanya kitu cha kizalendo bila ya kujali mdororo wa kiuchumi uliotokana na UVIKO-19 na vita vya Urusi na Ukraine kwa namna vimeathiri sana biashara katika dunia.

"Wiki hii tulikuwa tunatoa shukrani zetu kwa walipa kodi kwa kutoa misaada ya kijamii na leo tunawapongeza walipa kodi wa mkoa wetu waliofanya vizuri katika mwaka uliopita.

"Tumetoa magodoro 20 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, lakini tumetoa msaada wa vyakula katika Shule ya Msingi ya Mwereni, yenye wanafunzi wenye mahitaji maalum. Tumetembelea na kutoa msaada wa vyakula kwa makazi ya wazee wanaolelewa na serikali katika eneo la Njoro."

# Halmashauri yajizatiti kwa matibabu sumu ya nyoka

## • Dozi matibabu yake inagharimu 210,000/-

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mtwara mkoani Mtwara imesema sasa imejizatiti katika kutoa matibabu ya sumu ya nyoka kwa waathirika wa kung'atwa na nyoka baada ya kuwa kesi za aina hiyo mara kwa mara hasa kwa wakazi wa maeneo ya vijijini.

Mjini Mtwara jana, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Dk. Mathayo Malaika aliiambia Nipashe kuwa wameamua kuchukua hatua hiyo ya kuweka huduma hiyo kutokana na kuwapo malalamiko mengi hasa kwa wananchi ambao wanatoka vijijini, kukosa huduma hiyo wanapokumbana na tatizo hilo.

Dk. Malaika alisema kwa muda mrefu uongozi wa hospitali ulikuwa unafikiria kuweka huduma hiyo na sasa ipo, hivyo wananchi hawatakosa pindi wanapong'atwa na nyoka.

Alisema halmashauri tayari imeshaagiza dozi 25 za dawa ya kutibu sumu ya nyoka ambazo zimesambazwa katika Hospitali ya Nanguruwe na vituo vya kutolea huduma za afya.

Dk. Malaika alisema vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vitanufaika na mgawo huo wa dawa ya kutibu sumu ya nyoka ni pamoja na zahanati za Mahurunga, Kitere, Kilambo na Nalingu, hivyo kufanya huduma hiyo kuwa karibu na wananchi.

"Changamoto kubwa iliyoko ni bei ya hii dawa, kwenye vituo vyetu tutatoa dozi moja kwa Sh. 210,000 lakini kwa wale wenye bima kubwa ya NHIF wao watapatiwa bure, hivyo wananchi watakapokuwa wameng'atwa na nyoka, wawahi kwenye hospitali zetu," alisema.

Dk. Malaika alisema tayari uongozi wa hospitali umeshatoa maagizo kwa wataalamu wake kuwatangazia wananchi kwenye maeneo yao kuwa huduma hiyo inapatikana, hivyo wananchi wasisite kwenda kupata huduma pale wanapohitaji.

Alisema upatikanaji wa huduma hiyo ya matibabu ya sumu ya nyoka utapunguza au kuondoa kabisa malalamiko kutoka kwa wananchi ambayo yalidumu kwa muda mrefu kuhusu kukosa huduma hiyo.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, eneo lake la kazi lilikuwa na jumla ya kesi 15 za wananchi kung'atwa na nyoka zilizoripotiwa huku Kata ya Nalingu ikiongezeka kwa visa vya aina hiyo ikifuatwa na Kata ya Naumbu.

Salumu Liungu, mkazi wa Kijiji Naumbu, alipongeza serikali kwa kuweka huduma hiyo ya matibabu ya sumu ya nyoka katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa wananchi walikuwa wakihaingaa kupata huduma hiyo kwa muda mrefu.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (wa nne kushoto) akiwa pamoja Mkurugenzi Mtendaji wa Bora Rx Medicine, Margareth Maganga (wa tatu kulia), katika makabidhiano rasmi ya moja kati ya vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 48 kwa ajili ya Zahanati ya Gerezani, Ilala, Dar es Salaam juzi. (Wa tano kushoto) ni Mwekezaji kutoka Bora Fx Medicina, Elmira Hadzhykhanova. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako wanasa viroba vya mkaa

**Na Hamisi Nasri,** NANYAMBA

ZAIDI ya viroba 220 vya mkaa wilayani Nanyamba mkoani Mtwara vimenaswa wakati wa operesheni maalumu iliyofanywa na halmashauri hiyo kuwasaka watu wanaojihusisha na biashara ya mazao ya misitu kinyume cha sheria.

Operesheni hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki kupitia kikosi kazi cha Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba kwa kushirikiana na Idara ya Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira.

Akizungumzia operesheni hiyo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, Shija Mashamba, alisema wamefanikiwa kukamata zaidi ya viroba 220 vya mkaa kutoka kwa watu ambao wanakata miti na kuharibu misitu.

Mashamba alisema lengo la operesheni hiyo ni kuhakikisha misitu na mazingira yanahifadhiwa ipasavyo na jamii inakuwa na uelewa wa kutosha katika kuhifadhi misitu na mazingira kwa ujumla ili kulinda uoto wa asili.

Alisema wamefanya operesheni hiyo katika meneo mbalimbali, hasa vijijini ambako kwa kiasi kikubwa kumekuwa na uharibu mkubwa wa mazingira na ukataji miti.

"Huu ni mwendelezo wa operesheni za kukamata mazao ya misitu kwa wale wanaofanya shughuli hizo bila ya kufuata taratibu na sheria zilizoko, hivyo tunatoa wito kwa jamii kutunza misitu pamoja na mazingira, tuache kukata miti ovyo," alisema.

Mashamba alisema kitendo cha kukata miti na kuchoma mkaa bila kufuata sheria ni kosa kwa mujibu wa sheria na yeyote atakayekutwa akifanya hivyo, sheria itachukua mkondo wake.

Alisema halmashauri itaendelea kuwasisitiza wananchi wa mji wa Nanyamba kuendelea kutunza misitu asili na mazingira kwa kuwa ukataji miti kiholela ni chanzo cha ukame wa kuharibu vyanzo vya maji.

Hata hivyo, Mashamba alisema hawajafanikiwa kuwanasa wahusika wa mkaa huo ambao halmashauri umeukamata, akisisitiza kuwa msako unaendelea ili wafikishwe mahakamani.

# Trilioni 1.2/- kukusanywa mkoa wa kikodi Ilala

**Na Grace Gurisha**

KAIMU Meneja Mkoa wa Kikodi wa Ilala, Masau Malima, amesema kwa mwaka huu wa fedha wanatarajia kukusanya Sh. trilioni 1.25 kutokana na ushirikiano wanaoupata kutoka kwenye makundi mbalimbali ya walipakodi.

Malima alibainisha hayo jana baada ya kukabidhi zawadi mbalimbali kwenye kituo cha watu wenye mahitaji maalum cha Missionary Charity kilichoko Mburahati mkoani Dar es Salaam.

Alisema mkoa huo wa kikodi unaendelea kufanya shughuli zake za kukusanya mapato, akibainisha kuwa hadi kufikia Oktoba mwaka huu, ufanisi wao ulikuwa ni wa asilimia 104.5 katika lengo ambalo walikuwa wamepangiwa.

Malima alisema mkoa wao umeendelea kuonyesha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kukiwa na ukuaji wa makusanyo kwa zaidi ya asilimia 25 kulinganisha na mwaka uliopita.

"Kama unavyokumbuka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tangu Novemba 13, mwaka huu, tulianza kuadhimisha siku ya shukrani kwa mlipakodi, kipindi hiki kinaendelea hadi kufikia Novemba 30, mwaka huu.

"Tumekuja hapa kuleta zawadi mbalimbali na shukrani, lengo likiwa ni moja tu zisaidie katika shughuli zinazoendelea hapa, sisi kama sehemu ya jamii tumeguswa sana na makundi haya," alisema Malima.

Kiongozi huyo pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na baraza lake la mawaziri kwa miongozo mbalimbali ambayo imekuwa ikitolewa hasa katika taasisi yao.

Mzee Joachim Mkila alisema ana miaka tisa katika kituo hicho, akishukuru kwa kupewa msaada huo na kuwashukuru watu wote wanaokipatia msaada kituo hicho.

"Tunamshukuru sana kwa zawadi hizi, mmetusaidia kwa kila kitu, hapa hakiuzwi kitu kikiingia kimeingia, hapa tupo wengi ukihesabu sahani hata 100 zinafika, tunaomba na watu wengine kutoa msaada kama huu," alisema Mkila.

**Kiongozi huyo pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na baraza lake la mawaziri kwa miongozo mbalimbali ambayo imekuwa ikitolewa hasa katika taasisi yao.**



## Afa maji akijipiga picha maporomoko ya maji

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MKAZI wa Balang'a, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, Athuman Rashid, amepoteza maisha baada ya kufa maji, wakati akijipiga picha (selfie) katika eneo lililokuwa likipokea maji yaliyokuwa yakiporomoka kutoka milimani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP), Henry Mwaibambe, alisema marehemu Athuman, alipatwa na mkasa huo mwishoni mwa wiki akiwa katika Kata ya Kisangasa.

"Huyo Athuman yeye alipoteza maisha, baada ya kusombwa na maji yaliyokuwa yakiporomoka kutoka milimani kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. Inaelezwa kuwa maji hayo yalikuwa yakielekea Mto Balang'a yaliwavuta wananchi wengi kusogea karibu kushangaa maji hayo na ndipo marehemu alipoamua kuyakanyaga ili kujipiga picha na ndipo maji hayo yalipomzidi nguvu na kumzamisha majini," alisema.

Aidha, Kamanda Mwaibambe, alisema katika tukio jingine, mkazi wa kijiji cha Kibirashi, wilayani humo, Sandalo Mndaila, amekutwa amefariki dunia baada ya kujinyonga juu ya mti.

Alisema mwili wake ulikutwa alfajiri ya Novemba 25, mwaka huu, ukiwa unaning'inia katika maeneo yanayotumika kufyatulia matofali kwa ajili ya shughuli za ujenzi, huku akiwa ameacha ujumbe unaosema kifo chake kisihusishwe na mtu yeyote, ndugu wala mkewe kwa kuwa huo ni uamuzi wake binafsi.

Wakati huo huo, Kamanda Mwaibambe, alisema Jeshi la Polisi, linachunguza tukio la kucharangwa mapanga na kuchomwa kisu sehemu mbalimbali za mwili wake, mkazi wa Kwamwande, wilayani Kilindi, Bakar Omar, baada ya kuvamiwa na watu wasiojulikana.

Kamanda Mwaibambe, alisema Omar maarufu kama 'wembe' alikutwa na alishambuliwa na watu hao juzi alfajiri akiwa katika kituo kikuu cha mabasi cha Songe kilichoko Wilaya ya Kilindi.

Mmoja wa ndugu wa Wembe, Bakar Amani, akizungumzia tukio hilo, alisema ndugu yao alipata mkasa huo Novemba 25, mwaka huu, majira ya alfajiri ya saa 12.45 na alionekana akiwa hayupo katika hali yake ya kawaida, huku akiwa anavuja damu.

"Huyu ndugu yetu ana matatizo ya akili, alipita maeneo ya bodaboda, lakini alikuwa dhaifu na ametapakaa damu na walipomchunguza waligundua ana majeraha makubwa kichwani, mikono yote na mgongoni.

"Baada ya kuona hali yake sio nzuri, wasamaria wema walimkimbiza katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Songe inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kupatiwa tiba."




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere, akikabidhi tuzo ya cheti cha kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mati Super Brands Limited, David Mulokozi, mwishoni mwa wiki alipoibuka mshindi wa pili kwa walipakodi bora mkoani humo, tuzo zilizotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Manyara. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mashirika yabaini upungufu mpango kazi kutokomeza ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MASHIRIKA 18 ya kiraia yanayopigana kufa na kupona katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, kuhakikisha matukio ya ukatili wa kijinsia yanapungua au kukoma, yamebaini kuwa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), uliokuwa ukitekelezwa na serikali kuanzia Julai mwaka 2018 hadi Juni 2022, una upungufu kuliko mafanikio.

Upungufu huo ni pamoja na kuwapo ukinzani, kati ya Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, ambayo inawapa watuhumiwa wa makosa ya ukatili, upenyo wa kukwepa sheria.

Jana, wakati anawasilisha madai matano ya jamii katika kikao cha jukwaa la kisera lililoandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO ili kuisukuma serikali kuja na majibu ya upungufu yanayochangia utekelezaji wa sera na sheria, Jackson Muro, alisema ili wanawake washiriki fursa za kiuchumi na kimaendeleo na watoto kustawi, kusoma vyema na kukua katika maadili, utu wao kulindwa na kuthaminiwa, hawana budi kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa MTAKUWWA, ambao ukifanyiwa kazi vizuri, utakomesha vitendo vyote vya ukatili, kwa kuwa vina athari kubwa kwa afya ya akili na mwili.

Alisema katika kutafuta suluhu ya kudumu ya upungufu huo, dai la kwanza wanalotaka kufanyiwa kazi ni serikali kuzielekeza halmashauri kutenga rasilimali fedha zitakazoratibu utekelezaji wa MTAKUWWA, ngazi ya kata, mitaa na vijiji kwa kutumia asilimia mbili ya mapato ya ndani.

Dai la pili, ni kuimarisha uwezo wa wanakamati wa MTAKUWWA, watoa huduma (mfano, vituo vya afya, polisi), watoa ushauri nasaha na kisaikolojia), kwa kutumia mbinu mbalimbali za kusaidia waathirika wa ukatili wa kingono.

Wakati dai la tatu ni usambazaji na uelimishaji wa Mwongozo wa Taifa wa Makuzi na Malezi, ambao utaruhusu maofisa ustawi wa jamii wa wilaya na kata kunolewa kwa mafunzo ili na wao waweze kuelimisha wazazi, walezi, walimu na jamii kwa ujumla kwenye maeneo yao ya kazi, kwa lengo la kupunguza vitendo vya ukatili katika malezi.

Aidha, Muro alilitaja dai la nne, ni kuunda na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za kuzuia ukatili wa kingono na vichochezi vyake. Wakati dai la tano, ni kupatikana kwa sheria moja inayoshughulikia ukatili wa kijinsia Tanzania ili kuondoa ukinzani uliopo kwa sasa, kati ya Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu ambayo inawapa watuhumiwa upenyo wa kukwepa sheria.

"Madai yote haya na mengine kwa mfano ya kutochukuliwa hatua stahiki za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa makosa ya ukatili kijinsia na kingono, ndiyo yanayosababisha hivi sasa tutembee na kauli mbinu inayosema, utekelezaji wa sheria, sote tuwajibike kutokomeza ukatili wa kingono," alisisitiza.


Kabla ya kuwasilishwa madai hayo, Mkurugenzi wa Shirika la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa alisema, shirika hilo linatamani kuiona jamii yenye furaha na inayopata haki sawa kwa makundi yote bila kuangalia huyu ni mwanamke, huyu ni mwanamume au huyu ni mtu mwenye ulemavu tunataka apate haki zake kwa kuheshimu ule utu wake aliopewa na mwenyenzi Mungu, na haki hizo zichochee yeye kupata maisha bora na ustawi endelevu.

Akijibu madai hayo, Naibu Meya wa Manispaa ya Moshi, Stuwart Nathaniel, alisema katika kuhakikisha mwanamke na mtoto wanalindwa dhidi ya ukatili wa kingono, wanaunga mkono juhudi zinazofanywa na TUSONGE CDO katika kupambana na vichochezi vya kingono na kulinda utu wao na kwamba jambo hilo hata wao wanatamani lipate ufumbuzi, kwa kuwa linachochewa na ukosefu wa kipato.

"Ukosefu wa kipato unahatarisha kila uchao maisha ya wasichana, ukiwashawishi kufanya ngono ili kupata ujira. Niwapongeze kwa kuendelea kuboresha vipato vya walengwa hawa, kwa sababu hapo ndiko shina la ukatili limelala na watu wengi hasa, wanaume wanatumia udhaifu huo kuwarubini wasichana wadogo, lakini kama ambavyo TUSONGE CDO wamewezesha kuanzisha shughuli za ujasiriamali na sisi kama Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, tunatazama namna ya kuwaunga mkono. Tuna haja ya kuendelea kuwafikia watu wengi zaidi kwa kuwa watu wengi walikuwa hawajaufahamu mpamgo huu," alisema.

Kuhusu kutengwa kwa asilimia mbili ya fedha za mapato ya ndani, Naibu Meya huyo, alisema amekubaliana na jukwaa hilo la sera kwamba, jambo hilo ni jema, hivyo ni lazima huo mpango utengewe fedha ya kuanzisha shughuli ili wakati serikali inawaomba wadau wengine wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi wasaidie, watakuwa wanasaidia katika hatua inayofuata.

Kutokana na dai hilo, aliahidi kulipeleka katika Baraza la Madiwani ili likajadiliwe na kuona namna bora ya kuliweka, lakini ataliwasilisha kwa wabunge ili walipeleke Bungeni kujadiliwa na kupata ridhaa ya Bunge.





# Ripoti moto Mlima Kilimanjaro yaeleza chanzo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA), limetoa ripoti yake ya uchunguzi wa moto uliozuka Oktoba 21, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, ikisema ulisababishwa na shughuli za binadamu.

Kamishna Mkuu wa Uhifadhi wa TANAPA, Willium Mwakilema, akitoa taarifa hiyo kwa umma, alisema wakati moto huo ukiteketeza mimea na ikolojia ya hifadhi hiyo, hakuna madhara yoyote yaliyotokea kwa watalii, waongoza watalii, wapangazi pamoja na miundombinu ya barabara wanazotumia watalii wakati wa kupanda Mlima Kilimanjaro.

"Moto huo umeteketeza kilomita za mraba 34.2 za uoto wa asili kwenye eneo la Mlima Kilimanjaro, ambalo lina mimea aina ya Erica na Protea, inayoshika moto kwa kasi kutokana na ukame. Hivi sasa hali ni shwari katika hifadhi hiyo.

"Hata hivyo, taarifa za awali zimebaini kuwa chanzo cha moto huo ni shughuli za binadamu. Kitengo cha Usalama cha TANAPA, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama, vinaendelea na utafiti ili kubaini wahusika wa tukio hilo.

"Pia tulifungua jalada la uchunguzi katika Kituo Kikuu cha Polisi Moshi lenye kumbukumbu namba, MOS/RB/RB/9563 2020 na MOS/IR/877. Kwa minajili hiyo, atakayebainika pasi na shaka kuhusika na tukio hilo, atachukuliwa hatua stahiki ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia ya kusababisha moto katika hifadhi hiyo."

Kwa mujibu wa Mwakilema, uwapo wa moto huo ambao ulizuka katika eneo la Karanga, majira ya saa 2:30 usiku wa Oktoba 21, mwaka huu, TANAPA ilipata taarifa kupitia kwa Mwalimu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (Mweka) kutokana na bonde hilo kuonekana vizuri kutokea maeneo ya chuo hicho.

Alisema kazi ya kuzima moto huo, iliyoanza Oktoba 22, mwaka huu, haikuwa kazi rahisi, lakini hadi Oktoba 28, mwaka huu moto huo ulidhibitiwa katika maeneo mengi korofi na Oktoba 29 ulilipuka tena eneo la Mto Karanga na kusambaa kuelekea maeneo ya Umbwe na Baranco kutokana na upepo mkali uliosabaisha kulipuka mioto midogo iliyokuwa kwenye magogo ardhini yaliyokuwa yametengeneza mboji".

"Usiku wa Oktoba 29, mwaka huu moto mpya uliwaka eneo la Mandara, upande wa Marangu na kusambaa kushuka msitu wa asili, lakini kutokana na upepo mkali uliokuwa unabadilisha mwelekeo mara kwa mara ulisambaa kuelekea kwa Masheu na Mlima Kifinika, lakini hadi Novemba Mosi, mwaka huu kumekuwa na mafanikio makubwa ya kudhibiti moto huo na hadi sasa hakuna eneo lolote lenye moto na askari wetu wanaendelea na ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya mlima huo," alisema.

Aidha, Mwakilema alisema katika harakati za kuzima moto huo walikumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo makorongo makubwa ambayo ni vigumu kuyafikia kwa miguu hususani makorongo ya Karanga, Baranco, Umbwe, Lyamungo na Mweka.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni pamoja na uzoefu mdogo wa uzimaji moto kwenye mazingira ya milimani hususani kwa wadau ambao hawana uzoefu wa kupanda mlimaukame, upepo mkali, uwapo wa mimea ya Erica inayoshika moto haraka, mrundikano wa mboji kwenye udongo iliyokuwa inahifadhi moto ardhini.

Kuhusu madhara kwa watalii, waongoza watalii, wapagazi pamoja na miundombinu ya barabara zinazopitwa na watalii, Mwakilema alisema hakukuwa na madhara yoyote, lakini ilileta hofu kwa watalii na wananchi kutokana na taarifa za moto huo kutangazwa na vyombo vya kimataifa.

"Hakuna madhara yoyote kwa watalii kwa sababu moto uliwaka maeneo ya mbali na wanapopita watalii, lakini hakuna watalii waliofuta au kuahirisha safari za kwenda hifadhi hiyo kutokana na moto huo na hivi sasa hali ni shwari," alisema.

Kwa upande wa madhara, Mwakilema alisema sehemu ya hifadhi ya mlima huo yenye mimea ya Erica na Protea zaidi ya kilomita 34 zimeteketea kutokana na aina hiyo ya mimea kushika moto kwa kasi kutokana na ukame.

"Eneo la kilomita za mraba 34.2 za eneo lenye mimea ya Erica na Protea yameteketea kwa moto, mimea inayohifadhi maji ardhini imeteketea kwa moto kwenye maeneo moto ulikowaka, madhara ya kiikolojia pamoja na wanyama wadogo wagodo kufa kutokana na moto huo," alisema.



Kamati ya kuratibu miradi inayotekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania Mgera AP, ikikagua mradi wa maji wa Kijiji cha Saunyi, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, kutoka kulia ni mwezeshaji wa miradi, Biana Philimon, Meneja World Vision, Modest Kessy, Ofisa Tarafa ya Mgera, Goodluck Kimaro, Shekh Mngoya na Katibu, Athuman Mngoya. **PICHA: DEGE MASOLI**

# 'Pochi la Mama' lakamilisha vyumba vinne vya madarasa

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha, imekamilisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mringa, ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo unaoanza Januari mwaka ujao.

Ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa, uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 80, zimetolewa na serikali kuu kupitia mradi wa 'Pochi la Mama'.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mringa, Salum Magaka, alisema kiasi cha fedha hizo zimetumika kujenga vyumba vinne vya madarasa, meza na viti 160.

Aidha, alisema kukamilika kwa wakati kwa mradi huo, ni kutokana na uhitaji wa madarasa hayo na ari ya usimamizi wa kazi na kujituma kwa kamati ya ujenzi na kwa kushirikiana na wataalamu.

Pia ujenzi huo, umetumia mafundi jamii 'Force Akaunt' kwa kuwa ni maelekezo ya serikali kushirikisha jamii wakati utekelezaji wa miradi.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo, kutasaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi darasani na kuongeza kiwango cha ufaulu, pia kurahisisha mazingira ya walimu kufundisha.

"Tunaishukuru serikali kwa kutoa fedha za ujenzi huu, shule yetu ilikuwa na uhitaji wa vyumba vinne vya madarasa, fedha zimeletwa kwa idadi inayolingana na uhitaji, uwapo wa madarasa ya kutosha itasaidia kurahisisha tendo la kujifunza kwa wanafunzi na kufundisha kwa walimu, sambamba na mazingira bora ambayo yatachangia wanafunzi kupenda shule," alisema.

Shule ya Sekondari Mringa ni miongoni mwa zinazofanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa kwa kidato cha nne na cha sita, ina jumla ya wanafunzi 1,754.

# TRA yakusanya zaidi ya tril. 22/- mwaka 2021/22

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA), imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. trilioni 22.28 katika mwaka wa fedha 2021/2022, sawa na asilimia 99.22, huku ikiagiza maofisa wake nchini kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ili kuiwezesha serikali kutekeleza kwa tija wajibu wake wa kuboresha huduma za jamii.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika mji wa Babati, mkoani Manyara, wakati wa kuhitimisha kilele cha wiki ya mlipa kodi, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Richard Kayombo, alisema makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la Sh. trilioni 4.13 kutoka Sh. trilioni 18.15, iliyokusanywa mwaka wa fedha uliopita.

"Hapa jambo la ulipaji kodi mnalifanya kuwa ni ajenda ya kudumu na walipa kodi ni washirika na siyo adui wa TRA. Kwa mwaka huu tumepangiwa kukusanya Sh. trilioni 23.6 na makusanyo ya TRA ndio yanategemewa na serikali kwa asilimia 60 ili iweze kujiendesha.

"Niwapongeze walipa kodi wa Mkoa wa Manyara, kwa sababu mmekuwa na mchango mkubwa katika ulipaji wa kodi, licha ya kuwapo tatizo la ugonjwa wa UVIKO-19 na vita dhidi ya Urusi na Ukraine."

Katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema serikali itaendelea kuwawekea mazingira wezeshi wafanyabiasahara pamoja na kuziba mianya ya rushwa na kutokuruhusu watu wachache wakafaidika na wengi wakabaki kuumia.

Makongoro, alisema wafanyabiashara wanapolipa kodi, wanampa nguvu Rais Samia Suluhu Hassan, kufanikisha shughuli mbalimbali za maendeleo na kwamba tuzo walizozipata zinaongeza ari ya kulipa kodi zaidi.

Awali, Meneja wa TRA wa Mkoa wa Manyara, Pendolake Msangi, aliwashukuru walipa kodi wa Manyara, akisema kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 walikusanya Sh. bilioni 27.8, sawa na asilimia 89, wakati lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 31.3.

Vilevile, Msangi, alisema lengo la TRA kutoa tuzo hizo ni kuwatia moyo wafanyabiashara ili kazi ya ukusanyaji mapato iweze kufanyika, lakini kitu kilichowasaidia wakafanya vizuri kwenye robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 kukusanya Sh. bilioni 12.87, ni wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari.

Nipashe
Spotika



NYOTA WA5 WALIOSHANGAZA KOMBE LA DUNIA HADI SASA UK. 16



# NYEKUNDU QATAR...

Kipa wa Wales, Wayne Hennessey, akimchezea rafu mbaya, mshambuliaji wa Iran, Mehdi Taremi, katika mechi ya Kundi B ya Kombe la Dunia nchini Qatar Ijumaa iliyopita, ambayo ilimalizika kwa Iran kushinda 2-0. Hennessey alionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 86 na kuwa mchezaji wa kwanza kuadhibiwa kwa kutolewa kwa kadi nyekundu kwenye michuano hiyo mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**



## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa Ufaransa, Karim Benzema, amekuwa mshindi wa kwanza wa tuzo ya Ballon d'Or kukosa fainali hizo tangu Allan Simonsen raia wa Denmark kushindwa kufuzu kwa michuano hiyo ya mwaka 1978.

# NYOTA WA4 WALIOZIATHIRI TIMU KUKOSEKANA QATAR

Kocha Didier Deschamps anamkosa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, na kukosekana kwake katika safu ya kiungo kumeonyesha wazi kuathiri uchezaji wa Ufaransa.

Kante amekuwa nje ya uwanja kwa miezi kadhaa na ameichezea Chelsea mara mbili pekee katika michuano yote msimu huu.

**N'Golo Kante (Ufaransa)**



**DOHA, Qatar**

MCHEZO wa kwanza wa Kombe la Dunia Qatar 2022, ulichezwa Novemba 20, mwaka huu na toleo la mwaka huu litadumu hadi Desemba 18, 2022, fainali itakapochezwa.

Toleo la 2022 linashirikisha mataifa 32 kutoka mabara kadhaa na litakuwa la mwisho kwa wachezaji kadhaa wa daraja la juu kama Cristiano Ronaldo, Lionel Messi na Karim Benzema.

Lakini wachezaji kadhaa wamekosa Kombe la Dunia la Qatar 2022 kutokana na majeraha waliyopata wakati wa kampeni ya kufuzu.

Makala haya yanawaangazia wachezaji wanne ambao kukosekana kwao kunaweza kuathiri uchezaji wa taifa lao kwenye Kombe la Dunia, twende sasa...

**#4. N'Golo Kante (Ufaransa)**

Mfaransa huyo ni mmoja wa wachezaji ambao kukosekana kwao kumeonekana kuiathiri Ufaransa kwenye Kombe la Dunia la Qatar 2022.

Kante amekuwa nje ya uwanja kwa miezi kadhaa na ameichezea Chelsea mara mbili pekee katika michuano yote msimu huu.

Kante alikuwa kiungo muhimu, na ustadi wake wa ulinzi uliisaidia Ufaransa kushinda Kombe la Dunia la Urusi 2018.

Kocha Didier Deschamps anamkosa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, na kukosekana kwake katika safu ya kiungo kumeonyesha wazi kuathiri uchezaji wa Ufaransa.

Hii inatokana na wazo kwamba mbadala wake, Aurélien Tchouaméni, hana uzoefu katika mashindano haya. Pia Ufaransa inamkosa kiungo mshambuliaji, Paul Pogba.

**#3. Borja Iglesias (Hispania)**

Huyu ni mmoja wa washambuliaji waliofanya vizuri zaidi barani Ulaya msimu huu, lakini hakuchaguliwa katika kikosi cha Hispania kwenye Kombe la Dunia na kocha Luis Enrique.

Iglesias amefikisha mabao nane na kusajili asisti tatu katika mechi 17 alizocheza msimu huu.

Alvaro Morata ndiye mshambuliaji pekee wa asili katika kikosi cha Hispania, na hii inaweza kuwasumbua Wahispania kwa sababu ikiwa Morata atapata majeraha, hakuna mbadala wa mshambuliaji wa asili kwenye kikosi.

Kubadilisha fowadi wa nje kama Yeremy Pino na kuchukua nafasi ya mshambuliaji wa kiwango kama Iglesias huenda lingekuwa chaguo salama zaidi.




Sadio Mane

**#2. Christopher Nkunku (Ufaransa)**

Mshambuliaji huyo awali alichaguliwa katika kikosi cha Ufaransa, lakini alilazimika kujiondoa kutokana na jeraha alilolipata wakati wa mazoezi.

Nkunku amefunga mabao 16 na kusajili bao moja katika mashindano yote akiwa na RB Leipzig msimu huu.

Christopher Nkunku ametoka katika michuano ya Kombe la Dunia baada ya kupata jeraha la goti wakati wa mazoezi ya Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Ukilinganisha uchezaji wake na washambuliaji kadhaa wa Ufaransa kama Karim Benzema na Olivier Giroud, utagundua kuwa amefanya vema zaidi yao msimu huu.

Kutokuwapo kwake kunaongeza orodha kubwa ya wachezaji wa daraja la juu kutoka Ufaransa ambao wanakosa mashindano. Kwa hivyo, Ufaransa itakosa uthabiti wa kufunga na ufahamu wa Nkunku, ambao unaweza kuathiri ustadi wao wa kushambulia.

**#1. Sadio Mane (Senegal)**

Msenegal huyo bila shaka ni mmoja wa wachezaji bora wa sasa wa Kiafrika na ndiye mchezaji mwenye ushawishi mkubwa na mzoefu wa Senegal.

Sadio Mane amefunga mabao tisa na kusajili asisti nne katika mechi 22 alizoichezea Bayern Munich msimu huu.

Mane alikuwa muhimu kwa Senegal kwani uchezaji wake ulisaidia taifa lake kupata taji la Kombe la Mataifa ya Afrika mnamo 2021.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, awali alichaguliwa katika kikosi cha Senegal kinachoshiriki Kombe la Dunia licha ya jeraha lake, lakini alilazimika kujiondoa kutokana na kufanyiwa upasuaji.

Kukosekana kwake ni pigo kubwa kwa Senegal, na bila shaka hakuna mchezaji anayeweza kuchukua nafasi yake katika kikosi cha kwanza. Kwa hivyo, kutokuwapo kwake kumeliathiri taifa lake.

KOMBE LA DUNIA QATAR 2022

# MAKOCHA WA5 BORA KOMBE LA DUNIA


Tite

**DOHA, Qatar**

FAINALI za Kombe la Dunia la FIFA za 2022, zilianza Jumapili ya Novemba 20, mwaka huu na Ecuador iliwafunga wenyeji, Qatar 2-0 katika mechi ya ufunguzi. Timu 32 zinapambana ili kunyakua zawadi kubwa zaidi ya mchezo huo mwezi ujao.

Mashabiki wa soka wanasubiri kwa hamu kuona wachezaji bora katika mchezo wakiingia vitani. Lakini nafasi ya timu yoyote kuwa na mbio nzuri kwenye mashindano, itaamuliwa sana na akili za busara zinazofanya kazi pembeni.

Ndio maana umuhimu wa makocha katika mashindano kama Kombe la Dunia hauwezi kupuuzwa. Hapa tunaangalia makocha bora kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

**#5. Didier Deschamps (Ufaransa)**

Didier Deschamps aliiongoza Ufaransa kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia 2018. Mchezaji huyo wa zamani wa Ufaransa, amefanya kazi nzuri sana akiwa kocha wa 'Les Bleus' hao, na kuiongoza timu hiyo kushinda mara 84 katika mechi 132. Ana kiwango cha ushindi cha asilimia 63.64.

Deschamps pia aliiongoza timu ya Ufaransa kwa ushindi wa 2020-2021 kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa. Kwa urahisi ni mmoja wa makocha waliofanikiwa zaidi kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Hata hivyo, Deschamps anakabiliwa na kibarua kigumu cha kukiongoza kikosi chake kutetea ubingwa kwa mafanikio wakati huu. Ufaransa si kikosi chenye nguvu kama ilivyokuwa miaka minne iliyopita. Wamefanikiwa kupata ushindi mmoja pekee katika mechi zao sita zilizopita kwenye mashindano yote kabla ya Kombe la Dunia.

**#4. Lionel Scaloni (Argentina)**

Argentina ni moja ya timu zinazoangaliwa sana kwenye Kombe la Dunia na hiyo inatokana na ukweli kwamba hii inaweza kuwa michuano ya mwisho kwa Lionel Messi. Lakini pia kuna sababu nyingine za mashabiki wa Argentina kushangilia.

Argentina waliingia kwenye michuano hiyo wakiwa hawajafungwa katika mechi 36 kabla ya Saudi Arabia kuivunja rekodi hiyo kwa kuwachapa 2-1 na pia wana kikosi kilichojaa nyota wengi. Kocha wao Lionel Scaloni alikuwa bidhaa isiyojulikana sana katika duru za kimataifa, lakini kwa hakika amethibitisha thamani yake katika miaka michache iliyopita.

Scaloni aliwaongoza 'La Albiceleste' hao kutwaa ubingwa wa Copa America mwaka 2021 na kumaliza ukame wa miaka 28 katika mashindano hayo. Timu ya Scaloni ya Argentina imeshinda michezo 33 kati ya 48 katika mashindano yote hadi sasa kabla ya Kombe la Dunia.

**#3. Tite (Brazil)**

Brazil inatazamwa na watu wengi kama wenye nafasi kubwa zaidi kutwaa kombe hili mwaka huu. Wana moja ya kikosi bora kwenye mzunguko wa kimataifa hivi sasa na wachezaji wao wengi wako katika hali nzuri. Tite pia aliiongoza Brazil kunyakua taji la Copa America 2019 na amefanya kazi nzuri na timu hiyo katika miaka ya hivi karibuni.

Mwanafunzi huyo nguli Luiz Felipe Scolari, Tite ameifanya Brazil kuwa timu namba moja duniani kwa viwango vya FIFA. Rekodi ya Tite inajieleza yenyewe. Chini ya ukufunzi wake, Brazil wameshinda mechi 57 kati ya 76 katika mashindano yote na kocha huyo wa Brazil ana kiwango cha ushindi cha asilimia 75.

**#2. Luis Enrique (Hispania)**

Luis Enrique ni mmoja wa makocha bora na wenye uzoefu zaidi katika Kombe la Dunia. Enrique alipata mafanikio mengi akiwa na Barcelona kati ya 2014 na 2017 kabla ya kuchukua nafasi ya ukocha mkuu wa 'La Roja' hao.

Enrique bila shaka ndiye mtu anayefaa kuwa kocha wa Timu ya Taifa ya Hispania. Kutokana na kipindi chao cha mafanikio zaidi katika soka la kimataifa, Hispania ilidorora baada ya ushindi wao wa Euro 2012.

Lakini Enrique anaonekana kufufua kikosi hicho, na hadi sasa ameiongoza timu hiyo ya Hispania kushinda mara 19 katika mechi 35. Chini ya uongozi wake, Hispania wamepoteza mechi nne pekee katika mashindano yote.

Anatumaini kwamba kwa kuzungumza moja kwa moja na mashabiki, ataweza kuwapa maarifa ambayo hapo awali yalitolewa kwa vyombo vya habari pekee.

Lakini Enrique anaonekana kufufua kikosi hicho, na hadi sasa ameiongoza timu hiyo ya Hispania kushinda mara 19 katika mechi 35. Chini ya uongozi wake, Hispania wamepoteza mechi nne pekee katika mashindano yote.

**#1. Hans-Dieter Flick (Ujerumani)**

Hans-Dieter Flick alithibitisha sifa zake za ukocha kwa ushindi wa kihistoria na Bayern Munich katika msimu wa 2019-20. Baada ya miaka miwili ya mafanikio makubwa kama kocha mkuu wa Bavaria hao, Flick alichukua jukumu la kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani.

Kombe la Dunia la FIFA la 2022 ni michuano ya kwanza ya kimataifa wa Flick mbali na Ligi ya Mataifa ya UEFA. Ujerumani imekuwa timu ya kutisha chini ya kocha wao mpya, ikishinda 10 na kupoteza mara moja tu katika mechi 16 za mashindano yote hadi sasa.

## NJE YA UWANJA

MAKIPA bora watano walioachwa Kombe la Dunia; #1 David de Gea (Hispania), #2 Dean Henderson (England), #3 Jasper Cillessen (Uholanzi), #4 Zack Steffen (Marekani) na #5 Mitchell Langerak (Australia)



# NYOTA WA5 WALIOSHANGAZA KOMBE LA DUNIA HADI SASA



Kipa wa Japan, Shuichi Gonda, akifanya yake dhidi ya mshambuliaji wa Ujerumani, David Raum, kwenye mechi ya Kombe la Dunia Qatar wiki iliyopita wakati wakishinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la FIFA la 2022 nchini Qatar, linajumuisha kundi la watu wenye vipaji vya hali ya juu. Lakini mwisho wa siku, mpira wa miguu ni mchezo wa timu na wachezaji wote 11 uwanjani watahitaji kuchangia vya kutosha kwa sababu ya kawaida ikiwa timu itafanikiwa.

Ingawa mataifa mengi yanaweza kujivunia kuwa na wachezaji bora katika vikosi vyao, si kila upande una ubora ulioenea katika nafasi mbalimbali. Hata magwiji wa mchezo huo watahitaji kuungwa mkono ili kuleta mchezo wao.

Baadhi ya nyota wasiotarajiwa wameibuka katika wiki ya kwanza ya mchezo wa Kombe la Dunia nchini Qatar.

Mashabiki wa soka tayari wamekabiliwa na matukio mawili makubwa, huku Saudi Arabia ikiichapa Argentina na Japan ikishinda dhidi ya Ujerumani.

Miongoni mwa maonyesho hayo makubwa ya timu, kulikuwa na viwango vya binafsi ambavyo vilijitokeza, wachezaji walipojitokeza na kuwa mashujaa wa taifa.

Vile vile, tumeona chaguzi zingine mpya kabisa viwanjani, wachezaji ambao hawajawahi kuwa na majina makubwa kule wanakocheza kuanzia kwenye ligi zao.

Lakini ghafla wameibuka na kuwa nyota kwenye mashindano haya makubwa zaidi ya soka kwa ngazi ya taifa duniani.

Hapa tunawaangalia nyota watano walioshangaza kwenye Kombe la Dunia hadi sasa...

**# Shuichi Gonda (Japan)**

Hakuna kipa aliyeokoa hatari nyingi zaidi katika raundi ya kwanza ya mechi za Kombe la Dunia kama, Shuichi Gonda wa Japan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, aliokoa hatari nane dhidi ya Ujerumani, huku washindi hao wa Kombe la Dunia mwaka 2014 wakijaribu kila namna kumfunga, lakini wakashindwa na kujikuta wakishindwa kabisa kuepuka kichapo cha mabao 2-1.

Hatari nne kati ya hizo alizoziokoa zilikuja katika kipindi cha sekunde 20, ambacho kilijumuisha kuokoa mara mbili kwa haraka na kumnyima mara mbili Serge Gnabry wa Bayern Munich kufunga.

Akiwa na mechi 432 katika ngazi ya klabu, kipa huyo wa Shimizu S-Pulse ana uzoefu wa kutosha kwenye lango.

**# Lucas Paqueta (Brazil)**

Lucas Paqueta sasa ameichezea nchi yake mechi 36, hivyo haikushangaza kumuona akipangwa kwenye mechi ya ufunguzi ya Brazil dhidi ya Serbia.

Hata hivyo, iliwashangaza wengi kuona mchezaji anayejulikana kama mshambuliaji akiwekwa pamoja na Casemiro kwenye safu ya kiungo ya Brazil.

Mchezaji huyo nyota wa West Ham alipendekezwa zaidi ya Fred na Bruno Guimaraes, ambao wote walikuwa chaguo la asili zaidi katika nafasi hiyo.

Mabeki wa pembeni wa Brazil waliwekwa maeneo ambayo waliweza kuwalinda wachezaji hawa wawili wa kiungo na walioonekana kuwa bora zaidi. Paqueta aliweza kumiliki vizuri dimba la kati na anaweza kuwa mtu muhimu katika timu ya kocha, Tite katika mechi zijazo.

**# Michy Batshuayi (Ubelgiji)**

Baada ya kutumika kama mchezaji chipukizi kwa muda mrefu, hatimaye umeweza kuwa wakati muafaka kwa Michy Batshuayi kuwa nyota muhimu kwa kikosi cha Ubelgiji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alianza mbele ya Romelu Lukaku katika ushindi wa bao 1-0 wa Ubelgiji dhidi ya Canada na kufunga bao muhimu kwa kumalizia pasi ndefu ya Toby Alderweireld.

Pamoja na kwamba Lukaku ni muhimu kwa Ubelgiji, fowadi huyo wa Inter Milan amecheza mechi tano pekee katika ngazi ya klabu msimu huu, wakati Batshuayi amekuwa akianza na ni mfungaji wa mara kwa mara wa klabu yake mpya ya Fenerbahce.

Ni rahisi kusahau jinsi mshambuliaji huyo mwenye urefu wa futi sita alivyokuwa mwenye sifa ya juu alipowasili Chelsea kutoka Marseille mwaka 2016 na bado angeweza kutimiza ahadi yake kwenye hatua kubwa zaidi kwa kuchelewa.

**# Takuma Asano (Japan)**

Ujerumani inaweza kusamehewa kwa kutokuwekea maanani sana wakati Takuma Asano wa Japan alipoiingia kama mbadala wa kipindi cha pili dhidi yao Jumatano iliyopita.

Akiwa amesajiliwa na Arsenal mwaka 2016 na kunyimwa kibali cha kufanya kazi, Asano alikuwa kwa muda wa mkopo katika Klabu za Stuttgart na Hannover, ambako alijitahidi kujiimarisha.

Kurudi kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mwaka 2021 akiwa na Bochum kumemfanya mshambuliaji huyo wa Japan kufunga mara nne katika mechi 38.

Hata hivyo, Asano ndiye aliyepeleka kilio cha kukumbukwa kwa Ujerumani, kwa bao la kushangaza la dakika ya 83 ambapo alionyesha udhibiti kamili, nguvu, kasi na utulivu.

**# Salem Al Dawsari (Saudi Arabia)**

Salem Al Dawsari aliifungia Saudi Arabia bao la ushindi dhidi ya Argentina kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi.

Ushindi wa 2-1 wa Saudi Arabia dhidi ya Argentina katika Kundi C umetajwa kuwa mshtuko mkubwa zaidi katika historia ya Kombe la Dunia.

Alikuwa ni winga wa Saudi Arabia, Al Dawsari aliyefunga bao la pili ambalo tayari limekuwa maarufu, alipoudhibiti mpira uliopinda na kuwatoka mabeki kadhaa, kabla ya kumfunga golikipa, Emiliano Martinez.

Hiyo ilikuwa furaha kubwa zaidi ya ushindi huo ambao Serikali ya Saudi Arabia ilitangaza kuwa siku moja baada ya mechi ya Argentina kuwa sikukuu ya kitaifa na mapumziko.

Sasa ni juu ya Al Dawsari mwenye umri wa miaka 31, na wachezaji wenzake kurejesha utulivu wao ili kujihakikishia nafasi katika hatua ya mtoano, ambayo ilionekana kutowezekana kabla ya mashindano haya.



## Nukuu

"Ilitubidi kushinda leo [juzi] na tungeweza kufanya hivyo. Tulijua ulikuwa mchezo muhimu, kama hatukushinda tulikuwa nje. Kuna fainali nyingine inakuja Jumatano [dhidi ya Poland] na tunapaswa kuendelea kupigana wote kwa pamoja... Twende Argentina!!!" **Mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, baada ya kufunga wakati wakiichapa Mexico 2-0 kwenye mechi ya Kombe la Dunia.**



"Ninafahamu kuwa hili linaweza kuwa Kombe langu la mwisho la Dunia. Tayari wakati wa wimbo, nikiimba wimbo wa taifa, nilihisi hisia ndani yangu. Nilitaka si tu kukumbukwa kwa kuwa kwenye Kombe la Dunia, lakini kwa kufunga mabao huko pia. Siku zote nilipigania sana bao kwenye Kombe la Dunia na leo [juzi], nilifanikiwa," **Mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski baada ya kufunga wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Saudi Arabia.**



"Kuna maamuzi magumu yatafanyika ndani ya timu ikiwamo kwa baadhi ya wachezaji huenda tukaachana nao kwenye dirisha hili dogo la usajili na tunafanya yote kwa malengo ya kufanya vizuri kwenye mashindano yote kama malengo yetu yalivyo," **Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez**



Soka Bongo

# MAKIPA WA5 WAKALI WA 'CLEAN SHEETS' LIGI KUU

Na Adam Fungamwango

WAKATI mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara unakaribia kukamilika, baadhi ya makipa wameonyesha uwezo mkubwa wa kukaa langoni bila kuruhusu mabao kwenye baadhi ya mechi.

Mara nyingi makipa kwenye uwezo wa kukaa langoni bila kuruhusu mabao mara kwa mara wana mchango mkubwa wa kuzifanya timu zao kupata ushindi hata wa bao 1-0.

Makipa wenye uwezo wa kutoka na 'clean sheets' mara kwa mara wanawafanya hata mastraika kuchangamka na kusaka angalau bao moja, wakiamini linaweza kuwaweka salama na kumaliza mchezo, tofauti na wale ambao huruhusu mabao karibuni kila mechi hata kama timu yake inashinda.

Mpaka sasa wakati huu Ligi Kuu imefika hadi raundi ya 14, baadhi ya makipa ambao wanashindana kwa 'clean sheets', ni wakigeni na wazawa wakichuana vikali kwenye eneo hilo. Katika makala haya tunakuletea makipa wenye 'clean sheets' nyingi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu na klabu wanazodakia...

**Aishi Manula - Simba (clean sheets 8)**

Kama atakuwa amekaa langoni jana kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania na kutoruhusu bao atakuwa ametimiza 'clean sheets' tisa. Lakini hata kama hatosimama langoni, au akisimama akafungwa bao, bado ataendelea kuwa kinara wa kukaa langoni kwenye mechi nyingi bila kuruhusu bao.

Aishi Manula ambaye pia ni kipa wa timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, amekaa langoni mechi 12 kabla ya mechi ya jana, huku mechi moja tu dhidi ya Singida Big Stars ambayo hakuwepo langoni, badala yake alisimama Beno Kakolanya na pambano kumalizika kwa bao 1-1.

Maana yake ni kwamba ameruhusu mabao kwenye mechi nne tu. Kinara huyo akiwa amesimama langoni katika mechi ambazo Simba ilicheza dhidi ya Geita Gold na kushinda 3-0, dhidi ya Kagera Sugar ikishinda 2-0, dhidi ya Prisons ikishinda 1-0.

Mechi zingine ni ambazo timu yake ikishinda 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji, 5-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, 1-0 dhidi ya Ihefu, 1-0 dhidi ya Namungo na 4-0 ikiichapa Ruvu Shooting.

**Ali Ahmada - Azam FC (clean sheets 6)**

Ni golikipa raia wa Comoro ambaye amesajiliwa msimu huu na Azam FC. Ni moja wa makipa bora kwa sasa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania akikamata nafasi ya pili mpaka sasa akiwa amekaa langoni mara sita bila kuruhusu wavu wake kuguswa.

Uwezo wake huo umesababisha Azam FC kushinda mechi hizo kvuna pointi tatu, kwani zote sita ambazo hakuruhusu bao, timu yake imeshinda bao 1-0 tu.



Manula

Azam FC ilipata ushindi huo wa bao 1-0 ambao ndio umempa 'clean sheets', dhidi ya Mbeya City, Shingida Big Stars, Simba, Ihefu, Ruvu Shooting na Namungo.

**Djigui Diarra - Yanga (clean sheets 5)**

Ushindi wa mabao 2-0 iliyoupata Yanga juzi dhidi ya Mbeya City, umemfanya kipa huyu raia wa Mali kufikisha 'clean sheets' tano mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Amekaa langoni mechi 10, hivyo kuruhusu mipira kupita kwenye lango lake mara tano pia. Hajacheza mechi mbili kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ambazo alimpisha Aboutwalib Mshery dhidi ya Coastal Union na Dodoma Jiji.

Diarra ambaye ni raia wa Mali, mechi ambazo amekaa langoni na kutoruhusu mabao ni dhidi ya Mtibwa Sugar, Yanga ikishinda 3-0, KMC 1-0, Geita Gold 1-0, Kagera Sugar, 1-0 na Mbeya City mabao 2-0.

**Mahmoud Mroivili - Coastal (clean sheets 5)**

Kipa mwingine raia wa Comoro, Mahmoud Mroivili, kama mwenzake Al Ahmada wa Azam, naye yumo kwenye orodha ya wanaochuana kucheza mechi nyingi za ligi bila kuruhusu bao. Kama Diarra, ana 'clean sheets' tano mpaka sasa.

Ni kipa wa Coastal Union ambaye wamemsajili msimu huu na amekuwa msaada mkubwa kwenye timu hiyo.

'Clean sheets' zake amezipata kwenye mechi ambazo timu yake ilicheza dhidi ya KMC na kushinda 1-0, Namungo 1-0, Kagera Sugar 2-0, Geita Gold ikasuluhu, na ikaifunga Prisons 2-0.

**Metacha Mnata - Singida Big Stars (clean sheets 5)**

Kipa Mtanzania na aliwahi kuichezea Timu ya Taifa, Taifa Stars, Metacha Mnata pia ana 'clean sheets' tano.

Amezitengeneza kwenye mechi ambazo timu yake ya Singida Big Stars ilishinda 1-0 dhidi ya timu za Prisons, Ihefu, Polisi Tanzania na KMC, huku mechi moja dhidi ya Dodoma Jiji ikimalizika kwa suluhu.

**NDANI YA 18**



KIPIGO cha mabao 2-1 ilichokitoa Saudi Arabia kwa Argentina wiki iliyopita nchini Qatar, kinaifanya kuwa timu ya kwanza ambayo haitoki barani Ulaya kuwafunga Waargentina hao kwenye Kombe la Dunia tangu Cameroon ilipofanya hivyo mwaka 1990. Saudi Arabia ipo chini ya Kocha Mfaransa Herve Renard.

## FUNDI WA WIKI...



# MESSI

| | |
|---|---|
| **JINA KAMILI:** | Lionel Andrés Messi |
| **KUZALIWA:** | Juni 24, 1987 (miaka 35) |
| **ALIPOZALIWA:** | Rosario, Santa Fe, Argentina |
| **KIMO:** | 1.70 m (5 ft 7 in) |
| **NAFASI:** | Mshambuliaji |
| **KLABU:** | Paris Saint-Germain |
| **JEZI NAMBA:** | 30 |
| **TAIFA- NAMBA:** | 10 |

### REKODI KOMBE LA DUNIA

* Messi ameifikia rekodi ya Diego Maradona ya kuifungia Argentina mabao nane kwenye Kombe la Dunia yaliyotokana na mechi 21.
* Amefikisha idadi hiyo wakishinda 2-0 dhidi ya Mexico juzi. Hivyo sasa wanakuwa nyuma kwa mabao mawili dhidi ya Gabriel Batistuta anayeongoza kwa kuifungia Argentina.
* Pia amemfikia Cristiano Ronaldo wa Ureno ambaye naye ana mabao nane Kombe la Dunia hadi sasa.

# WACHEZAJI MAKINDA ZAIDI KOMBE LA DUNIA QATAR

**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la FIFA la 2022, linaendelea na msisimuko mkubwa zaidi nchini Qatar. Wachezaji wengi bora zaidi duniani wapo kwenye mashindano hayo na kuna wigo mzima wa hisia zinazohusishwa na tukio hilo.

Michuano hiyo itakuwa chungu kwa baadhi ya magwiji wa mchezo huo ambao wanaweza kucheza kwenye hatua kubwa zaidi ya soka kwa mara ya mwisho katika maisha yao ya soka.

Huenda hili likawa Kombe la Dunia la mwisho kwa wachezaji bora wa wakati wote, Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.

Hii pia itakuwa mara ya kwanza kwa wachezaji kadhaa kuingia kwenye hatua kubwa. Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji watano wachanga zaidi kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

**#5. Bilal El Khannouss (Morocco) - Alizaliwa Mei 10, 2004 (Ana miaka 18)**

Morocco ipo na Bilal El Khannouss mwenye umri wa miaka 18, katika kikosi chao cha Kombe la Dunia la FIFA 2022. Alikuwa gumzo la jiji la Ubelgiji kwa hisani ya uchezaji wake bora katika Klabu ya Racing Genk. El Khanouss alikuwa na chaguo la kuiwakilisha Ubelgiji juu ya Morocco, lakini aliamua kwenda na timu yake ya asili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, amekuwa Genk tangu akiwa na miaka 14 na ameiwakilisha Ubelgiji katika timu za taifa za vijana chini ya umri wa miaka 15 na U-16. Katika mechi 16 kwenye mashindano yote ya Racing Genk msimu wa 2022-23 hadi sasa, kiungo huyo mkabaji ametoa asisti moja.

**#4. Jewison Bennette (Costa Rica) - Alizaliwa Juni 15, 2004 (Ana miaka 18)**

Costa Rica ina wachezaji wachache wenye vipaji katika kikosi chao na Jewison Bennette ndiye mkuu kati yao. Winga huyo mwenye umri wa miaka 18, alicheza jukumu muhimu katika kusaidia Costa Rica kunyakua pointi 19 kati ya 21 zilizowawezesha kutoka katika mechi saba zilizopita za kufuzu Kombe la Dunia.

Bennette kwa sasa anaichezea Klabu ya Sunderland. Amefunga mabao matatu na kutoa asisti moja katika mechi 16 kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu.

Katika mechi saba kwenye michuano yote aliyoichezea Costa Rica hadi sasa katika maisha yake ya soka, kijana huyo amefunga mabao mawili na kutoa asisti mbili.

**#3 Gavi (Hispania) - Alizaliwa 5 Agosti 2004 (Ana miaka 18)**

Mshambulizi huyo wa Hispania tayari amejitambulisha kama mchezaji muhimu kwa Barcelona na timu ya taifa. Uwezo mkubwa wa kiungo huyo wa kati na akili ya mchezo inakanusha umri wake na amekuwa mchezaji muhimu kwa Hispania kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 amecheza mechi 19 katika mashindano yote akiwa na Barcelona hadi sasa msimu huu na ametoa asisti moja. Tayari ameshaichezea Timu ya Taifa ya Hispania mara 13.

**#2. Garang Kuol (Australia) - Alizaliwa Septemba 15, 2004 (Ana miaka 18)**

Australia wapo na kikosi chao cha wachezaji 26 na Garang Kuol, mwenye umri wa miaka 18, ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kwenye orodha yao. Inafurahisha, Kuol bado hajaanza mechi ya ligi katika maisha yake ya soka ya wakubwa na ni bidhaa isiyojulikana kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Kuol atajiunga na Newcastle United inayoshiriki Ligi Kuu England Januari 2022 na amefurahishwa na uchezaji wake akiwa nje ya benchi kwa timu yake ya sasa ya Central Coast Mariners. Amecheza jumla ya mechi 12 za ligi nje ya benchi na kupokea mwito wake wa kwanza kwenye kikosi cha kimataifa cha Australia mnamo Septemba.

Alipata mechi yake ya kwanza katika mechi ya kirafiki dhidi ya New Zealand (Septemba).

**#1. Youssoufa Moukoko (Ujerumani) - Alizaliwa 20 Novemba 2004 (Ana miaka 17)**

Youssoufa Moukoko ana msimu mpya na tayari ameshapata ofa kutoka kwa klabu kadha za Ulaya. Kinda huyo amekuwa katika hali ya kustaajabisha msimu huu na amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa Borussia Dortmund hadi sasa msimu huu.

Amefunga mabao sita na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 22 kwenye michuano yote akiwa na Dortmund hadi sasa. Ukweli ni kwamba ameanza mechi 11 pekee kati ya hizo na kufanya idadi yake kuwa ya kuvutia zaidi.



## JE, WAJUA?

UFARANSA na Australia zilikutana katika mechi yao ya ufunguzi ya Kundi C kwenye Fainali za Kombe la Dunia mwaka 2018 na Wafaransa kushinda kwa tabu mabao 2-1 baada ya beki wa kushoto, Aziz Behich kujifunga dakika za mwisho, ambapo Ufaransa ilimaliza michuano hiyo kwa kuwa mabingwa. Na fainali hizi nchini Qatar zimepangwa pamoja Kundi D na mechi yao ya ufunguzi Ufaransa ikashinda 4-1. Je, historia itajirudia tena?





## Wanaoharibu misitu kuanza kuchukuliwa hatua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya, imetangaza kuanza kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaoharibu misitu iliyohifadhiwa pamoja na vyanzo vya maji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alitangaza kuanza kuchukua hatua hizo alipofanya ziara ya kukagua uharibifu wa mazingira kwenye misitu inayozunguka Hifadhi ya Safu za Mlima Mbeya.

Alisema kuna baadhi ya watu wanaingia kinyemela kwenye misitu iliyohifadhiwa na kuanza kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa pamoja na kufanya shughuli za kilimo.

Alisema yeyote atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali za kisheria huku akiwataka wananchi wa maeneo hayo kuwa walinzi wa misitu kwa kutoa taarifa kuhusu waharibifu wanaovamia.

"Tutakagua misitu yote iliyohifadhiwa ndani ya wilaya hii ili kubaini hali ya uharibifu na kuanza kuchukua hatua, lakini kuna wale wanaharibu vyanzo vya maji kwa kufanya shughuli zao kwenye maeneo hayo, tutachukua hatua," alisema Dk. Chuachua.

Aliwataka viongozi wa serikali za vijiji kushirikiana na maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kulinda misitu kwa kuhakikisha wanawachukulia hatua wahalifu wote.

Alisema wananchi wanatakiwa kuingia kwenye misitu hiyo baada ya kupata vibali maalumu vinavyotolewa na TFS na kwamba wanaoingia bila utaratibu huo ni majangili kama walivyo majangili wa wanyama.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa maeneo nchini ambayo kwa sasa yanakabiliwa na uharibifu wa mazingira hali iliyosababisha hata vyanzo vya maji kuanza kupungua.

# Mchimba madini atuhumiwa kumuua mkusanya ushuru kwa deni la 7,500

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WILLIAM Mgaya (58) aliyekuwa wakala wa kukusanya ushuru wa maegesho jijini hapo, ameuawa kwa madai ya kupigwa risasi kifuani na mchimba madini, Ezekia Rwesya (31) wakati akimshinikiza kulipa deni la Sh. 7,500 alilokuwa anadaiwa.

Tukio hilo lilitokea juzi asubuhi katika eneo la Mwanjelwa jijini hapo, wakati mawakala hao walipokuwa kwenye operesheni ya kukagua magari yanayodaiwa madeni ya maegesho.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na mtuhumiwa anashikiliwa na jeshi hilo.

Alisema marehemu pamoja na mwenzake Almas Shaban walilikamata gari la mtuhumiwa lenye namba za usajili T.772 DVY aina ya Toyota Hilux na walipolikagua walibaini kuwa lilikuwa linadaiwa Sh. 7,500.

Alisema walipomwelekeza mtuhumiwa kuhusu deni hilo alitaka kujua usahihi wa taarifa za deni hilo na ndipo mawakala hao wakaamua kwenda naye kwenye ofisi za Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili kuhakiki kwenye mfumo kama alivyotaka mtuhumiwa.

Alisema baada ya kuangalia kwenye mfumo, mtuhumiwa aliridhika na kukubali kulipa deni hilo na kutaka kuondoka, lakini mawakala hao walimzuia wakitaka alipe papo hapo kwa maelezo kuwa deni hilo lilikuwa limekaa muda mrefu.

"Hali hiyo ilizua majibizano baina ya marehemu na mtuhumiwa na kusababisha mtuhumiwa kuchukua pisto yake na kufyatua risasi moja kuelekea upande alikokuwa marehemu," alisema Kamanda Kuzaga na kuongeza.

"Risasi hiyo ilimpata marehemu eneo la kifuani upande wa kulia na kusababisha kifo chake muda mfupi baada ya kufikishwa katika hospitali ya rufani ya mkoa wa Mbeya," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema kwa sasa jeshi hilo linaendelea kumhoji mtuhumiwa na baada ya kukamilisha mahojiano watamfikisha mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria. Kamanda Kuzaga aliwataka wamiliki wote wa silaha ndani ya mkoa huo kuzitumia kwa mujibu wa masharti ya umilikishwaji waliyopewa.

Almas Shaaban (32) ambaye alishirikiana na marehemu kukagua gari la mtuhumiwa alisema risasi iliyomuua mwenzake ilikuwa imelengwa kumuua yeye, lakini aliokolewa na kiatu ambacho aliinama kwa ajili ya kukiva avizuri kabla ya kufyatuliwa.

Alisema baada ya mtuhumiwa kumpiga Mgaya, alifanikiwa kumvamia na kumwangusha chini kabla ya wananchi wengine hawajatokea kwa ajili ya kusaidiana naye kumdhibiti.

Alisema walifanikiwa kumnyang'anya silaha yake na baadhi ya wananchi walianza kumsaidia marehemu kumkimbiza hospitalini kabla ya kufariki.

Alisema tukio hilo lilizua taharuki kwa sababu lilikuwa halijatarajiwa.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe,Waziri Kindamba (wa sita kushoto), akishirikiana na watendaji wa Wizara ya Fedha, TRA na Trade Mark kukata utepe kuashiria uzinduzi wa mashine ya mdaki ya ukaguzi wa shehena za mizigo katika mpaka wa Tunduma mkoani Songwe mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpaka Tanzania, Zambia wasimikwa vifaa vya kisasa

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

TATIZO la msongamano wa malori katika mpaka wa Tanzania na Zambia katika mji wa Tunduma mkoani Songwe uliokuwa unasababishwa na teknolojia duni za ukaguzi na uondoshaji wa shehena, umepata suluhu baada ya kusimikwa vifaa vya kisasa.

Umesimikwa mdaki wa kisasa (X-Ray) unaokagua shehena za mizigo kwenye malori kwa kutumia mionzi badala ya mbinu ya awali ambayo maofisa wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) walikuwa wanalazimika kufungua kila lori na kukagua mizigo iliyobebwa.

Pia midaki mingine miwili ya kidigitali ya kukagua watu wanaopita kwenye mpaka huo kuingia nchini pamoja na mizigo wanayobeba ili kuepuka uingizaji wa vitu visivyoruhusiwa.

Mradi huo umetekelezwa kwa ufadhili wa Jumuiya mbalimbali za maendeleo za kimataifa, Balozi za Ireland na Norway kupitia Taasisi ya Trade Mark East Afrika (TMEA) na umegharimu Dola za Kimarekani milioni 2.692.

Mkurugenzi Mkazi wa TMEA, Monica Hangi, alisema mdaki huo una uwezo wa kukagua malori kati ya 100 na 150 kwa saa tofauti na awali maofisa wa TRA walikuwa wanatumia saa moja kukagua lori moja.

Alisema matumizi ya mdaki huo yamesaidia kupunguza muda wa malori kusubiri ukaguzi katika mpaka huo kwa zaidi ya asilimia 70 na kwa sasa lori moja linakaguliwa ndani ya dakika mbili na kubaini kilichoko ndani.

Alisema lengo la kuweka mdaki huo ni kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara kati ya Tanzania na nchi za Ukanda wa SADC kwa kuharakisha ukaguzi na uondoshaji wa mizigo inayoingizwa Tanzania na inayotoka nje ya Tanzania. "Tumetekeleza mradi huu tangu mwaka 2019 kwa kuanza na ujenzi wa majengo ya Kituo cha Pamoja cha Forodha (One Stop Border Post) ambayo tayari yalishaanza kazi na sasa tumeleta mdaki huu kwa lengo lile lile la kuboresha mazingira," alisema Monica na kuongeza.

"Mradi huu kwa pamoja umegharimu Dola za Marekani milioni tisa (Sh. bilioni 20), tunaamini mdaki huu utaongeza idadi ya shehena zitakazokuwa zinapita hapa," aliongeza.

Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alisema mdaki huo ni wa kisasa na utasaidia kuondoa msongamano wa malori kwenye mpaka huo ambao ulikuwa ukitokea mara kwa mara kutokana na mbinu zilizokuwa zinatumika.

Alisema mdaki unatumia mionzi na kutoa picha ya kila kilichomo ndani ya lori ili maofisa wa TRA waweze kutambua mzigo uliomo ndani na kwamba tayari maofisa hao wamepatiwa mafunzo na wafadhili hao kuhusu matumizi na namna ya kuutengeneza ukileta hitilafu.

Alisema watahakikisha wanaitunza na kuitumia vizuri midaki hiyo ili ilete manufaa ndani ya miaka 10 ambayo watengenezaji wamewaelekeza itafanya kazi.

Akizindua mdaki huo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Kindamba, alisema wamekuwa wakipata shida ya kusuluhisha migogoro ya mara kwa mara na madereva wa malori ambao wamekuwa wakileta migomo kutokana na kukaa muda mrefu. Alisema kitendo cha muda wa ukaguzi na uondoshaji wa shehena kupungua kitasaidia hata bei ya bidhaa kupungua na kusaidia serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Vilevile, alisema mdaki huo utasaidia kupunguza udanganyifu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wasafirishaji kuingiza nchini bidhaa haramu kwa kuzihifadhi ndani ya malori ya mizigo.

Baadhi ya madereva walisema kwa sasa wana uhakika wa kupunguza matumizi kwa maelezo kuwa kitendo cha kukaa muda mrefu kwenye mji huo wa Tunduma kilikuwa kinawaongezea gharama za maisha.





# Polisi yaweka mikakati kutokomeza ukatili kijinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma limeweka mikakati mbalimbali ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ikiwamo matukio ya ulawiti kwa watoto wa shule za msingi ambayo yameshika kasi siku za karibuni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya ushiriki wa jeshi hilo katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili zinazoanza Novemba 25 hadi Desemba 10 kila mwaka.

Alisema, duniani kote jana yameanza maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na jeshi hilo limejipanga kushiriki kwa kufanya shughuli mbalimbali katika jamii.

"Leo (jana) nchi zote duniani zimeanza maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsi hivyo sisi kama Jeshi la Polisi tumejipanga kuendesha shughuli mbalimbali ambazo tutazifanya katika siku hizo zote," alisema.

Kamanda Otieno, alisema jeshi hilo Mkoa wa Dodoma pia wamepanga kutoa elimu kwa jamii kuelimisha kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Tunapanga kuwa na utaratibu wa kutoa elimu ili kuhamasisha jamii kuachana na vitendo vya ukatili, tutakwenda katika maeneo ya nyumba za ibada, shule, sokoni, nyumba kwa nyumba na hata katika vyombo vya usafiri kutoa elimu kwa kushirikiana na dawati la jinsia mkoa," alisisitiza.

Alisema moja kati ya matukio ya ukatili ambayo yanaripotiwa mara nyingi katika Mkoa wa Dodoma ni ubakaji na kwamba anatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia pamoja na matukio mengine ya kihalifu.

Vile vile, alisema lengo la jeshi hilo mkoani humo ni kutumia siku hizo 16 kutoa elimu kuiwezesha jamii kutambua madhara ya vitendo vya ukatili na kuchukua hatua ya kukabiliana navyo.

"Lengo lingine ni kuhakikisha kuwa jamii inakuwa na uelewa ili kukemea ukatili katika jamii inayotuzunguka," alisema.

Kadhalika, alisema katika siku hizo 16 watashiriki maadhimisho ya siku ya wenye ulemavu ambayo kimkoa yamepagwa kufanyika Desemba 3, mwaka huu, wilayani Mpwapwa.

"Vilevile tumepanga kutembelea nyumba za kutunza watoto pamoja na wale wenye uhitaji na kutoa misaada mbalimbali, kutoa mafunzo kwa askari wetu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Mmoja wa wakazi wa Jiji la Dodoma, Michael Mwafute, alisema ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini kila mtu anapaswa kuwa na hofu ya Mungu.

"Hivi sasa matukio ya ukatili wa kijinsia yamekithiri sana kila unaposikiliza vyombo vya habari unasikia mtu kamuua mke wake au kiongozi wa dini kamlawiti mtoto hii yote ni kukosa hofu ya Mungu," alisema Mwafute.



Mkurugenzi wa Idara ya Mipango na Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi katika Wizara ya Kilimo, Juma Mdeke (katikati), akiwa ameshikana mikono na Rais wa Bodi ya Vi Agroforestry, Charllota Szczepanowski kutoka Sweden, wakati wa upandaji miti kwenye maonesho ya 7 ya kilimo cha mseto. **PICHA: VALENTINE OFORO**

# Wanafunzi waonywa tabia ya kuwatega wahadhiri vyuoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewaagiza wanafunzi kuacha tabia ya kuwatega wahadhiri na rushwa ya ngono ili wawakamatishe na kupewa adhabu.

Ndejembi aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kongamano la kukuza maadili na mapambano dhidi ya rushwa lililofanyika jana jijini hapo.

Naibu Waziri huyo alisema kumekuwa na tabia ya wanafunzi kuwatega walimu jambo lisilokubalika na kuwataka wahadhiri kujiridhisha pale wanapoletewa tuhuma za mhadhiri mwenzao kabla ya hatua kali kuchukuliwa.

"Ninaomba walimu mjiridhishe kabla ya kutoa adhabu kwa sababu kuna wahadhiri wengine wametegwa na wanafunzi," alisema Ndejembi.

Alisema lengo lao ni kuona rushwa haikubaliki kwa sababu inachangia kupata viongozi wasio na maadili hapo baadaye.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuhakikisha makongamano hayo yanafanyika kila mkoa ili kila mmoja asaidie kupiga vita rushwa ambayo ni adui wa haki.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, aliwapongeza wanafunzi kwa kujitokeza kwa wingi katika kongamano hilo ambalo ni muhimu kwao.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TAKUKURU, Joseph Mwaisela, alisema jukumu la kupiga vita rushwa ni la wote na wanapaswa kushirikiana ili kuitokomeza.

# Mradi watambuliwa kuboresha afua maambukizi VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MRADI wa Kizazi Hodari umetambuliwa mkoani hapo unaolenga kuboresha afua za maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kufikia malengo ya dunia ya kupambana na VVU.

Mradi huo unaotekelezwa na Taasisi ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa kushirikiana na Shirika la Action for Community Care (ACC) katika Halmashauri nne za Mkoa wa Dodoma kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

Akizungumza jana katika hafla ya kutambulisha mradi huo, Meneja wa Kanda ya Kati wa mradi wa USAID Kizazi Hodari kutoka KKKT, Issa Murshid, alisema utafikia walengwa 10,074 wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Wilaya za Chamwino, Kongwa na Mpwapwa na utatekelezwa kwa miaka mitano.

"Yaani mlengwa awe na vinasaba vya VVU na Ukimwi ambaye aidha wazazi wake wamefariki kutokana na ugonjwa huo au mzazi mmoja aliyebaki anaishi na maambukizi au mzazi au mlezi ana tabia hatarishi zinazoweza sababisha kupata VVU na Ukimwi kama wale wanaoojiuza."

"Tunalenga kufikia malengo ya dunia ya UNAIDS ya 95-95-95, mradi unalenga kuimarisha afya, ustawi na ulinzi kwa watoto waishio katika mazingira magumu na vijana balehe katika jamii zenye kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU," alisema.

Alisema pia unalenga kuibua na kupambana na matukio yote ya ukatili wa kijinsia kwa watoto ili kupunguza hali hiyo kwa jamii na watashirikiana na majukwaa ya asasi za kidini kufanikisha.

Meneja Mradi kutoka Shirika la ACC, Merina Mgongo, alisema Shirika linatekeleza mradi huo kwa Kanda ya Kaskazini Mashariki na walengwa wengine ni wanawake wenye VVU ambao wananyonyesha watoto chini ya miaka miwili na vijana balehe waliopata mimba za utotoni.

"Tunashirikiana na serikali kupitia mipango yote inayoratibiwa na serikali ili kuhakikisha wanapata huduma stahiki kama ilivyoelekezwa kwenye kufanya mashauri ya watoto, tunashirikiana hadi ngazi ya kata ambapo walengwa wetu tunawapata, mradi huu upo hadi mwaka 2027," alisema.

Akizungumzia kuwaimarisha kiuchumi walengwa hao, Mratibu wa Uimarishaji Kiuchumi wa mradi huo kutoka KKKT Kanda ya Kati, Emmanuel Sule, alisema unalenga kuwaunganisha walezi wa watoto waliopo kwenye mradi kujiunga kwenye vikundi vya kuweka na kukopa.

"Mradi unafanya afua mbalimbali za kuwajengea uwezo na kuwafundisha namna ya kuweka akiba, kukopa na kurejesha ili kuanzisha biashara itakayomwongezea kipato," alisema.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa mkoa huo, Josephine Mwaipopo, alisema wameupokea mradi huo na una manufaa kwa serikali na jamii.

"Mradi unaenda kutatua changamoto za kiafya, pia wenye VVU ambao wakati mwingine hushindwa kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya watawezeshwa nauli ili kufika na watanufaika na mafunzo ya ujasiriamali kwa wazazi wanaoishi na watoto wenye VVU," alisema.





## Serikali yasitisha ujenzi michezo ya baharini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, amesitisha ujenzi wa michezo ya baharini (water sports), unaojengwa na mwekezaji wa Kampuni ya NJ Water Sports eneo la fukwe za bahari Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A' kwa madai ya kukiuka kanuni na Sheria ya Ardhi.

Aliyasema hayo jana baada ya kufanya ziara katika eneo hilo ambalo linadaiwa kuwa na mgogoro wa ardhi baina ya mwekezaji huyo na Kampuni ya Matemwe Bungalos, kesi ya mgogoro huo imeshafikishwa Mahakama ya Ardhi visiwani humo.

"Nimelazimika kusitisha ujenzi unaoendelea ili kuutafutia ufumbuzi mgogoro huo ikiwa ni msimamizi mkuu wa masuala ya ardhi" sitoweza kuacha ujenzi uendelee wakati kesi iko mahakamani alisema waziri huyo.

Alisema Mahakama ya Ardhi Gamba imeshatoa uamuzi wa kusimamisha ujenzi wa mwekezaji NJ Water Spots ambaye anadaiwa kuingia eneo la mwekezaji mwenzake.

Alisema Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi haina nia mbaya ya kumwonea mtu, inachohitaji wananchi wafuate sheria ili kuepusha migogoro ya ardhi inayojitokeza.

Aidha, aliwataka wageni na wenyeji wanaohitaji kuwekeza ujenzi wa aina yoyote kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa ikiwamo kupata kibali cha ujenzi kutoka taasisi ya utoaji wa vibali vya ujenzi (DCU) kabla ya kuanza hatua ya ujenzi huo.

Mkurugenzi Mipango Miji na Vijiji kutoka Kamisheni ya Ardhi, Muchi Juma Ameir, alisema lengo la kuwapo kwa taasisi hiyo ni kuepusha migogoro ya ardhi isiyo na ulazima ambayo inarudisha nyuma jitihada za kuleta maendeleo ya nchi.

"Kibali ambacho kinatolewa na DCU huwa kinaonesha michoro ya ujenzi katika eneo husika na mipaka, hivyo vibali vya wawekezaji hao vitaonesha mpaka wa kila mmoja," alisema Muchi.

# Maryam Mwinyi akemea wanaoficha wadhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais, Maryam Mwinyi, ameitaka jamii kuacha kuwaficha watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji kwa kuwataja hadharani ili wachukuliwe hatua.

Aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya siku 16 za wanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, Kikwajuni mjini hapo.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, matukio ya udhalilishaji yaliyoripotiwa polisi kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu ni 865, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja inaongoza kwa kuwa na matukio 171 ikifuatiwa na Magharibi 'A' kuwa na matukio 153 na Wilaya ya Mjini matukio 148.

Alisema jamii ina wajibu wa kulinda na kusimamia haki za watoto na wanawake ili kuhakikisha kundi hilo lenye mchango mkubwa wa maendeleo linakuwa salama na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema wanawake na watoto ni waathirika wakuu wa vitendo hivyo ambavyo sio vya kibinadamu na vinapaswa kupigwa vita na kukemewa kwa nguvu zote.

Maryam alisema wanawake na watoto duniani wana mchango mkubwa wa maendeleo ya jamii na ni vyema kulindwa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

Alisema siku 16 za kupinga vitendo vya udhalilishaji ni muhimu na inatoa nafasi kutathmini juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na wadau katika kupambana na vitendo hivyo na kupanga mikakati mipya ya kuendeleza mapambano hayo.

"Tunapoadhimisha siku hii leo tukumbuke kwamba dunia yote inatambua na kuthamini suala zima la haki na usalama wa wanawake na watoto hivyo tutahakikisha tunazitumia siku hizi kutafahari kuchambua madhira hayo yanayoandama wanawake na watoto kote duniani," alibainisha.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo ulimwenguni, dunia ilianzisha kampeni iliyotokana na mkutano wa wanaharakati dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia mjini Bogata Colombia na kuweka maazimio ya kupinga vitendo hivyo duniani.

Alisema mkutano huo uliazimia na kuchagua siku 16 za kila mwaka kuanzia Novemba 25 ni siku ya kitaifa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji hadi Desemba 19 ambayo ni siku ya kimataifa ya haki za binadamu kwa lengo la kuhusisha masuala ya ukatili na masuala ya haki za binadamu duniani.

Alisema jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika katika jamii ili kuhakikisha vitendo hivyo haviendelei kutokea na pale inapotokea hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya mhusika na mwathirika hupatiwa huduma za kiustawi kumfanya asiendelee kuathirika kisaikolojia.

Balozi wa Umoja wa Mataifa, Manfredo Fanti na Lucy Tesha, kutoka Shirika la Kimataifa la Kusaidia Wanawake (UN Women), walisema lazima kuwa na uongozi wa pamoja katika kupinga vitendo hivyo na mataifa hayo yanachukua njia mbalimbali ya kutokomeza vitendo hivyo ikiwamo kutoa elimu.




Ofisa Uhusiano Jamii wa Barrick North Mara, Zakayo Makobero, akiongea na wanafunzi katika kampeni ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia inayoendeshwa na mgodi huo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika vijiji 11 vinavyozunguka mgodi huo katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ilioanza wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA, Shijiwaza wazindua mradi kuondoa ombaomba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), upande wa Zanzibar kwa kushirikiana na Shirikisho la Jumuiya za watu wenye ulemavu Zanzibar (Shijiwaza) imezindua mradi wa kuwawezesha watu wenye ulemavu kiuchumi (Kijaluba iSAVE Project) ambao utasaidia kuondoa tatizo la ombaomba kwa watu hao.

Akizindua mradi huo jana visiwani humo, MKUU wa Wilaya ya Kusini Unguja, Yussuf Rajab Mkasaba, amesema mradi huo utasaidia kundi kubwa la watu wenye ulemavu ambalo liliachwa nyuma katika harakati za kujiletea maendeleo.

Mkasaba alisema utekelezaji wa mradi huo ni moja ya jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na taasisi pamoja na wadau wa maendeleo katika kuiunga mkono Serikali ya Zanzibar, kuwaletea maendeleo wananchi wake hasa kwa upande wa watu wenye ulemavu.

"Mradi huu utalijengea uwezo kundi hilo katika kuweka akiba, kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kukuza mitaji yao biashara pamoja na kuwahusisha katika shughuli za ujasiriamali kupitia vikundi vyao vya ushirika ili kuwaongezea kipato, kupunguza utegemezi na kuimarisha ustawi wa maisha yao," alisema.

Aidha, aliwataka masheha wa shehia za mradi huo kuhakikisha wanawafichua walengwa wa mradi huo ili kushiriki katika mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Chakechake Pemba, Abdalla Rashid Ali, alisema watashirikiana pamoja katika kutekeleza mradi huo na uwapo wake utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto za kiuchumi kwa makundi ya watu hao.


Mkurugenzi wa Baraza la Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Ussi Khamis Debe, alisema watahakikisha baraza hilo linalinda na kutetea mradi huo kwa maslahi mapana ya watu hao na taifa kwa ujumla.

Alisema serikali ina malengo ya dhati ya watu hao kuona wanapata haki na fursa mbalimbali zinazojitokeza nchini ili kunufaika nazo.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema TAMWA inasimamia miradi mbalimbali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, watahakikisha mradi huo unakuwa chachu kwa kundi hilo kuinuka kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Mwenyekiti wa SHIJUWAZA, Mwandawa Khamis, alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kichumi ikiwamo kukosa mitaji na kuendelea kuwa maskini, uwapo wa mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwahamasisha kuweka akiba pamoja na kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kujiongezea kipato chao.

Mradi huo wa miaka miwili kwa majaribio unatekelezwa katika wilaya tatu ikiwamo ya Kusini Unguja, Magharibi Unguja na Chakechake Pemba, chini ya ufadhili wa Shirika la watu wenye ulemavu la Norway (Norwegian Association of Disabled-NAD).



# Mahindi tani 10 kuwapoza waathirika wa tope

**Na Neema Sawaka,** KISHAPU

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula nchini (NFRA), Kanda ya Shinyanga imetoa msaada wa tani 10 za mahindi katika kaya 149 zilizoathiriwa na tope maji kutoka bwawa lililokuwa limepasuka la Kampuni ya Diamond Williamson Ltd, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Akikabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki, Mbunge wa Viti Maalum, Lucy Mayenga kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imetoa msaada huo huku kaya 38 zinaishi kwenye kambi na zilipoteza chakula na makazi.

Mayenga alisema tukio hilo lilitokea Novemba 7, 2022 na serikali imeguswa kwa kiasi kikubwa na tatizo hilo huku akiwataka wananchi kuishi salama wakati taratibu za kupata makazi zikiendelea.

Kaimu Meneja wa NFRA Kanda ya Shinyanga, Revocatus Bisama, alisema wametoa tani 10 za mahindi ambazozitagawiwakwawanaoishi kambini, kaya 38 tani tano na waliopanga kaya 111 tani tano.

Meneja uhusiano kutoka kampuni hiyo, Bernad Mihayo, aliishukuru serikali kwa kutoa msaada nakuona jinsi serikali ipo pamoja na wawekezaji katika kuisaidia jamii nakuokoa wananchi kutokana na majanga mbalimbali.

Mihayo alisema mgodi umeridhia kaya hizo kutoka kwenye kambi nakwenda kupanga huku kiwalipia kodi ya nyumba kipindi cha miezi sita wakati wakiwajengea nyumba za kudumu wananchi hao.

"Mgodi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kishapu wameandaa mashamba na kuyalima kwa ajili ya kuja kuwagawia waathirika hao vyakula hivyo kipindi cha mavuno," alisema Mihayo.

Mea Ndole, mwathirika wa tope hilo aliishukuru serikali kwa kutoa msaada huo pamoja na waathirika wenzake na kuahidi kuelekea katika nyumba za kupanga wakisubiri maelekezo mengine.



Mwalimu wa lugha za alama kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA), Carlos Mgulukwenda, akiwaelekeza wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi Kahama na wauguzi herufi P wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuwasiliana na wagonjwa wenye uziwi, yaliyofanyika wilayani Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wauguzi wajengewa uwezo matumizi lugha za alama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JUMLA ya wauguzi 50 wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama na wanachuo wa Chuo cha Uuguzi wilayani humo mkoani Shinyanga, wamepatiwa mafunzo ya lugha za alama kwa lengo la kuwasaidia katika utendaji kazi wao wanapokutana na wagonjwa viziwi na wenye usikivu hafifu.

Mafunzo hayo yametolewa juzi na Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) kwa ufadhili wa kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu Barrick ikiwa ni mwendelezo wa mafunzo kwa kundi hilo na tayari yameshafanyika Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa kwa maofisa tabibu.

Mtendaji Mkuu wa TAMAVITA, Kelvin Nyema alisema, wametoa mafunzo hayo ili kuboresha mawasiliano ya lugha za alama baina ya viziwi, wenye usikivu hafifu, wauguzi na wanachuo wa ngazi ya stashahada ambao wanajiandaa kuingia kwenye mfumo wa ajira baada ya kuhitimu.

Alisema, wauguzi na madaktari katika hospitali na vituo vya afya wamekuwa na tatizo la kutoelewana na kundi hilo kwa kuwa wengi wao wanatoa huduma kinyume na tatizo la mgonjwa hali inayosababisha wagonjwa hao kutokupata huduma sahihi.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya alisema, serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya imeendelea kutatua changamoto zinazoikabili Idara ya Afya hususani kwa wauguzi na madaktari ili kuboresha utendaji kazi wao na makundi hayo yanapata huduma stahiki.

Hata hivyo, aliwasihi watoa huduma kutojihusisha na lugha chafu na kutoa huduma bila kubagua makundi ya watu wenye ulemavu kwa kuwa nao wana haki ya kupata huduma kama yalivyo makundi mengine na watakaobainika kufanya hivyo watawajibishwa kisheria kwa mujibu wa miongozo ya kazi zao.

Muuguzi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Joyce Michael alisema, wanapata wagonjwa wa aina hiyo mara kwa mara na kuwahudumia kwa uzoefu walionao kwa sababu wanaishi nao katika jamii na wakati mwingine kupewa tafsiri na ndugu zao.

Alisema, mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kuzungumza na makundi hayo na kujua wanaumwa magonjwa gani ili kutoa huduma sahihi na kudhibiti magonjwa ambayo yanasababishwa na watoa huduma.

Mmoja wa wanachuo wa Chuo cha Uuguzi Kahama, Mwanaidi Ally, ameiomba serikali kuweka somo la lugha ya alama katika vyuo hivyo ili kuwajengea uwezo wa kuwasiliana vizuri na makundi ya viziwi na wenye usikivu hafifu wakati wanapokuwa kazini.

Alisema, wanapokuwa katika mafunzo ya vitendo hospitalini, wanakutana na tatizo hilo na kushindwa kutoa huduma na kwamba elimu hiyo kama itatolewa katika vyuo vyote vya afya itasaidia kuwajengea uwezo wanachuo namna sahihi ya kuzungumza na kutoa huduma kwa kundi hilo.

## Waombwa udhibiti uharibifu miundombinu ya maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wananchi katika Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuchukua hatua kali kwa watu wanaoharibu miundombinu ya maji kwa kukata mabomba na kuiba vifaa wakiisababishia hasara serikali wakati mwingine wananchi kukosa huduma ya maji.

Baadhi ya wananchi na viongozi wa vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi za jamii (CBWSO), kutoka katika vijiji vya Wilaya ya Misungwi ambavyo serikali kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira imetekeleza miradi ya maji kwa asilimia 100.

Peter Paul, Meneja wa chombo cha watoa huduma za maji ngazi ya jamii katika mradi wa maji vijijini wa Fela-Usagara (FEUWASA), aliiambia Nipashe kuwa licha ya kupatiwa mradi huo kuna watu wachache wanaohujumu miundombinu yake kwa kukata na kutoboa mabomba wengine wakiiba baadhi ya vifaa.

Alisema mradi huo wa Fela-Usagara unazalisha lita 24,000 kwa saa ikiwa kwa siku moja unazalisha lita 230,000 na kuhudumia vijiji vinne huku maji hayo yakiuzwa kwa wananchi kwa wastani wa Sh. 30 kwa ndoo moja ya lita 20.

Haruna Juma, Meneja wa ISENUWASA katika mradi wa Isenengeja-Nunduru alisema licha mradi huo kutoa huduma kwa wananchi zaidi ya 900 wa Kata ya Isenengeja, wanajitahidi kutoa elimu ili watunze miundombinu hiyo ambayo imewapunguzia kufuata maji umbali wa zaidi ya kilometa tano.

Baadhi ya wananchi wanaonufaika na miradi ya maji katika wilaya za Misungwi, Kwimba Magu, Sengerema na Ukerewe, waliiomba serikali kupitia RUWASA kuendelea kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji ili viendelee kuwanufaisha na utekelezaji wa miradi ya maji.

"Hii miradi inatusaidia kupata majisafi na salama tofauti na awali tulikuwa tukitembea umbali wa kilometa tano kufuata maji ziwani ambayo hata hivyo sio safi na salama, hivyo wakidhibiti hujuma hizo ndogondogo hatutokosa majisafi tena," alisema Rucia Jilala, mkazi wa Nunduru. Meneja wa RUWASA wilayani Misungwi alikemea vitendo hivyo na kuwataka wananchi kuwa walinzi wa miradi hiyo kutokana na serikali kutumia fedha nyingi katika utekelezwaji wake.

Alisema katika wilaya hiyo wanahudumia vijiji 101 ikiwa tayari wamekamilisha mitatu yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.8 yenye vituo vya kuchota maji 935 na bado wanayo miradi 17 wanayotekeleza ili kuhakikisha wanamaliza tatizo la maji katika wilaya hiyo.

HABARI KIMATAIFA

# Baba amwalika binti yake kushuhudia akinyongwa

**WASHINGTON,** MAREKANI

BABA aliyetambulika kwa jina la Kevin Johnson (37) amemwalika binti yake Khorry Ramey (19) aliyemwacha akiwa na miaka miwili, kushuhudia akinyongwa huko Marekani, huku hakimu akiweka pingamizi kwamba umri wa binti huyo ni mdogo kushuhudia tukio hilo.

Kevin Johnson anakabiliwa na hukumu ya kunyongwa na kwa mujibu wa Mahakama nchini humo, atanyongwa Jumanne kwa kosa la mauaji ya ofisa wa polisi mwaka 2005, ambaye alikuwa ni baba wa watoto watatu.

Inaelezwa kuwa Johnson aliomba binti yake, Khorry Ramey, ahudhurie na kushuhudia akinyongwa, ombi ambalo hakimu wa mahakama husika alilikataa.

Taasisi ya 'The American Civil Liberties Union' iliyowasilisha hoja ya dharura kwa niaba yake, ilisema kuwa sheria ya serikali ilikiuka haki zake za kikatiba.

Taasisi hiyo ilisema kwamba hitaji la umri katika sheria ya Missouri kumzuia mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 21 kushuhudia kunyongwa hakukuwa na madhumuni ya usalama.

Ilitajwa kwamba Johnson alikuwa gerezani tangu binti yake Ramey alipokuwa na umri wa miaka miwili.

Wawili hao walijenga ukaribu mkubwa kupitia kutembelewa gerezani, simu, barua na barua pepe, huku ikielezwa kuwa binti huyo mwezi uliopita alimpeleka mtoto wake mchanga gerezani kukutana na babu yake.

Ramey alisema katika taarifa yake kuwa baba yake alifanya kazi kwa bidii ili kujirekebisha gerezani, na kwamba alikuwa akiombea dua ili Gavana wa Missouri kumpa msamaha, huku akionyesha kutoridhishwa kutokana na kukataliwa kwa ombi la baba yake.

"Nimeumia sana kwamba sitaweza kuwa na baba yangu katika dakika zake za mwisho," alisema.

**BBC**

## 10 wafariki kwa moto maandamano nchini China

**URUMQI,** CHINA

MAANDAMANO dhidi ya masharti ya Covid nchini China yanaonekana kushamiri kufuatia moto ulioua watu 10 katika jengo la ghorofa huko Urumqi.

Katika jiji la Shanghai, video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii na waandishi wa habari wa kigeni zinaonyesha maelfu ya watu wakiingia barabarani kuwakumbuka walioathiriwa lakini kuandamana dhidi ya vizuizi vya Covid.

Ilielezwa kuwa watu wengi wamelaumu vifo hivyo, wakidai kwamba vimesababishwa na kufungwa kwa majengo hayo ya makazi, huku mamia wakisikika wakimtaka Rais Xi Jinping ajiuzulu.

Mamlaka ya China ilikanusha kuwa wao ndio sababu, ingawa mamlaka ya Urumqi iliomba msamaha usio wa kawaida mwishoni mwa juma lililopita, wakiapa kumwadhibu mtu yeyote ambaye hajatekeleza wajibu wake.

Katika mkusanyiko huo mjini Shanghai, wengine walisikika wakipiga kelele zilizoashiria kumtaka Rais Xi Jinping kung'atuka. **BBC**

**Ilielezwa kuwa watu wengi wamelaumu vifo hivyo, wakidai kwamba vimesababishwa na kufungwa kwa majengo hayo ya makazi, huku mamia wakisikika wakimtaka Rais Xi Jinping ajiuzulu.**



Kutoka kushoto, Mjumbe wa upinzani wa Venezuela, Gerardo Blyde Pérez, Waziri wa Mambo ya Nje wa Mexico, Marcelo Ebrard, mwanadiplomasia wa Norway, Dag Nylander na Spika wa Bunge la Venezuela, Jorge Rodriguez, walipokutana Jumamosi nchini Mexico kwa ajili ya kujadili masuala ya ulinzi wa kijamii, hali iliyofanikisha vikwazo vya Marekani vinavyoielemea sekta ya mafuta ya Caracas kuanza kuondolewa. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Nguema ashinda muhula wa sita Guinea

**MALABO,** GUINEA

KIONGOZI wa Guinea ya Ikweta, Rais Teodoro Obiang Nguema, ametangazwa mshindi wa kiti cha urais kwa muhula wa sita nchini humo, kwa kupata asilimia 94.9 ya kura zote zilizopigwa.

Hayo yalielezwa na maofisa wa Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo mwishoni mwa juma lililopita, ambapo walisema idadi ya wapigakura ilikuwa asilimia 98 ya raia wote walioandikishwa.

Obiang, mwenye umri wa miaka 80, aliingia madarakani kwa njia ya mapinduzi ya jeshi ya mnamo mwaka 1979, huku ikielezwa kuwa kwa sasa ndiye kiongozi aliyekaa madarakani kwa muda mrefu zaidi ukiondoa orodha ya watawala wa kifalme.

Tangu alipochukua hatamu za uongozi hajawahi kushinda uchaguzi kwa chini ya asilimia 93 ya kura.

Mkuu wa tume ya uchaguzi nchini Guinea Faustino Esono, alithibitisha kuwa Obiang ataendelea na wadhifa wa urais kwa muhula mwingine wa miaka saba.

Ushindi huo wa kishindo kwa sehemu kubwa ulitarajiwa kwenye taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa mafuta.

Inadaiwa kuwa kwa ujumla upinzani wa taifa hilo ni dhaifu na Chama cha Obiang cha 'Democratic Party of Equatorial Guinea' (PDGE) kina nguvu kubwa.

Katika uchaguzi wa mwaka huu uliofanyika Jumapili iliyopita, Nguema alikuwa akiungwa mkono na muungano wa vyama vya siasa 15 ikiwamo chama chake cha PDGE.

Chama hicho ambacho ndiyo kilikuwa taasisi halali ya kisiasa nchini Guinea hadi mwaka 1991, kimeshinda pia viti vyote vya Bunge la Taifa na Baraza la Seneti.

Hata hivyo tume ya uchaguzi haikutangaza asilimia ya matokeo waliyopata wagombea wa urais wa upande wa upinzani ambao ni Andres Esono Ondo wa Chama cha 'Convergence for Social Democracy' na Buenaventura Monsuy Asumu wa 'Social Democratic Coalition Party'.

"Kwa mara nyingine matokeo ya mwisho ya uchaguzi yameonyesha kuwa upande wetu" aliandika kupitia ukurasa wa Twitter mtoto wa kiume wa rais Obiang, ambaye ni makamu wa rais wa nchi hiyo Teodoro Nguema.

Ujumbe wake uliongeza kwamba utaendelea kuthibitisha kwamba wao ni chama kikubwa.

Obiang, anadaiwa kuwa mtawala wa mkono wa chuma anayeshutumiwa kwa ufisadi na ukandamizaji wa upinzani.

Obiang aliitawala Guinea ya Ikweta kwa zaidi ya miaka 43 baada ya kumpindua mjomba wake, Francisco Macias Nguema, ambaye baadaye alihukumiwa kuuawa kwa kupigwa risasi.

Pia inadaiwa kuwa tangu alipoingia madarakani amekuwa akikandamiza kila aina ya upinzani na ukosoaji na amefanikiwa kuzuia majaribio kadhaa ya mapinduzi kwenye taifa hilo ambalo ni koloni la zamani la Uhispania.

Kabla ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi vikosi vya usalama viliwakamata wanasiasa kadhaa wa upinzani chini ya kile utawala wa nchi hiyo ulikitaja kuwa kuzima njama za kufanyika mashambulizi kwenye mji mkuu Malabo na katika mji mkubwa wa kibiashara wa Bata.

Serikali pia iliifunga mipaka yake ya ardhini na mataifa jirani ya Gabon na Cameroon kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi, ikisema inazuia wahujumu kutovuruga uchaguzi.

Obiang ni rais wa pili wa Guinea ya Ikweta tangu taifa hilo lilipopata uhuru mwaka 1968 kutoka Uhispania, iliyokuwa mtawala wake wa kikoloni kwa karibu karne mbili. Licha ya utajiri mkubwa wa mafuta, taifa linaongoza linaorodheshwa kuwa miongoni mwa yale maskini zaidi duniani.

Rushwa na ufujaji wa mali ya umma ni masuala yanayotajwa kukita mizizi ndani ya utawala wa miongo minne wa familia ya Nguema. **DW**




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande (kushoto), akikabidhiwa zawadi na Ofisa Biashara Mwandamizi wa Benki ya Maendeleo TIB, John Mboje (kulia), alipotembelea banda la TIB kwenye maonesho ya Wiki ya Huduma ya Fedha Kitaifa yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uchawi umepanda kidijitali!

**Na Marie binti Shaba,**
TAMWA

HIVI karibuni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitayarisha warsha ambayo ilibeba mada ya kupunguza madhara yahusuyo uchawi na kutafuta wachawi.

Wadau kutoka sekta mbalimbali walihudhuria na wengine walitoa mada zenye kutoa fikra na mitazamo mbalimbali. Je uchawi na uganga ni sarafu yenye pande mbili? Kuna tofauti kati ya mchawi na mganga? Je, uchawi ni sayansi au teknolojia?

Hivi sasa uchawi unachukuliwa kwa namna ya pekee katika anga za wasomi duniani; sio tu kwa mtazamo wa kisomi, bali ni katika kuelewa, kujadili kwa dhati ili kupata suluhu endelevu. Uchawi umeingia katika anga za kidijitali kama suala mtambuka, kukemea na kuhubiri hakujatusaidia, inabidi lichukuliwe kwa mbinu mtambuka pia.

TAMWA ni asasi ya kitaalamu na kiharakati iliyojikita katika masuala yenye maslahi kwa wanawake na watoto. Wanatoa ushawishi na utetezi ili haki na usawa kwenye sera na sheria zilete mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa wote. Ajenda ya kwanza ilikuwa kupambana na mifumo katili inayo dhalilisha utu wa wanawake na watoto.

Mnamo 1997, TAMWA pamoja na wadau wake waliandaa warsha ili kuwakilisha, kujadili na kutoa mapendekezo kwa wabunge matokeo ya kazi ya miaka 10 ya mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia. Wakiwa wamelala kwenye mahema katika uwanja wa Chuo cha Biashara Dodoma walitoa ushawishi na utetezi kwa wabunge kabla ya warsha, na baada ya warsha tunda la kwanza lilikua sheria maalumu ya masuala ya kujamiiana (1998). Kama asasi hai bado inafuatilia ajenda hii sugu na kujiuliza; hivi kwa nini baada ya miaka 25, mapendekezo mengi yamekua yakienda mwendopole na kuleta mtanziko katika harakati?

Tofauti kati ya uchawi na uganga ni kama maziwa na tui la nazi. Tanzania sio nchi pekee ambayo iko katika mtanziko kuhusu jambo hili, tofauti ni katika changamano. Mathalani namkumbuka yule mbuzi mweupe wakati Mfalme Charles wa III anatawazwa, je, kitendo kile ni uchawi au ushirikina? Inategemea wewe katika urithi wako wa utamaduni mbuzi mweupe kwenye sherehe anawakilisha nini.

Kimsingi mganga wa asili ana shabihiana sana na mganga wa kisasa kwa vile wanalengo la kutibu, ili atibu inabidi kwanza abaini tatizo ili aweze kuelekeza tiba stahiki. Wote wana tumia njia mbalimbali kutibu maradhi ya kimwili, kiroho au kinafsi. Mantiki hapa ni kwamba hata kama huelewi wanachofanya au wasichofanya mradi wewe unajisikia kupona utamwamini mganga wako. Ndipo Waswahili wakasema uwongo wa mganga nafuu ya mgonjwa.

Mchawi huanza na wazo ovu na uchawi ni njia anayotumia kutekeleza nia yake mbaya. Kwa maana hiyo sie wote ni wachawi watarajiwa kwa mawazo, maneno na matendo. Waswahili wana maana gani wanaposema heri mchawi kuliko muongo. Mchawi sharti umfuate lakini muongo anatumia ulimi wake kama njia ya kumdhuru mtu. Na ulimi ni silaha kubwa ambayo inaweza kuleta machafuko kuliko uchawi.

Waingereza walituachia urithi wa sheria za nchi zilizoandikwa ambazo zilipiga marufuku yale ambayo hawakuyaelewa au hawakuweza kuyadhibiti. Walidhoofisha nadharia na desturi zetu kwa ajili ya maslahi yao ya kiuchumi na kiutawala. Leo hii serikali iko katika mtanziko mkubwa kuhusu uchawi kwa sababu haiwezi kutoa adhabu bila ushahidi unao shikika au kuonekana.

Sheria za kimila ni za kurithi kutoka kizazi hadi kizazi na haziandikwi bali zinahifadhiwa na kuongozwa na maadili katika nyanja zote za maisha, kwa maslahi ya jamii husika na adhabu zilitolewa kimaadili. Imani za kidini zinatambua uchawi katika vitabu vitakatifu. Kwenye dini adhabu zinaahirishwa mpaka siku ya kiama. Wao hutumia zaidi ushawishi na miongozo.

Mtanziko mpana zaidi ni kwamba sheria za nchi zina kinzana na sheria za jamii iwe za jadi au za dini. Sheria za nchi zinalazimishwa kwa jamii ambayo tayari ina sheria zake zilizohifadhiwa tangu dahari. Je, inawezekana kupata suluhu au kuzilinganisha?

Vyombo vya habari viko njia panda kwa sababu mitazamo hasi pande zote ni gurudumu lililopata pancha huwezi kwenda popote. Jamii inatumia vigezo vyake ili haki itendeke haraka kwani haki inayocheleshwa ni haki inayominywa. Serikali inachukua muda mwingi kwa sababu haki inayo harakishwa ni haki inayozikwa.

Tunahitaji muda wa kutosha kuelewa maana halisi ya urithi wa utamaduni wetu kabla ya kupitisha sheria kwani uchawi ni suala mtambuka. Inabidi tulenge mbali na sio kupiga filimbi za tahadhari; wachawi na uchawi wako kijiditali sasa.

Tumegawanyika sana, je, tutaweza kuainisha anuai ya vyombo vya habari, vyama vingi vya siasa, asasi nyingi za kila aina ya imani na wadau wa maendeleo na sera zinazokinzana na maslahi yetu? Au tulipulize liende na upepo?

## Milioni 3 wachanja chanjo ya UVIKO-19

**Na Romana Mallya**

IDADI ya wananchi Mkoa wa Dar es Salaam waliochanja chanjo ya UVIKO-19 imeongezeka na kufikia watu milioni 3.4 kulinganisha na milioni 3.3 waliochanja awali.

Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla alibainisha hayo jana wakati wa matembezi ya hiari yaliyoandaliwa na Hospitali ya Aga Khan, Umoja wa Ulaya (EU) kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa ya Maendeleo ya Aga Khan (AKDN) yenye lengo la kukuza uelewa na mwitikio kuhusu chanjo.

Makalla alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kuendelea kuchanja chanjo ya UVIKO-19 ili kulinda afya zao na kuondokana na madhara mabaya yanayoweza kujitokeza kutokana na kutochanja huku akizitaka taasisi ziendelee kuelimisha umma kuhusu umuhimu wake.

"Ninawapongeza Aga Khan mwendelee kuhamasishana wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19, niwapongeze EU kwa kushirikiana na serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya afya," alisema.

Makalla alisema EU imeshirikiana na serikali, Wizara ya Afya na Mkoa wa Dar es Salaam kukarabati jengo la wazazi katika Hospitali ya Rufani ya Amana na kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya.

Awali Mkurugenzi wa Tiba, Huduma za Aga Khan Tanzania, Dk. Harrison Chuwa alisema Mtandao wa Mashirika ya Kimataifa ya Aga Khan waliingia makubaliano ya mradi wa paund milioni 9.4, unaolenga kuboresha miitikio ya kimfumo na ambayo inazingatia jinsia, ili kushinda madhara ya kiafya, kiuchumi na kijamii yaliyosababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19 katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Msumbiji.

Alisema kupitia huduma za Aga Khan Tanzania na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Aga khan, utahudumia watu zaidi 700,000 kwa kutekeleza mikakati ya kukabiliana na UVIKO-19 kwa wanaume na wanawake walio hatarini na kuunda mfumo wa utoaji huduma za afya kwa ajili ya usimamizi fanisi wa UVIKO-19.

"Utaimarisha ustahimilivu wa asasi za kiraia, utaimarisha mifumo ya afya na utawafikia vijana kwa upande wa afya na shughuli za kiuchumi," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema mwitikio wa uchanjaji kwa mkoa huo ni mkubwa na kutaka kasi ya uhamasishaji na uelimishaji wa jamii kuhusu umuhimu wake.

Dk. Mfaume aliwashukuru Aga Khan kwa kuja na miradi huo wa kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kama vile saratani na magonjwa ya moyo na figo.

Pia aliwashukuru kwa kufanya ukarabati katika Hospitali ya Rufani Amana katika jengo la kuhudumia wagonjwa wa dharura wa mifumo ya upumuaji na kuweka vifaa vya kisasa pamoja na kuwajengea uwezo watumishi namna ya kutumia mashine hizo na namna ya kutoa huduma vizuri.

# Madonna atoa siri ya kutozeeka

**LOS ANGELES,** Marekani

NYOTA wa kike wa muziki wa Pop wa Marekani, Madonna, amesema siri kubwa ya yeye kuonekana bado msichana mrembo ni kwa sababu anashiriki tendo la ndoa mara kwa mara.

Akizungumza katika kipindi cha Finally Enough Talk: 50 Questions With Madonna, amedai licha ya umri wake wa miaka 64, lakini anaonekana bado mrembo.

Ikumbukwe kwa mara ya kwanza Madonna aliolewa na Sean Penn Agosti 16, 1985 ambayo ni siku yake ya kuzaliwa na wakadumu hadi mwaka 1989 walipoachana, mwaka 2000 alikuja kuolewa tena na Guy Ritchie na kudumu hadi mwaka 2008 walipotengana.

Akitoa fursa kwa mashabiki wake kumuuliza maswali, Madonna alisema miongoni mwa maamuzi ambayo aliwahi kuyachukua maishani mwake na kujutia hadi kutamani muda urudi nyuma aweze kurekebisha, ni suala la kuolewa tena katika ndoa mbili ambazo zote zimevunjika.

Madonna alijaliwa mtoto wake wa kwanza, Lourdes Oktoba 14, 1996 na aliyekuwa mpenzi wake na mkufunzi wa mazoezi ya viungo, Carlos Leon.

Kwa sasa mwanawe Lourdes ni mwanamitindo aliyefanikiwa kwa kiasi chake, amefanya kazi katika kutangaza bidhaa za urembo za Rihanna, Savage x Fenty, huku akitokea kwenye kava za majarida makubwa kama Vogue na Vanity Fair.






# DIAMOND AFUNGUKA KUMALIZANA NA RAYVANY

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Wasafi Classic Baby (WCB), Nasibu Abdul 'Diamond Platnumz' amesema, wakati aliyekuwa msanii wake Rayvanny anataka kuondoka walitofautiana kidogo, lakini walishamaliza.

Diamond alizungumza hayo kwenye jukwaa la Acces lililowakutanisha wadau wa sanaa jijini Dar es Salaam ambapo mfalme huyo wa Bongo Fleva alikuwa miongoni mwa wazungumzaji na alipokuwa akizungumza kuhusu fursa za mitandao ndipo alipomgusia Rayvanny.

"Rayvanny kama mnavyojua alindoka WCB, namshukuru Mungu ananiheshimu, tulitofautiana kidogo kama unavyojua mnapoachana kunakuwa na vitu wakati mwingine inaweza visiende sawa, lakini namshukuru Mungu tulimaliza vizuri.

"Kama unaona ameenda WCB anafanya kazi ya muziki na wimbo wake wa kwanza amenishirikisha mimi," alisema Diamond.

# *Ray aibuka upya*

**Na Mwandishi Wetu**

MKONGWE wa Bongo Muvi, Vincent Kigosi 'Ray', amesema anashangaa watu wanaosema kuwa alikuwa akibebwa na marehemu Steven Kanumba na sasa anakuja kivingine.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati akitangaza dili lake jipya na kampuni ya ulinzi nchini 4SSecurity kama balozi mpya wa kampuni hiyo, alisema Bongo Muvi kwa sasa imeshindwa kuzalisha vipaji vipya.

"Watu wanasema nilikuwa nabebwa na Kanumba, wakati Kanumba alitokea kwenye mikono yangu," alisema Ray.

"Waigizaji kama Ireen Uwoya, Jacqueline Wolper, Johari na wengine kibao wakubwa kama Thea walitokea kwenye mikono yangu.

"Kudumaa kwa tasnia ya uigizaji nchini ni kwa sababu ya kutokuzalishwa kwa waigizaji wapya wenye vipaji vya kufikia levo za kina Wema Sepetu."

Mbali na hili Ray amedokeza ujio wa kazi zake mpya na kubwa na amesema anarudi kwenye sanaa kuiboresha upya kwa kuleta vipaji vipya kwa sababu ana karama hiyo ya kuviibua.



# NBC YAKABIDHI ZAWADI ZA OKTOBA KWA SABILO, NABI

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambao ni wadhamini Wakuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara (NBC Premier League) wamekabidhi zawadi ya pesa na tuzo kwa mchezaji bora wa ligi hiyo wa mwezi Oktoba, Sixtus Sabilo kutoka Mbeya City pamoja na kocha bora wa mwezi huo, Nasreddine Nabi wa Yanga.

**Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika juzi muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo kati ya Yanga na Mbeya City FC uliofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mchezo ambao ulikamilika kwa Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa mshambuliaji wa timu hiyo, Fiston Mayele aliyetupia yote mawili.**

Katika makabidhiano ya zawadi hizo, ilishuhudiwa Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru, akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja pamoja na tuzo sambamba na king'amuzi cha Azam kwa kila mmoja, Nabi na Sabilo.

"Kimsingi ni kwamba sisi kama wadhamini wa ligi hii tunaendelea kujivunia sana kuona ligi yenye ushindani na viwango bora vya kiuchezaji vinavyoendelea kuonekana kwenye ligi hii. Ndio maana utaona kwamba pamoja na ligi kuwa na wachezaji wengi wa kigeni bado wachezaji wazawa wanapambana na kufanya vizuri na wanachukua tuzo hizi. Huu ni uthibitisho kwamba klabu zote kwa sasa zinaweza kuhudumia vema wachezaji wake kiasi cha kuweza kutoa ushindani unaotakiwa," alisema.

Ndunguru, alisema NBC inaendelea na mikakati mbalimbali kuhakikisha timu hizo zinanufaika zaidi na udhamini wa benki hiyo kwenye ligi hiyo ambayo hadi sasa imetoa ajira na kipato kwa watu zaidi ya 12,000.

Aliitaja mikakati mbalimbali ikiwamo mikopo ya mabasi kwa klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo ili kurahisisha usafiri, mpango ambao upo kwenye hatua za mwisho za utekelezwaji.

"Na jitihada zetu hizi haziishii kwenye mchezo wa soka tu, bali pia michezo mingine ikiwamo gofu na mchezo wa riadha ambapo kupitia NBC Dodoma Marathon inayofanyika kila mwaka jijini Dodoma, tumekuwa tukikusanya fedha kwa ajili ya elimu na matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi changamoto ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya kinamama.

"Kupitia jitihada hizo hadi sasa zaidi ya wanawake 9,000 wamefanya vipimo na kati yao 500 wamegundulika kuwa na saratani hiyo na wameshaanza matibabu kwa kushirikiana na Taasisi Ya Saratani Ocean Road(Orci)," alisema.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja pamoja na tuzo kwa mshambuliaji wa Mbeya City, Sixtus Sabilo, baada ya kutangazwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara (NBC Premier League) kwa mwezi Oktoba, wakati wa mechi kati ya timu hiyo na Yanga iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Mchezo huo ulimalizika kwa Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Pluijm atoa mkakati Singida Big Stars*

**Hadija Mngwai na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm amefunguka kuwa yupo kwenye Ligi Kuu Bara kushindana na si kushiriki, hivyo mkakati wake ni kuhakikisha anatwaa pointi tatu katika kila mchezo.

Singida Big Stars ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 24 ikicheza michezo 13 ikiwa nyuma ya Simba yenye pointi 28.

Katika ligi hiyo, Singida Big Stars iliyopanda daraja msimu huu ni moja ya timu ambazo zimekuwa zikitoa ushindani mkubwa kwenye.

Akizungumza na Nipashe jana, Pluijm, alisema wanahitaji kujipanga zaidi ili kuweza kupata matokeo mazuri kwa kuwa yupo kwenye ushindani.

"Tupo kwenye ligi kushindana na si kushiriki, tunajipanga ili kuweza kushinda kila mchezo uliokuwa mbele yetu, kila mchezo kwetu tunacheza kama fainali.

"Tunahitaji kumaliza ligi tukiwa katika moja ya nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, kikosi kipo vizuri wachezaji wana morali," alisema Pluijm.

Kauli hiyo ya Pluijm imekuja baada ya juzi kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, jambo ambalo mshambuliaji wa timu hiyo Amissi Tambwe alisema wamejiwekea malengo ya kushinda mechi zao nyumbani, na zile za ugenini wafanye kila njia walau kupata pointi moja.

"Tumeambizana wenyewe wachezaji kuwa tukicheza nyumbani tushinde na ugenini tupate walau pointi moja na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa mpaka sasa, ila wakati mwingine inatusumbua kwa sababu ya uchovu wa safari.

"Watu wanasema kwenye mechi dhidi ya Yanga hatukucheza vizuri, lakini hata hii pia hatukucheza vizuri kwa sababu ya uchovu wa safari, tulitoka Singida, tukaja Dar kucheza na Yanga, halafu tukarudi Singida, tumekuja tena Dar kucheza na Ruvu Shooting, tunachoka sana," alisema Tambwe, mchezaji wa zamani wa Simba na Yanga.

Mfungaji wa bao pekee kwenye mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, Frank Zacharia alisema ni maandalizi mema ndiyo yanayowafanya kufanya vema kwenye mechi za hivi karibuni, akiahidi kufunga mabao zaidi mechi zijazo.

## Vishale 'kurushwa' Nairobi Februari

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Afrika ya mchezo wa vishale yanatarajiwa kufanyika Februari 17, mwakani jijini Nairobi, Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Vishale Tanzania, Redemta Mwebesa, alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi zote za Afrika na kwamba wanaendelea vizuri na maandalizi.

Mwenyekiti huyo aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kujiunga na mchezo huo kwa kuwa hauna tofauti na michezo mingine huku akihimiza vyama vya wilaya na mikoa kufanya chaguzi zao.

"Tunawasisitiza viongozi wa vyama vya michezo vya wilaya na mikoa kuhimiza watu wao wafanye uchaguzi kwa kuwa chama kinahitaji kufanya kazi na viongozi wenye weledi," alisema mwenyekiti huyo.

## TPBRC yageukia rushwa ulingoni

**Na Hadija Mngwai**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania imesema kwa sasa imejipanga kikamilifu kuondoa rushwa katika mchezo huo ili kuwavutia wadau mbalimbali kuupenda mchezo huo hapa nchini.

Mchezo wa ngumi ni wa pili kupendwa hapa nchini baada ya soka jambo ambalo uongozi huo umeona ni unapaswa kusimamia sheria na kanuni ipasavyo kwa kuhakikisha unaondoa madai ya kuwapo kwa rushwa katika baadhi ya mapambano.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu Kamisheni ya Ngumi za kulipwa nchini (TPBRC), Yahya Poli, alisema kuna madai ya kuwapo kwa rushwa ambayo wamekuwa wakisikia katika baadhi ya mapambano, hivyo wanajitahidi kufuatilia ili kutokomeza taswira hiyo mbaya inayotaka kuchafua mchezo huo pendwa nchini.

"Tumekuwa tukipata tetesi za suala la rushwa katika mchezo huu, jambo ambalo tumekuwa tukijitahidi kuliondoa ili kuwe na haki kwa kutumia semina mbalimbali tunazotoa.

"Mfano semina iliyomalizika hivi karibuni tulikuwa na waamuzi kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo Iringa, Njombe, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na Pwani, wote tumewaeleza umuhimu wa mchezo wa ngumi na kuondoa rushwa katika mchezo huu," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO MKATABA MNONO

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, amepewa ofa ya mkataba mnono wa miaka mitatu wenye thamani ya pauni milioni 186 na Klabu ya Saudi Arabia, Al Nassr. ***(CBS)***

### RICE ATAKIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imeingia katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 23. ***(El Nacional, via Fichajes)***

### KANE MAMBO BADO SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur bado haijaanza mazungumzo na nahodha na mshambuliaji wa England, Harry Kane, 29, kuhusu mkataba mpya, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika msimu wa majira ya joto wa mwaka 2024. ***(ESPN)***

### HAG ATAKA UNITED ISAJILI

KOCHA Erik ten Hag ameiomba Manchester United kufanya usajili katika dirisha la Januari ili kupata mrithi wa Cristiano Ronaldo. Katika orodha fupi ya usajili ya klabu hiyo yumo winga wa PSV na Uholanzi, Cody Gakpo, 23 na mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, 23. ***(ESPN)***

### LIVERPOOL NAO KUSAJILI

LIVERPOOL pia wapo tayari kutumia fedha nyingi katika usajili ujao wa Januari, licha ya kutokuwa na uhakika kuhusu umiliki wa klabu. ***(Football Insider)***

### UNITED NA BELLINGHAM

KLABU ya Manchester United imerudi nyuma katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 19, kutoka Borussia Dortmund. ***(Sky Sports)***

### MESSI ATAKIWA MAREKANI

KAMISHNA wa Ligi Kuu ya soka ya Marekani, Don Garber amethibitisha kuwa klabu kadhaa katika ligi hiyo zina nia ya kumsajili mshambuliaji Lionel Messi, 35, wakati mkataba wake na Paris St-Germain utakapokamilika mwishoni mwa msimu. ***(90Min)***

### BALDE SASA AJIPIGIA DEBE

MLINZI wa kushoto wa Barcelona, Alejandro Balde, 19, ameitaja Manchester United kuwa klabu ambayo angependa kuichezea ukiacha timu yake ya LaLiga. ***(Mundo Deportivo)***

### DURAN AGOMBEWA EPL

KLABU za West Ham na Everton zimejiunga katika harakati za kuwania saini ya winga wa Colombia, Jhon Duran, 18, kutoka Chicago Fire, lakini Liverpool na Manchester United pia zinamtaka. ***(Sun)***

### MCKENNIE AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua kiungo wa Juventus, Weston McKennie, 24, baada ya kumalizika kwa Kombe la Dunia. ***(CBS, via Express)***

### DIA ANYATIWA LEEDS

LEEDS United, Everton, West Ham na Leicester City ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mshambuliaji wa Senegal, Boulaye Dia, 26. Mchezaji huyo kwa sasa yuko kwa mkopo Salernitana akitokea Villarreal. ***(CBS)***

## DONDO SOKA MAGAZ ULAYA




# MESSI: ARGENTINA SASA NDIO IMEANZA KOMBE LA DUNIA

**● ● ● Kulikuwa na sababu nyingi nyuma ya kushindwa kwa Saudi Arabia, kama vile wachezaji...**

**DOHA,** Qatar

LIONEL Messi amesema kampeni ya Argentina ya Kombe la Dunia sasa imeanza rasmi baada ya kuiwezesha timu yake kushinda mabao 2-0 dhidi ya Mexico ili kuzuia kuondolewa mapema katika mashindano hayo.

**Baada ya kichapo cha 2-1 kutoka kwa Saudi Arabia katika mechi yao ya ufunguzi ya Kundi C, Argentina waliingia katika mpambano wa Jumamosi na Mexico wakijua kushindwa kutawafanya washindwe kusonga mbele.**

Vijana wa kocha Lionel Scaloni walikuwa na ugumu wa kushambulia katika kipindi cha kwanza katika mechi hiyo iliyopigwa dimba la Lusail kabla ya Messi kufunga kwa shuti la umbali wa yadi 25.

Fowadi huyo wa Paris Saint-Germain kisha akamtengenezea pande Enzo Fernandez aliyetokea benchi na kufunga bao la pili kwa Argentina, ambao wanaungana na Saudi Arabia wakiwa na pointi tatu.

'La Albiceleste' hao watakutana na Poland, ambao wako pointi moja zaidi kileleni, katika mchezo wao wa mwisho na watahakikishiwa kutinga hatua ya 16-bora kwa ushindi, wakati sare pia inaweza kutosha.

Messi alifurahia kujibu kichapo dhidi ya Saudi Arabia, lakini akasisitiza bado kuna kazi kubwa ya kufanya ikiwa wanataka kutinga hatua ya mtoano.

"Kombe jingine la Dunia limeanza kwetu leo," alisema.

"Kulikuwa na sababu nyingi nyuma ya kushindwa kwa Saudi Arabia, kama vile wachezaji kucheza kwenye Kombe la Dunia la kwanza na ratiba.

"Hicho si kisingizio, lakini tulijua lazima tushinde leo (juzi), tulilazimika kucheza kama tulivyocheza kwa sababu Mexico ilifanya vizuri na ina kocha mzuri.

"Tulitulia zaidi katika kipindi cha pili na kupata bao tulilohitaji. Hatuwezi kukata tamaa sasa; tuna fainali kuanzia wakati huu na hatuwezi kufanya makosa."

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or alifikisha mabao nane kwenye kinyang'anyiro hicho, hivyo kumfanya kuwa sawa na Diego Maradona na nyuma ya Gabriel Batistuta (10) pekee wa Argentina.

Yeye ndiye mchezaji mdogo zaidi (miaka 18, siku 357 dhidi ya Serbia mwaka 2006) na mchezaji mkubwa zaidi (miaka 35, siku 155 dhidi ya Mexico) kufunga na kusaidia bao katika mchezo mmoja wa Kombe la Dunia tangu rekodi hizo zilipoanza mwaka 1966.

Ushindi huo wa Argentina ulipatikana mbele ya umati wa watu 88,966, na huo ndio ulikuwa wa juu zaidi kwa mechi ya Kombe la Dunia la wanaume tangu fainali ya mwaka 1994 kwenye Uwanja wa Rose Bowl jijini California nchini Marekani (94,194).

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PORTUGAL
VERSUS
URUGUAY
1 | 1.94
X | 3.35
2 | 3.90

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CASEMIRO: BRAZIL INAWEZA KUSHINDA BILA NEYMAR

**DOHA, Qatar**

CASEMIRO ana imani kuwa Brazil inaweza kushinda bila Neymar kwa sasa kwani alimuunga mkono "nyota wa timu" ili kuwa fiti kwa wakati kwa ajili ya mwisho wa biashara ya Kombe la Dunia.

Jeraha la kifundo cha mguu lilimlazimu Neymar kubadilishwa dakika ya mwisho katika ushindi wa 2-0 wa Brazil dhidi ya Serbia Alhamisi iliyopita.

Richarlison alifunga mabao yote mawili ya Brazil na kiwango cha mshambuliaji huyo wa Tottenham Hotspur ni sababu moja inayompa moyo kiungo mkabaji Casemiro.

Neymar bila shaka atakosa mchezo dhidi ya Uswisi leo, Jumatatu na kuna uwezekano mkubwa akakosa pia mechi dhidi ya Cameroon Ijumaa.

Iwapo atapona kwa wakati ili kushiriki katika hatua ya mtoano bado haijajulikana, lakini Brazil wana matumaini.

Casemiro, aliyenukuliwa na gazeti la Globo la Brazil, alisema: "Ikiwa tutaendelea kuzungumza kuhusu Neymar, tutakaa hapa kwa siku, kwa sababu ya umuhimu wake.

"Yeye ndiye nyota wa timu, ambaye analeta mabadiliko. Lakini tuna wachezaji wengine sawa: Raphinha, Vini (Vinicius Junior), Richarlison. Tuna chaguzi mbalimbali.

"Neymar ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, na kwa bahati mbaya hatakuwapo kwenye mchezo ujao, lakini tuna wachezaji wenye ubora wa kuchukua nafasi yake, lakini bila shaka si katika kiwango chake."

Casemiro alimtaja Lucas Paqueta wa West Ham kama mchezaji ambaye anaweza kuingia kwenye kikosi cha kwanza na kuleta utofauti kwa kukosekana kwa Neymar.

"Ni mchezaji mwingine muhimu," Casemiro alisema. "Ana nguvu sana. Anacheza vizuri sana."



# 'Mbappe ndio kila kitu Ufaransa'

**DOHA, Qatar**

KYLIAN Mbappe anacheza soka "kama treni ya umeme" na alionyesha sifa zake za uongozi tulivu kwa mabao mawili yaliyoivusha Ufaransa katika raundi ya mtoano ya Kombe la Dunia, amesema Kocha Didier Deschamps.

'Les Bleus' hao walipata ushindi wa 2-1 dhidi ya Denmark shukrani kwa mabao ya fowadi huyo, na hivyo kujihakikishia kusonga mbele kutoka Kundi D baada ya ushindi wa ufunguzi dhidi ya Australia.

Baada ya kuumia kwa Karim Benzema, Mbappe aliwasili Qatar akitumainiwa zaidi kuibeba Ufaransa.

"Yeye ni kiongozi," alisema Deschapms. "Sidhani kama uongozi una sura moja. Kylian haongei, si mzungumzaji sana. Hata hivyo, ni kama treni ya umeme uwanjani.

"Kylian daima ana jukumu sawa. Anajua timu ya Ufaransa inamhitaji, na tunamhitaji kuwa katika ubora wake. Uthibitisho umeonyeshwa katika michezo miwili ya kwanza."



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# JKT, KITAYOSCE, FOUNTAIN GATE ZATOANA MACHO CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Champioship ambayo itatoa timu zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, inazidi kupamba moto huku timu za JKT Tanzania, Kitayosce na Fountain Gate 'zikitoana macho' kusaka nafasi ya kupanda moja kwa moja bila kupitia mechi za mchujo.

Juzi, kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, JKT Tanzania ambayo ilishindwa kutinga Ligi Kuu msimu huu ilipofungwa kwenye mechi ya 'play off' dhidi ya Prisons, inaonekana haitaki masihara baada ya kuitwanga African Sports bao 1-0 lililofungwa na Ally Makarani na kuzidi kujishindilia kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo iliyo kwenye raundi ya 11, ikifikisha pointi 28.

Timu ya Kitayosce ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Mwandui Complex, Shinyanga, iliachia kipigo kizito cha mabao 4-0 dhidi ya wenyeji Gwambina, yakiwekwa wavuni na Jerome Lambele, Fabrice Ngoyi, Daniel Lukandamila na Mbelenge Ngulakwey.

Matokeo hayo yameifanya kukamata nafasi ya pili kwenye msimamo kwa pointi zake 26. Fountain Gate inashikilia nafasi ya tatu ikiwa na pointi 24 baada ya kuifumua Mbuni FC mabao 2-1, mechi ikipigwa Uwanja wa CCM Gairo Morogoro. Mabao ya washindi yalifungwa na Salim Aiyee, huku Pamba nayo ikionekana kuzinduka baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 ugenini katika Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma dhidi ya Mashujaa.

## NIMEMALIZA...



Mmoja wa wahitimu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, akicheza kwa furaha katika Mahafali ya 17 ya chuo hicho yaliyofanyika chuoni hapo Kigamboni, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kocha Nabi apiga mbili

INATOKA UK. 32

kumu ninayowapa na kila mmoja kutambua wajibu wake na hata waliokuwa benchi wanakuwa makini na utayari wa kucheza muda wowote, wanatakiwa kuonyesha kila ninachowapa katika uwanja wa mazoezi," alisema.

# CHAMA, PHIRI BALAA SIMBA

INATOKA UK. 32

Polisi Tanzania kukusanyika pamoja kwa ajili ya kuuzuia mpira huo uwababue, lakini hakufanya hivyo, badala yake wakaachia nafasi kwa wachezaji wengine waliokuwa huru, akaupeleka kwa mfungaji aliyeujaza wavuni kirahisi.

Kipindi cha pili timu ziliendelea kushambuliana kwa zamu na dakika ya 52 Simba iliandika bao la tatu ambalo pia Chama akihusika. Akiwa kwenye wingi ya kushoto aliingia ndani kidogo na kuonekana kama atafunga yeye, lakini akapiga pasi ambayo kama Pape Sakho angekuwa makini angeuweka wavuni, lakini akaukosa, ukamkuta Phiri aliyeukwamisha nyavuni kwa mara nyingine na mguu wa kushoto kama alivyofunga la kwanza.

Mabadiliko ya kumtoa Kipagwile na kumuingiza Ambrose Awio na Simba kuwatoa Gadiel Michael na Bocco, wakaingia Kibu Denis na Kennedy Juma yaliisaidia zaidi Polisi Tanzania na kufanikiwa kupata bao la kufutia machozi dakika ya pili ya nyongeza kabla ya mechi kumalizika kupitia kwa Zuberi Hamisi akiunganisha krosi ya Awio, huku kipa Manula akiwa ametoka langoni.

Polisi Tanzania inaendelea kubaki na pointi zake tisa ikiwa kwenye nafasi ya 14 kwa mechi 14 ilizocheza.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 28/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1526 | Keshla FK vs Kapaz | 1.96 | 3.26 | 3.55 |
| 13:00 | 2008 | Cameroon vs Serbia | 4.90 | 3.60 | 1.70 |
| 13:00 | 3835 | Lernayin Artsakh vs Van Yerevan | 2.57 | 2.91 | 2.72 |
| 14:00 | 3824 | Kagera Sugar vs Mtibwa Sugar | 2.04 | 2.86 | 3.84 |
| 14:00 | 4219 | Oleksandria vs Rukh Vinnyky | 1.64 | 3.69 | 4.56 |
| 15:00 | 5546 | FC Kryvbas Kriviy Rih vs SC Dnipro 1 | 5.64 | 3.99 | 1.49 |
| 16:00 | 1803 | Marines FC Gisenyi vs AS Kigali | 5.63 | 3.40 | 1.59 |
| 16:00 | 2215 | O F Ierapetras vs Proodeftiki FC | 1.94 | 3.16 | 3.74 |
| 16:00 | 3769 | South Korea vs Ghana | 2.45 | 3.05 | 3.00 |
| 16:00 | 4016 | Al Jahra vs AL Sahel | 1.71 | 3.69 | 4.08 |
| 16:00 | 4474 | Estrela Amadora U23 vs CD Mafra U23 | 1.65 | 3.99 | 4.09 |
| 16:00 | 5044 | KMC vs Tanzania Prisons | 1.82 | 3.02 | 4.57 |
| 16:00 | 5148 | FC Famalicao U23 vs Gil Vicente FC U23 | 2.37 | 3.36 | 2.63 |
| 16:00 | 5438 | Wakiso Giants FC vs Express FC | 2.17 | 3.15 | 3.45 |
| 16:00 | 5793 | AL Nasr vs AL Tadamon | 2.44 | 3.03 | 2.78 |
| 16:15 | 5342 | Kifisias vs Kallithea FC | 2.40 | 2.73 | 3.17 |
| 16:30 | 2665 | Mekelakeya vs Ethiopia Electricity | 1.97 | 3.21 | 3.55 |
| 16:30 | 4944 | Minerva FC vs Aizawl FC | 1.84 | 3.50 | 3.70 |
| 17:00 | 3722 | Recreativo DO Libolo vs Wiliete SC | 1.91 | 3.06 | 3.98 |
| 17:00 | 5162 | CD Lunda Sul vs Bravos Maqui | 1.95 | 2.92 | 4.08 |
| 18:00 | 2555 | SL Benfica W vs SC Braga W | 1.58 | 3.90 | 4.77 |
| 18:00 | 2874 | Karabakh vs Zira | 1.10 | 7.77 | 16.52 |
| 18:30 | 2871 | Ethiopian Medhin vs Hawassa Kenema SC | 1.95 | 3.74 | 3.11 |
| 18:30 | 4684 | ES Bafing vs Club Omnisports de Korhogo | 1.63 | 3.56 | 4.88 |
| 19:00 | 4377 | Brazil vs Switzerland | 1.48 | 4.20 | 6.40 |
| 20:00 | 1219 | Altinordu vs Manisa BBSK | 3.12 | 3.31 | 2.09 |
| 20:00 | 2478 | Aris Limassol vs Pafos FC | 2.80 | 3.20 | 2.50 |
| 20:00 | 2752 | Olympiakos Nicosia vs Nea Salamis | 2.59 | 3.19 | 2.69 |
| 21:00 | 1231 | Miercurea Ciuc vs ACS Viitorul Selimbar | 1.63 | 3.46 | 5.07 |
| 21:00 | 1596 | Lommel U21 vs Kmsk Deinze U21 | 1.60 | 4.46 | 3.98 |
| 21:00 | 4622 | Parma Calcio vs Inter Milan W | 6.19 | 4.74 | 1.37 |
| 21:30 | 2405 | AS Eupen U21 vs Westerlo U21 | 1.59 | 4.10 | 4.39 |
| 21:30 | 3721 | Oostende U21 vs Waasland Beveren U21 | 1.51 | 4.38 | 4.77 |
| 21:30 | 4087 | Kortrijk U21 vs St Truiden U21 | 4.49 | 4.10 | 1.58 |
| 22:00 | 2343 | Portugal vs Uruguay | 1.94 | 3.35 | 3.90 |
| 22:00 | 3659 | Lierse SK U21 vs Excelsior Virton U21 | 1.82 | 4.00 | 3.32 |
| 22:00 | 5541 | FCV Dender EH U21 vs RWD Molenbeek U21 | 2.49 | 3.76 | 2.31 |
| 22:30 | 1087 | Arzignanochiampo vs Vicenza | 3.05 | 3.20 | 2.32 |
| 22:30 | 1244 | UE Santa Coloma B vs UE Engordany B | 1.72 | 3.84 | 3.88 |
| 22:45 | 1563 | Hitchin Town vs Redditch United | 2.70 | 3.60 | 2.35 |
| 22:45 | 2197 | Carshalton Athletic vs Billericay Town | 2.23 | 3.60 | 2.68 |
| 22:45 | 4776 | Ayr United vs Pollok | 1.21 | 6.02 | 9.12 |
| 23:00 | 1385 | UD Ibiza Eivissa vs FC Andorra | 2.87 | 2.97 | 2.53 |
| 23:00 | 5256 | Chateauroux vs Le Mans | 2.13 | 3.25 | 3.25 |

JUMANNE - 29/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 18:00 | 1571 | Ecuador vs Senegal | 2.39 | 3.09 | 3.04 |
| 18:00 | 4481 | Netherlands vs Qatar | 1.16 | 7.01 | 15.02 |
| 22:00 | 1541 | Wales vs England | 6.58 | 4.14 | 1.48 |
| 22:00 | 4843 | Iran vs USA | 4.00 | 3.40 | 1.90 |
| 23:45 | 1184 | Santa Clara vs Oliveirense | 1.56 | 3.84 | 5.06 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Novemba 28, 2022

Nipashe





UKURASA 29

## Messi: Argentina sasa ndio imeanza

HESABU...




Beki wa kati wa Ubelgiji, Jan Vertonghen (kushoto), akipiga hesabu namna ya kumdhibiti mshambuliaji wa Morocco, Youssef En-Nesyri, kwenye mechi ya Kundi F ya Kombe la Dunia iliyopigwa nchini Qatar jana na Morocco kushinda 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# CHAMA, PHIRI BALAA SIMBA

## ●●●Waifyeka Polisi Tanzania, huku Bocco akiendelea tena kuwasha moto wa mabao...

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA wa Simba, nahodha John Bocco na Mzambia Moses Phiri, jana walifunga mabao matatu yaliyoiwezesha Simba kuibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Phiri alifunga mawili yaliyomfanya kufikisha mabao nane kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu, mawili nyuma ya kinara, Mkongomani Fiston Mayele wa Yanga mwenye mabao 10.

Bao la Bocco limemfanya kufikisha mabao manne kwenye Ligi Kuu baada ya kufunga mabao matatu Novemba 19, mwaka huu kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, Simba ikishinda mabao 4-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ni ushindi ulioipeleka kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa ligi ikifikisha pointi 31, moja nyuma ya vinara Yanga wenye alama 32 mpaka sasa.

Kuendelea kukaa nafasi ya pili kwa Simba kutatokana na mechi ya jana usiku ambapo Azam FC ilikuwa ikicheza na Coastal Union kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Kama Azam yenye pointi 29 itatoa sare ama kupoteza basi Simba itaendelea kuwa kwenye nafasi hiyo, lakini ikishinda itakuwa imeshuka tena hadi nafasi ya tatu

Simba ilianza mechi kwa kasi na kama Bocco angekuwa makini angeweza kufunga bao dakika ya kwanza tu, lakini alinyang'anywa mpira na Chilo Mkama akiwa ndani ya eneo la hatari.

Dakika ya tatu, Moses Phiri aliupata mpira uliokuwa umeokolewa na mabeki wa Polisi Tanzania walioruka juu na Bocco, na akiwa nje kidogo ya boksi alipiga shuti lililopaa juu.

Kuona hivyo, Polisi Tanzania ilishtuka na kuanza kujibu mashambulizi hayo, na nusura ipate bao dakika ya 10, wakati Idd Kipwagile alipowatoka mabeki wa wageni wao, akampasia Vitalis Mayanga ambaye aliachia shuti, lakini Aishi Manula akikaa imara na kulidaka.

Dakika tatu baadaye, Mayanga aliikosesha tena timu yake bao baada ya kuukosa mpira wa krosi uliyopigwa na Kipwagile.

Sadio Kanoute alikaribia kufunga bao dakika ya 29, alipounganisha mpira na kona wa Clatous Chama, lakini kichwa chake cha kudundisha kilipaa juu ya lango la Polisi Tanzania.

Ndipo ulipokuja muda ambao wanachama na mashabiki wa Simba walikuwa wanausubiria, ambapo Bocco alipoiandikia bao la kwa dakika ya 32.

Mpira ulianzia kwa Mzamiru Yassin akaupeleka kwa Shomari Kapombe naye akammegea pande Chama, lakini mchezaji huyo aliuruka mpira uliomkuta mfungaji akiwa kwenye eneo zuri akaachia fataki lililokwenda kulia kwa kipa Jeremiaha Kisubi na kujaa wavuni.

Dakika mbili kabla ya mapumziko, Phiri alipachika bao la pili kwa Simba baada ya mpira mrefu kumkuta Chama akiwa kwenye nafasi nzuri, lakini akiwa amezungukwa na mabeki wa Polisi Tanzania, akatishia kama anapiga na kuwafanya mabeki wa

INAENDELEA UK. 31

## Nabi apiga mbili kwa moja Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anaendelea kujenga timu yake kuwa imara zaidi kwa ajili ya kuleta ushindani mkubwa katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kuelekea hatua ya makundi.

Nabi aliyasema hayo juzi baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kushinda 2-0, shukrani zikimwendea mshambuliaji Fiston Mayele aliyetupia yote mawili

Kocha huyo alisema anashukuru kwa ushindi walioupata kwa sababu ya nidhamu ya wachezaji wake kwa kumuheshimu mpinzani na kujituma kuhakikisha wanapata pointi tatu zinazowawezesha kuendelea kupambania malengo yao.

Alisema licha ya timu yake kuonyesha ushindani katika ligi hiyo, bado haijafikia asilimia anazohitaji kwa ajili ya kwenda kushindana na timu ambazo atakutana nazo katika hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tunatambua tunafanya vizuri na mashabiki kuona Yanga imekamilika kwa asilimia 100, kwangu ni bado naweza kusema niko kwa asilimia 50 au 60 kwa sababu ya mashindano yaliyoko mbele yetu hasa ya Shirikisho huku kuna timu ambazo ziko imara na bora zaidi.

"Kiukweli bado hatujafikia asilimia tunayohitaji, tunatakiwa kuendelea kujiandaa taratibu ili hata tunapokuja kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho tuwe vizuri.

"Kwa sasa najivunia nidhamu ya wachezaji katika ligi hasa kwa kujituma zaidi katika huu mchezo wa leo (juzi), wamejitoa nawashukuru kwa ushindi wanastahili pongezi," alisema Nabi.

Kuhusu mabadiliko aliyoyafanya katika kikosi chake, alisema ni ili tu kuwapumzisha baadhi ya wachezaji waliotumika sana katika michezo iliyopita na kuwapa nafasi wale ambao hawaonekani mara kwa mara uwanjani.

"Mabadiliko haya ni ishara ya kila mchezaji kutambua maju-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >